# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

## RONGAI CONSTITUENCY,

## HELD AT KIBORONJO FULL GOSPEL CHURCH

## ON

**FRIDAY 12TH JULY 2002**

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, RONGAI CONSTITUENCY HELD AT KIBORONJO FULL GOSPEL ON FRIDAY 12TH JULY 20O2**

**Present**

1. Com. Domiziano Ratanya
2. Com. Salome Muigai
3. Com. Riunga Raiji

**Secretariat In Attendance**

| | |
|---|---|
| Samuel Wanjoi | Programme Officer |
| Mathew Ngugi | Assistant Programme Officer |
| Gladys Osimbo | Verbatim Recorder |

**The meeting started at 10:30 a.m. with Com. Domiziano Ratanya in the Chair.**

Hamjamboni wote wananchi, kabla hatujaanza kikao hiki ningetaka kuona huyu pastor, kama pastor yuko karibu, pastor Jackson atuongoze kwa maombi.

**Pastor Jackson**: Tunataka kuomba. Baba wetu mtakatifu, twakushukuru na twakupenda maana wewe ni mwema. Asante kwa uwezo wako, asante kwa nguvu zako ambazo zimetuweka hapa kuwa hai mpaka siku ya leo. Twakushukuru na twakuinua kwa sababu ya siku hii maana uliitenga na uliiweka kwa sababu ya kazi hii malumu ambayo iko mbele zetu. Tunapoingia kuanza mkutano huu, wa maoni yetu kuhuzu Katiba ya nchi yetu, baba twaomba msaada wako uwe pamoja na sisi. Uwezo wako utuangazie hata kila atakaye nena, Mungu uongoze mawazo ya kila moja katika jina la Yesu. Asante kwa

sababu ya viongozi wote ambao wafika mahali hapa, nasi twakushuru kwa vile umewasaidia, umewasafirisha mpaka wamefika kikaoni hiki twasema ni asante. Tunapoendelea Mungu uwezo wako wa roho mtakatifu ukatamalaki hapa, ukazunguke mawazo yetu, ukausunguke mioyo yetu hata eneo hili na jamii yote ya Kenya ukaibarikie katika jina la Yesu. Kwa hivyo mambo yote twayaweka mbele zako tukiamini ya kwamba utatuongoza, Mungu utatubariki, utatuzingira, utatulinda na uwepo wako na ni katika jina la Yesu Kristo zote twaomba na kuamini.

**Com. Domiziano Ratanya**: Sasa kabla hatujaanza ningetaka co-ordinator ama yule ambaye ameanjiwa na Co-ordinator ahanze na kutujulisha viongozi wa upande huu pamoja na ile kamiti yake inayomsaidia kwa Constitutional Review. Bwana Co-cordinator.

**Kitangi Jacob:** Commissioners na wananchi watukufu ninawasalimua hamjamboni.

**Wananchi:** Hatujambo

**Kitangi Jacob:** Ni mimi nashikilia co-ordinator wetu, ambaye atakuja kama amechelwe. Bado 3 'c hawajafika hapa. Lakini tuko na walimu wale ambao tuko nao kusaidiana kwa hii mambo, watasimama tuwaone , hawa ndio walimu ambao tuko nao wamekuwa wakifanya kazi hii kuifanikisha . Pia mimi ni mwalimu, moja wao. Asanteni. Mwenye kiti ndiye huyu hapa.

**Com. Domiziano Ratanya**: It okey wengine wakija utatuonyesha wakija baadaye, Sasa wananchi karibuni nyote kwa hiki kikao cha Tume ya kurekebisha Katiba yetu ya Kenya na kutoka sasa ningetaka kutangaza rasmi hiki sasa ni kikao cha Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya na tumeanza sasa.

Ni kuendele tu tunaindelea kwa sababu tulikuwa upande ule mwingine wa Rongai jana na sasa tumekuja upande mwingine wa Constituency hii ya Rongai. Kwa vile tunashukuru kwa sabab upande huu, watu wa upande mumekuja ili mtupatie maoni yenu. Na kabla hatujaanza sasa, ningetaka muwajue Commissioners ambao tuko hapa kwa panel yetu. Upande wangu wa kulia nina Com. Salome Muigai na upande wangu mwingine nina Commissioner Riunga Raiji. Na mimi mwenywe ninaitwa Domiziano Ndochokera Ratanya, ambaye ninakuwa mwenye kiti wa kikao hiki ya siku ya leo.

Wale wengine ambao tumeandamana nao, tuna Programme Officer wetu ambaye anashikilia office yetu, kwa sababu tuna office ya Commission hapa, tuna secretariat yetu ambayo inasimamiwa na Bwana Samuel Wanjohi, na anasaidiwa na Bwana Mathew Ngugi, ndiye huyo, na mwigine anayemsaidia ni Gladys Osimbo, wengine ambao wametusaidia kufika hapa kuongoza hii magari ni ma-drivers wetu. Sijui kama wako hapo inje ama wako karibu lakini tuna Kamau, ninamuona pale, tuna Maingi, yuko hapa karibu na Ebrahim Muthee. Kwa hivyo Karibuni tena wananchi na tutaendelea kusikia maoni yenu. Na kabla hatujafanya hivyo, kuna procedures. Ama kuna mpango ambao tumepanga ambao tutafuata.

Na ningetaka tueshimiyane kabisa kwa huu mpango nitaweleza. Ili kila mtu aweze kutuo maoni yake, tukiondoka hapa kila

mtu awe amezungumza. Kitu cha kwanza, kikao hiki, tumewambia ni cha Tume yetu ya kurekebisha Kaatiba na kulingana na sheria ambayo imetuweka, tunaruhuziwa kuchukua maoni ya wanachi na kwenda pahali popote katika Kenya kama vile tunaenda sasa round kwa Constituency zote na hakuna kuokoba. Usiokobe chochote wakati unapeana maoni yako. Uko free, sema yale maoni yako na usiokobe yeyote atakupeleka kortini ama yoyete atakufanyia chotechote. Wewe ni mwananchi wa Kenya na una uhuru kamilifi wa kusema yale unafikiria yatasaidia katika Katika yetu.

Na kitu kingine cha muhimu ni kwamba, tufikirie lugha ambayo tutatumia. Lugha yetu ambayo tunajuwa ni Kingereza ni lugha ya kwanza ambao tunatumia sana katika Kenya, na ingine ni Kiswahili, lakini ukiwa uwezi kuongea Kiswahili ama Kingereza, utakuwa na nafasi yako na una uhuru wa kuongea lugha ya mama. Lugha yeyote ambayo ni ya mama utatumia. Na tutakuwa na interpreters ambao wanatuambia vile wanasema.

Ingine ni kwamba hapa nina list, hii ni list ambayo tuna-register, tunaandikisha wale wanaingia hapa. Ili tujue ni nani atapeana maoni. Si list ya kushitaki yeyote, nikujua ni nani wanapeana maoni na ni nani yuko hapa, ili tuweze kuifuata kwa kupeana maoni. Na ndiyo list tutatumia. Ukiwa wa kwanza tutkuita kama wakwanza. Wa pili na kuendelea namna hivyo. Lakini tuna uwezo kama Tume ya kusrukia hii list kama tuna sababu yeyote. Sababu kama nikiona pengine akina mama, ama walemavu, ama wazee, wamama kwa wababa, tukiona wengine ni wezee na wanataka kupeana maoni warudi, pengine ni wagonjwa, na akina mama wapewe nafasi ama wasiojiweza, hapo tunaweza kurukia na kwenda kumuita mama moja ama mtu asiye jiweza mmoja apeane maoni yake. Ama nikiona mwanafunzi, anatoka shule na anataka kupeana maoni yake arudi, katika class, kwa hapo nitarukia na nimpe hiyo nafasi apeane maoni yake na alafu aende katika class. Na pengine hiyo haitakuwa taabu wananchi. Tnakupaliana kwa hiyo?

**Wanachi:** Tunakubali

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey, hiyo ni sawasawa na kitu kingine ningeendelea kuwajulisha kwamba, wakati wa kupeana maoni yenu, utapeana na njia hizi, njia ya kwanza, kama una maandishi ambayo umeandika, hii tunaita memorandum, na ungetaka kupeana utuwajie sisi kama Tume twende tukasome, unaweza kupatia Programme Officer wetu pale na u-sign register yetu na tutachuka hiyo memorandum yako kwenda mpaka office yetu Nairobi wakati tutarudi na tutaisoma kweli kweli, hiyo ni njia moja. Uweza kupeana tu na uende kama hutaki kusema lolote.

Lakini kama kwa hiyo memorandum, unataka kuitetea kidogo, usema yale ya muhimu katika hiyo memorandum, utapewa dakika tano. Na yale ya muhimu si kusoma memorandum, ni kusema yale unasikia ni ya muhimu kwa hiyo dakika tano kwa sababu utapewa dakika tano. Hatutaki kuona mtu anachukua memorandum ambayo ni 50 pages ama 100 anaedelea kusoma moja kwa moja. Hiyo itakaa mpaka usiku, na pengine watu wengine hawatapata nafasi ya kuongea. Memorandum ni kusema yale ya muhumu. Kama una point twenty, chukua ile ya muhimu pili ama tatu, ambayo itatosha hiyo dakika tano. Halafu ukimaliza utupatie hiyo memorandum, tutaandisha pale na tunaenda kuisoma zaidi. Kwa hivyo hapo wananchi tusikizane

kabisa. Kwa sababu ukiendelea kusoma hapa, wengine watakaa bila kusema lolote na tutachelewa hata ukifika usiku. Hiyo ni jinzi moja..

Jinzi ingine ni ya kwanza nimesema ni hiyo ya memorandum bila kuongea na hii ya pili nimesema unaweza kutetea memorandum kidogo. Sasa ni ya tatu, unaweza kuwa huna maandishi yeyote, mambo yanatoka katika kinjwa yako, yale umepanga. Unapewa hiyo dakika tano na utasema yale unaka. Yale ambayo unataka kuchangia kwa Kurekebisha Katiba, na hata hiyo ni dakika tano. Kwa hivyo hapo tueshimiane kwa hiyo njinzi kama tatu na tusipoteze wakati. Nikikwambia wakati wako umekwisha, heshimu wale wengine wako hapa, pamoja na sisi na uende ukaketi na mwingine aitwe aendelee kupeana maoni yake.

Tena kama Commissioners wangetaka kuhuliza ufafanue kitu chochote baada ya kupeana maoni yako, tutakuuliza maswali. Commissioners hapa sisi, yeyote angetaka kuliza masali kama ni clarification, kama ni kufafanua kitu, tutakuwa na hiyo nafasi ya kukuuliza. Na tena tutakuwa na mtu wa kutafusiri lugha ambayo tunaita sign language ya hawa watu ambao hawezi kuzungumza na pengine yuko karibu hapa. Kama tutakuwa na watu kama hawa pengine coordinator atajuwa. Na kwa hivyo wananchi, kwa hayo nimewambia, tueshimiane na tufanye hii iwe kitu ambacho tutapeana maoni yetu na kumaliza mapema na kila mtu awe amesema kitu.

Kabla hatujaanza hapa tunaona tuna DO wetu Bwana Opondo, yuko hapa, tunashukuru sana kwa sababu ametupatia area yake ambayo anasimamia na amekuja kama wananchi wengine, kiongozi wa area hii, na tumefurahi sana yuko hapa, DO na mnamjua na tumefurahi sana Bwana DO kuwa nawe hata ingawa hatungeweza kupita ofisi. Tulikuwa tunafikiria ofisi iko kwa wanachi na bahati tukakuta umetangulia. Asante sana Bwana DO. Hata pengine Chief, nimesikia pengine chief wameandamana naye, hata Chief wa area hii yuko hapa, sikupata jina lako lakini tumefurahi kuwa nawe na tutaendelea katika hii area yako. Asante sana.

Kwa hivyo, kwa hayo sasa nimesema tungetaka sasa kuanza na mtu wa kwanza ambeye ni Isaac Muchiri. Na mtu akija ataketi pale, utachukua hiki kipaza sauti na tena hiyo ni muhimu kwa sababu uongee kwa hiyo ili sauti yako ichukuliwe. Usipoongea kwa hiyo, sauti yako haitachukuliwa na uanze na kusema jina lako kila wakati. Na wale wana simu ya mkono, ama ya mfuko, hapa haifanyi, nasikia haifanyi, wangesima, kwa vile haifanyi, hakuna maana ya hiyo. Tuendele bwna Isaac Muchiri.

**Isaac Muchiri:** Mimi ninaitwa Isaac Muchiri na ninatoka upande wa Kiriko. Ningependa kusema, katika Katiba yetu ya Kenya tuwe, kama ni Bunge iwe miaka tano kulingana na Katiba ya zamani. Hiyo ni ya kwanza.

Ya pili, ningependelea chakula yetu au mazao yetu iwe ikiwekwa control na ile ingine kama mbegu za mahindi tunazonunua, iwe ikipimwa kama mahindi kwa maana kilo tisaini inanunuliwa na bei ya shilingi mia nne. Na hio tunanunu a kwa shilingi elfu moja

mia tatu. Kitu ningependelea kuwa na price control ya mzao yetu.

Ya tatu, ningependelea katika Bunge yetu ya Kenya iwe ikichagua makamu wa Raisi katika Serikali yetu ya Kenya.

Ya nne, commissioner wa wale waandikishaji wa watu wa kazi, wawe wakitutembelea katika mikoa au locations. Kwa sababu tuna watoto wetu ambao wamesoma na hawafikiriwi katika Katiba yetu ya Kenya. Tungependa wawe wakitutembelea katika kila location, na waweze kupatia kazi.

Ya tano, ningependelea, katika serikali yatu iwe hata awe aichaguliwa na raia, ndio awe akitumikia raia. Kwa maana anakuwa kama mtu wa serikali na tukiongea na yeye anatwambia yeye ni mtu wa serikali sitaki hataki maneno yetu, na akichaguliwa na raia atakuwa akitumikia wewe kama raia.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey umemaliza Isaac?

**Isaac Muchiri:** Nimemaliza.

**Com. Domiziano Ratanya**: Asante sana, Sasa tutaenda kwa Jospeh Wanyeri. Ni wakati wako bwana Joseph. Inaoneka Joseph hayuko, Opondo John no Obsever, Baraza ni Obsever, Kiprono na wengine hao lakini twende kwa Joseph M. Korir, huyo ana memorandu, lakini una dakika tano ya kutetea hiyo memorandum yako. So Bwana Joseph Korir. Kama unataka kuzungumza kama hutaki, upeane memorandum. Anza na kusema jina lako bwana Joseph.

**Joseph Korir.** Jina langu ninaitwa Jospeh M. Korir. Maoni yangu, ya kwanza ni Chiefs ni lazima wawe wakichaguliwa na raia, vile MP's wanavyo chaguliwa Na wakaae kwa miaka tano na wafutwe. Kwa sababu corruption ni nyingi.

Na kunatakiwa tena mambo ya lands, yaani sheria ya mashamba, kuwe na sheria kamili ya mashamba kwa sababu unapata watu wengine wana shamba hekari elfu ishirini ila wengine hawana hata pahali pa kusikwa.

Kuna sheria zingine kama zile wizi, kuna wezi wa aina nyingi. Mwingine anaweza kuiba mbuzi mali ya one thousand five hundred, na mwingine anaiba pesa ya Serikali kama Golden Berg, ankula pesa kama biliions, na hiyo anafanyiwa fair na yule aliyeiba mbuzi anawekwa ndani miaka saba. Kwa nini yule aliyeiba billions hajafungwa, na anafanya kezi akiwa inje na anachukua lawyer?

Ya nne, family affairs, lazima iwe tangled na according to the laws of customary because we have about, Wakenya tuko na watu kama forty two tribes, lazima kuwe na sheria za kitamaduni.

Ya tano ni, environment laws, kuwe na sheria ya mazingira kwa sababu watu wengine wanaweza kukatalia pahali kuko na maji na wengine wakose.

Upande wa kazi, kazi katika Kenya imekuwa ngumu na watu wengine wameshika kazi nyingi. Wanakuwa na biashara na kila kitu, sasa tunashindwa hawa watu wengine watakuwa wakifanya kazi gani. Tena kuwe na sheria ya kuwa councillors wawe wakilipwa kutoka kwa Treasury.

Parliament, lazima iwe controlled na Parliament itself. Iwe ikifunguliwa na wawe na Committee yao wenyewe, watakuwa wakisema ifungwe leo na sio wengine kusima ifungwe bure kabla ya mjadala haijamaliswa.

Kuna hii mashamba ya ADC, wengine wako na mashamba nyingi kwa NDC na wengine bado hawana mashamba. ADC ichukue na ipatie hata masikini.

PC's na ma-DO's, wawe wakiwa appointed by the Parliament and according to their qualifications.

Kuwe na sheria ile kali kwa watu wengine kwa sababu huu umasikini uliopo hapa Kenya, wengine wemeweka pesa nchi za inje. Kuwe na sheria kali ya kuzuhia kama death sentence.

Nitarudi tena kidogo kwa upande wa economy. Economy ya nchi ya Kenya, iliaribiwa na watu, na mtu yule ambaye anaharibu economy ya nchi lazima apewe death sentence ikiwezekana, kwa sababu hii sasa ni very serious. Kama vile Obasanjo amerudisha ile pesa ile wengine wamechukua, lakini, itamchukua muda mrefu sana kurudisha hiyo pesa.

Police, pasiwe na traffic police kwa maana hawasaidii Kenya. Wanakula na waleta corruption. Lakini sisemi hivyo kwa ubaya. Kwa sababu kuna watu wengine wananichukulia kwa ubaya.

Judges, women judges huwa very harsh to the men, kama siku nyingine nilisoma kwa gazeti, anaweka sentence kwa family affairs ya ten years. Kwa sababu ya family problem.

In Kenya kuwe sheria ya one man one job. Kwa sababu unakuta wabunge wako na job pili na wanakula pesa, wameongeswa mara sita. Tunabaki bure hatuna pesa, na wana business hata ya shops na hata wanarudi kwa kiosks, which is very bad.

**Com. Domiziano Ratanya:** Sasa Korir wakati wako umekwisha, Nimwita mtu mwingine. Kuna Swali.

**Joseph Korir**: Thank You.

**Com. Salome Muigai:** Bwana Korir nina swali kwako, asante sana kwa maoni yako, mimi nina maswali kadha, moja umesema kuwa wale watu wenya mashamba makubwa na wengine hawana, heri kuwe na mpangalio wa kuwafanya wenye mashamba makubwa mashamba yao ikatwe. Ungetaka kiasi kipi kiwe ndio kitakuwa na mtu moja? hilo ni swali la kwanza, nina maswali tofauti tafadhali, Swali la pili ni hii family affairs ifwatanishwe na mila zetu, akina mama wamekuwa wakilalamika kila pahali penye tumeenda kuwa, mila saa ingine haiwatetei. Kwanza hata ikipelekwa kwa wazee wanasema hao wazee waote ni akina baba. Kwa hivyo maoni yao hiyo kezi haiendi vizuri kwao, na wewe pia umefafanua kwa kusema ma-judge wanawake are to harsh kwa wanaume, kwa hivyo pia wakina mama wanasema, hawa wazee are to harsh on them Kwa hivyo tungetaka kujua maoni yako kwa hii korti za mila. Hayo ndiyo maswali yangu mawili.

**Joseph Korir:** Swali la kwamba ebu nikumbushe.

**Com. Salome Muigai**: Ni habari ya shamba, unataka kiasi gani ndicho kinakupaliwa mtu mmoja.

**Jospeh Korir:** Ni kisema ukweli kuna watu wengine kama family ya Kenyatta wako na--

**Com. Salome Muigai:** Hiyo tumeelewa, hiyo kitu yenye tunauliza, ikiwa wewe kwa pendekezo lako, ungeona shamba lipi ndilo likupaliwe mtu mmoja.

**Joseph Korori:** Wapate square kilometers za Kenya tupate kujua ni ngapi, na 20 hectares or ten hectares kwa kila mtu atleast kila mtu apate.

**Com. Salome Muigai:** Okey

**Joseph Korir:** Hiyo ingine ni ya Judges?

**Com. Salome Muigai**: Ile ingine ya kutumia mila, customary laws.

**Joseph Korir:** Vile nimesema hapo mbele I will refer you back Kwa maana kama watu wakuwa transparent vizuri, wawe na elders wale wazuri, wanaoweza sema ukweli, hao ndio watakuwa pamoja na Chiefs kama corruption hakuna Lakini kwa sababu ya corruption ndiyo inaleta all these things kuwa foreign

**Com. Salome Muigai**: Wakina mama wanalalamika kuwa hata hao waze wenye ni wezee akina papa pekee yao. Kwa hivyo hawaoni saa ingine masilahi ya mama. Hata mama wakati mwingine hawezi hata kuwaeleza wale wazee shida yake ya kinyumba, kwani wote ni wanaume, na pengine wakati mwingi ni wazee, ni akina baba yao akina mama. Kwa hivyo mila zetu pia, sinakuwa na upunguvu kwa kuweza hao akina mama kujieleza, nataka unieleza, ukileta hizo pendekezo, tutajali aje masilahi ya akina mama, kina baba, watoto wa kike, wavulana na kila mtu?

**Joseph Korir**: Hapo ningesema itakuwa vizuri kama watu wengekua transparent vizuri, hii maneno wakichukuliwe wawe na haki. Tutakuwa tukijua family affairs kama huyu mama. Wewe unajua kuna wamama wengine kweli wako na ubaya, na kuna wengi ni wazuri, sio wote, unakuta mwigine bibi yake amekufa kabla hawajapata watoto wengi, na amechukua ile mali iliyokuwa kwa nyumba fulani na akaenda nayo kuolewa na na mwingine. Sasa hiyo mali ya hapo haitabakia hapo kwa sababu amenda na kuolewa kwingine. Unaona sasa it will be unfair.

**Com. Domiziano Ratanya:** Tunaona kama hayo tumeelewa bwana Korir, na asante sana kwa maoni yako. Uende pale na ujiandikishe. Joseph Wanyeri, Dan Cherioyot, Simon Sang, Jack Kariuki, Simon Kiko, Jack Kariuki, jina lako halikuwe limeandikwa vizuri. Sema Majina yako Bwana Kariuki.

**Jack Kariuki:** Majina yangu ni Jack Kariuki. Yangu nina maneno mawili pekee yake ambayo nitasema tu orally.

La kwanza ni hili, ya kwamba kuna uhuru wa kuabudu hapa nchini Kenya, kwenye katiba yetu kuna hiyo. Na lile ambalo nilitaka kusema ama kuchangia ni ya kwamba uhuru huu wa kuabudu utengeneswe ya kwamba anakaye abdiwa ni nani, iaandikwe ni nani anaye abudiwa hapa nchni Kenya.

La pili langu ni hili, ya kwamba kuna vitambulisho, na birth cerficate ambazo sinapeanwa kwa kazi za wilaya na hata pengine za division, ninataka kusema ya kwamba hizi birth certificate itafutwe njia ya kurahisisha kuzipata, yaani siletwe kwa locational level. Kuwe na njia ya kupata birth certificates na vitambulisho kwa center ya division. Ni hayo tu peeke yake.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey asante sana bwna Jack, then Jack, kwanza utaenda hapo utupe majina yako. Joseph Wanyeri amekuja, then Dan Cheroyot, Simon Sang, Simon Kiko, Paul Murage. Sasa ni wakati wa Paul Murage, useme jina lako.

**Paul Murage:** Jina langu ni Paul Murage Moani yangu ni District focus, ningeonelea kwamba kama ni walimu wawe wakiwa na transfers. Wasifnayie kazi pahali wako na mashamba. Kwa sababu kama mwalimu ako na ngo'mbe na hii ngombe yake ni gonjwa, ni saa gani atataenda kusomesha watoto, fikira zake sitakuwa kule kule tu kwa ngo'mbe yake. Hata watoto weu watakuwa wakuumia.

Ya pili ni price control, sekali wawe waki-conrol prices ya vidha kama zamani. Kwa sababu kama sasa wafanyi biashara wanauza vitu kama wamenunua shilingi pili wanauza shilling inne. Kwa hivyo wanafaidika. Kwa biashara iwe na price control kama zamani.

Nitaongea habari ya umuhimu wa Katiba, watu wengi hawajui Katiba ni nini, kwa hivyo ningeuliza serikali watupangie, kuwe na vitabu vya kufunza watu Katiba, na hizo vitabu ziwe zikuhuswa kwa ma-bookshops, kama vitabu vingine.

Ya pili ningeongea habari ya ukulima, sisi wakulima tuko na taabu sana, kwa sababu kama sasa tunauza mahindi shilingi mia nne, na tumenunua fertilizer shilingi elfu moja na mia bili. Na hiyo ni kilo hamisini ya fertilizer. Tumenunua mahindi kilo kumi, kwa shilingi elfu moja na mia pili. Kwa hivyo ni kunia ngapi tutauza ili tuweze kununua fartilizer. Hiyo serikali watusaidie inputs iwe balanced na uhuzaji wa vyakula vyetu.

Ta tatu ningeongea habari ya Wabunge. Wabunge tukiwachagua, wakaae miaka miwili bila kutusaidia tuwe na uwezo wa kuwafuta na kuchagua wengine. Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey kuna swali hapo bwana Murage, Ngoja kidogo.

**Com. Riunga Raiji**: Bwana Murage, nilisikia kama ulipendekeza kwamba, price ciontrol irudishwa vile ilikuwa zamani, je unapendekeza iletwe kwa bidha vyote kwa jumla au ni kwa bidha fulani.

**Paul Murange:** Ni kwa vidha zote kwa jumla. Hata kama ni sukari, price yake iwe controlled by serikali. Watu wote wanye wana biashara waulize bidha kwa bei moja.

**Com. Riunga Raiji:** Anyefuata ni Michel Njoroge. Na ukija useme jina lako.

**Michael Njoroge**: Kwa majina ninaitwa Michael Njoroge Mburu. Mimi ninataka kuongea habari ya mazingira. Hi nchi imeharibika kwa sababu ya ukosefu wa mvua kwa ajili ya mti kukatwa. Na sana sana, inaonekana kuko na watu ambao wamepewa mashamba kwa forest. Hiyo sehemu ilikuwa imetengwa na Serikali irudishwe.

Tena ninataka kupendekeza habari ya masomo, tunaeleswa masomo ni bure, na tukiangalia sana, mimi sio mzee sana wakati nilikuwa ninasoma, tulikuwa tunalipa kitu iliyoitwa fees. Lakini hatuwa tunanunua kalamu, Geometry set na lakini sasa tunaambiwa ni ya bure na tunanunu vitu vyote. Masomo irudishwe kama zamani. Ni hiyo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Sasa unapendekeza nini, iwe namna gani?

**Michael Njoroge**: Masomo irudishwe kama zamani, tuwe tukilipa pesa ya fee, vile tulikuwa tunalipa. Na tunapewa kalamu, Geometry set, vitu yote vinapeanwa na vitabu. Wazazi wasiwe wakinunua exercise books, tex books, hiyo vitu zote watoto wanapewa.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey, Bwana Michael hayo ni maoni yako, Okey asante, enda pale ukajiandikishe. Na pahali tumefika ni kwamba, mweshimiwa wetu Hon. Muroko ameingia, Muheshimiwa unajua tulikuwa na wewe kutoka jana katika

Constituency yako na hata leo. Kwa hivyo karibu sana tuwe nawe hata leo, usikilize maoni ya wananchi wako na ukitaka nawe kupeana yako, uko huru. Welcome Muheshimiwa. Sasa tuna Julius Maina. Julius maina hayuko? Julius Maina karibu, sema majina yako maina.

**Julius Miana:** Majina yangu ni Julius Maina Kariuki, mimi ninamaoni kuhuzu mambo ya vile serikali iko, kuna mikono mitatu ya serikali ambaye tunaelewa, hiyo inakawana mamulaka. Kwa hivyo kila mkono hutekeleze jukumu lake.

Mambo ya masomo, katika primary education, ninapendekeza kuwe na kItu kinaitwa free education. Kwa sababu tukiangalia katika wakati huu, kuna watoto wengi sana wamekuwa drop outs katika darasa za katikati kabla ya kufika standard eight. Mambo ya afya. Pia itekeleswe kwa njia bila malipo. Kusiwe na mambo ya cost sharing.

Unemployment, hii iwe inagawanwa equally ama tuseme kila mtu anapoaandikwa kazi, haweze kufanya kazi kwa miaka kumi. Iwe ni kama contract ili watu wote wapate kazi. Mambo ya watoto, rights za watoto sitekelezwe vilivyo.

Mambo ya wanawake, rights for women, sitekeleswe lakini wasiwe na uwezo kuliko wanaume, kwa sababu hata bibilia imekataa.

Mamo ya Electoral process, hiyo ningependekeza tuwe na Electoral process ambayo ni independent. Iwe na staff na pia ifungue ma-office hati location level.

Mengine ni kuhuzu vile vyama vya political parties vinavyo hudumu. Siwe sinashirikiana vilivyo. Visiwe kama adui. Nafikiri yangu maoni imefika hapo, na pia nina written, ambayo sijui kama mtaipokea?

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey Bwana Julius Maina, hiyo mambo umeandika tutapokea. Kwa hivyo asante kwa maoni yako. Upeane pale. Jason Waweru, ni wakati wako.

**Jason Waweru:** Mimi nitaongea kwa lugha ya mama.

**Jason Waweru:** Ritwa riakwa ni Jason Waweru wa Ruoro
**Translator:** Majina yake ni Jason Waweru Ruoro.
**Jason Waweru:** guitu ni goku weuomererie
**Translator:** kwetu ni hapa huyumilie.
**Jason Waweru:** Ondu uria ikuga re
**Translator:** Lile mbalo nitasema,
**Jason Waweru:** ne ondu ukanainie na mititu**.**

**Translator**: ni kuhusu misitu.

**Jason Waweru:** Mititu ni yanangetuo muno

**Translator**: Kwasababu msitu yetu imeharibiwa vilivyo

**Jason Waweru:** Na nekio urona kinya mbura ndiraura.

**Translator**: Na ndivyo unaona ya kwamba hata mvua hainyeshi,

**Jason Waweru:** No nyende sheria ekero

**Translator:** na kwa hivyo ningependa sheria iwekwe,

**Jason Waweru:** Ne getha borori oyo wity wa Kenya ohane otakawaida.

**Translator**: ili kwamba nchi yetu ya Kenya irudi kama mwanzo,

**Jason Waweru**: Ona ongerora kirima kiria kia rogoko.

**Translator:** maana hata ukitazama mlima kule juu,

**Jason Waweru:** Gotire na mti

**Translator:** hakuna mti,

**Jason Waweru:** Na ndirauga gwekero watho ati andu mahande mti

**Translator**: lakini ningesema kuwekwe sheria watu wapande mti

**Jason Waweru:** Ne getha andu mahote kuona gia koria.

**Translator:** na ili watu wapate chakula,

**Jason Waweru:** Ne ohoro wegie mbura.

**Translator:** kwa sababu hali ya mvua

**Jason Waweru**: wakwa no ocio.

**Translator:** Yangu ni hiyo.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey asante sana Jason Waweru, Twende kwa Joel Langat. Ni wakti wako Bwana Joel.

**Joel Langat:** Kwa majina ni hayo mumesikia, Joel Langati, leo nitaongea juu ya Commossion. Tuwe na Commission ya kushukulikia mambo ya freedom fighters. Hawa ndugu zetu ambo walipigania uhuru wa nchi hii, tuwe na Commission ya kuangalia welfare yao. Kwa sababu inaoneka Katiba ya zamani, ilisau welfare yao

Pia mambo ya maji, maji iwe ni haki ya wakenya wote. Wale wanao fikiria kufanya irrigation, basi wasitumie maji ya mitoni. Waweze kijimba bore holes zao lakini maji ya mtoni iwe ni haki ya wakenya wote waweze kutumia. Na ipigwa marufuku kabisa, ministry of water wasikupalie mtu yoyote kutumia maji ya mito kwa irrigation farming.

Cemetry, watu wote wakenya waweze kuzikwa katika ma-cementry. Hii tabia ya kusika watu manyumbani, iweze kupigwa marufuku.

Lease farms,mashamba yote ambayo yako chini ya lease, yapinduliwe yawe free hold titles, ile watu wengine wale wajuaji wasitumie nafasi hiyo, wakijua 99 years, ama 999 years imeisha, wanakipia na wanapindua hizo titles. Kwa hivyo tungetaka mashamba zote Kenya yawe chini ya free hold titles.

Age, wazee wangongwa baina ya mama na wazee kuanzia miaka themanini na kuendelea mbele wawe ni mali ya central government. Central government iangalie welfare yao na wale wazee ambao wamekaa nyumbani, basi wawekwe katika manyumba ya wezee na garama zote sikaramiwe na central government.

Muslim day na seveth day, siku za waislamu kama ijuma, jumamosi ya seveth day iheshimiwe sawa na Sunday, kwa ajili ya wakristo. Ama national day ina-fall on a Friday, or on a Saturday, basi siku hiyo iwese kuharishwa ili nao pia wasikie ya kuwa they are part of Kenyans.

Ma-chiefs na ma-assistant chief, wakiandikwa kazi basi wa apply kazi kwa mtindo huu uliyoko sasa, lakini watatu wawe vetted wale the best wame-qualify na watu watatu warudishwe kwa raia kuwapigia kura. System hii ambayo iko ipate tu kuendelea lakini kabla mtu hajawajiriwa kazi, aletwe nyumbani, ili wenyeji wajue ya kwamba mtoto huyu anasitahili kuwa Chief wetu. Kwa sababu katika ukoo zetu kuna manyumba ya watawala, kuna manyumba ya askari, wale wa vita, kwa hivyo manyumba ya wale wanao tawala basi wafikiriwe kwanza. Kwa sababu tunahitaji utawala mzuri. Basi ni hayo tu siku ya leo, kwa sababu sikutaka kupoteza wakati mwingi ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Bwana Joel, ngojea kwanza kuna swali.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana bwana Langat kwa maoni yako, swali langu ni, jamii zenye simechanganyika kama hapa kwenu, kama tukitumia mila za jamii moja vile unasema hii nyumba ilikuwa ya ma-chief na hii nyumba ni ya askari na ile jamii yangu niseme kwa kikwetu ndio ma-chief, how do we harmonize na……… kusikiliza hayo mambo kwa jamii silizochanganyika kama hapa………………

**Joel Langat**: Jamii ya wa-kalejini wana ukoo ya uongozi, basi hawa watafikiriwa kwa utaribu huo.

**Com. Domiziano Ranya:** Okey Bwana Langat, okey kwa maoni yako. Halfu twende kwa John Njenga. Jonh Njenga yuko na written memorandum, kama ungetaka kutuelezea kidogo.

**John Njenga:** Ningetaka kuzungumza kidogo. Jina ni John Njenga Kichure. Ningetaka kuzungumzia juu ya mashamba. Wakati wa ukoloni, watu walipigana vita kwa sababu ya mashamba, tulikuwa na taabu kubwa. Na ile taaabu tulikuwa nayo, mpaka wa leo ingalipo. Kwa sababu watu wetu wengi hawana pahali pa kukaa. Ningepekeza wale ambao wako na mashamba makubwa, waaje na ikawiwe wale watu ambao hawana mashamba, maanake wao pia ni Wakenya. Na hatutaki vita

mara ingine, twataka kila mkenya awe na shamba. Kiasi cha shamba, ni mzuri mtu awe na heka kama kumi, kuliko awe na hekari elfu mia mbili na mwingine hana. Hilo ni jambo moja.

Jambo lingine, tuna watoto wasichana, hao tumewaza kama wale wengine, tunataka wale watoto baba yake akiwa yuko, agawe uridhi sawa na vijana. Kwa sababu hata yeye ni mtoto wako.

Ya tatu tuna taabu hapa Kenya. Taabu ile tunayo ni polisi wale tumeandika, hawafanyi kazi hata kidogo. Kwa sababu ukikimbia barabarani unakuta wamesimama barabarani kuangalia ajali, na hata magari yakiwa wamejaa namna gani, wanazungumza na yule mwenye gari, na inaendelea. Sasa tumeshindwa nini? Tupewe uwezo wa kuwashitaki na tujulishwe ni wapi tunaweza kuwashitaki. Kwa sababu hawalindi raia.

Kuna jambo lingine ningalipenda kusema, wale wezi wanao tembea usiku wakiwa na silaha, ni jambo kubwa sana mwanaume kukutwa kwake nyumbani na mwaume mwingine na amekuja kumnyang'anya mali yake na yuko na silaha na huyu hana. Mwneye nyumba hukaa kama mwanamke tu, basi tunauliza kama serikali wanaweza kukubali, ingefaa mtu yule yuko na uwezo akubaliwe kununua silaha naye ajilinde kama mwanaume kuliko kupigwa kama mwanamke. Hili ni jambo kubwa sana.

Mashule ni kweli watu wameelezwa ati ni ya bure, nafikiri si bure, kwa sababu kila siku, mimi sina mtoto sasa, watoto wangu ni kama nyinyi, lakini nimeona wazazi wa siku hizi wamezumbuka sana. Mtoto akifika shule wanarudishwa nyumbani kuja kuchukua pesa. Pesa hii tunauliza tena, na elimu elipeanwa bure ni ya nini. Hi pesa iondolewe. Serikali ichukue masomo yote hata na mjengo, kwani wewe ikiwa huna nyumba wewe ni mtu gani. Serikali kama inasema mashule ni yake, injenge. Langu ni hilo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Kuna swali.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana Gichure, swali langu ni kuhuzu tu kitu umezungumzia. Umesema kuwa wanaume wakiingiliwa nyumbani, wanapikwa kama wanawake. Nao wakina mama watwapia. Katiba yenye inakuja sasa, hawangetaka kupigwa, na wewe umesema watoto wako ni kama rika yangu, kwa hivyo wenye kupigwa ni bindi zako, ndio unasema wapatiwe mashamba, maoni yako ni nini kwa kupigwa kwa wanaweka.?

**John Njenga:** Maoni yangu mtoto ya msichana ni kama tu mvulana. Kusema ukweli hakuna mtoto anazaliwa vizuri kuliko mwingine. Kwenye maoni yangu nimesema namna hii, wale watu wanaopiga wanawake wao kama Punda washikwe na washitakiwe, wafungwe.

**Com. Domiziano Ratanya:** Asante Bwaba Njenga enda pale using register yetu. Tunaenda kwa John Kiprono. Endelee bwana Kiprono.

**John Kiprono:** Jina langu ni John Kiprono. Nimeshaandika lakini nitakuzia macheche tu nitakuzia.

Kama kuhuzu hali ya mashamba, kazi ya mashamba hivi, mambo mengi yamefanyika kwa sababu watu wengi pengine wamekuwa wakinyang'anya mashamba. Lakini wakipelekwa kortini, pengine mengine ni masikini na mwingine ni tajiri, sasa unyanyasaji wa mawakili. Kwa hivyo ningeomba kwa maoni yangu, hiyo kezi irudishwe kwa wazee kwa sababu wanajua historia sana ya hayo mashamba.

Kingine ni kuhuzu police. Police pengine wanaweza kuwa wametumwa mahali fulani, lakini hawaendi kutekeleza hizo kazi, wanaenda ku-serch kwa manyumba ya watu na kuingia nyumba ya mtu wakiwa free na kuanza kikutisha kwa njia nyingi na kuataka mambo ya hongo. Hata ile kazi walikuwa wametuwa, wanasahau. Kwa hivyo wawe na ile serch warrant na waende directly pahali wametumwa au kama ni kushika mtu waende huko direct. Na sio kutangatanga na kupitia kwa manyumba ya wengine. Wanaanza kufanya kazi kama ngo'mbe imeibiwa, hawafuati na wanaanza kufuata mambo ya pombe na kutisha raia kwa njia zingine na kuitisha pombe.

Kuhuzu tena mashamba, kuna malalamiko mengi sana kwa mambo ya Title Deeds. Kutoka kwa lands, kuna watu wanang'ang' ania Title Deed. Shamba moja unaona wako na title deed kwa shamba moja, sijui lands inafanya nini. Kwa hivyo ingalie hapo. Tena kuhuzu Title Deeds, unahawa viongozi wengine wanaitisha pesa nyingi sana za Title Deed. Kwa hivyo tuwe na control kutoka kwa lands. Kama wale ambao hawajapata title deeds, kuwe na control ile ya bei ya kutoa Title Deeds. Kwa sababu kuna walakai viongozi wengine amabo wanaitisha zaidi. Na kumbe kule kwa lands

Tena kuhuzu mashamba. Kuna watu maskini, squatters, na kuna wale wanao miliki mashamba zingine kubwa sana Kenya na hawaitumii. Na hata zingine ni za wanyama, kwa hivyo hata hizo shamba zenye hasiangaliwe sipatiwe squatters. Kwa sababu hao ni raia wa Kenya.

Kuhuzu hali ya uraia, kama sisi ni Wakenya, tunaweza kutembea mahali popote. Kusiwe na matisho at wewe ni nani kama ukiwa mgeni mahali fulani, unaanza kufanyiwa serch nyingi sana. Na pengine unafurukwa.

Kuhuzu mahakama kama mtu amesshitakuwa na bado haku kwa remand. Kuna matisho mengi sana kwa yule ambaye hajamaliza kezi yake kama kuhukumiwa, huwa wananyanyaswa huko gerezani sana. Baadaya ya kuhukumiwa, pengine alikuwa ameroboka maombo mengi kwa sababu ya mateso. Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Mwinge ni David Njoroge Mwangi.

**David Njoroge Mwangi:** Kwa jina ni David Njoroge Mwangi. Kwanza nitazungumzia kitu ambacho kinaitwa afya.

Ningependekeza sahanati zote za watu binafsi, kwa maana serikali imeshindwa kusaida watu wao, iwe na mpangilio, kama mtu ni daktari, asiwe na sahanati yake. Sahanati ambazo hasifai sifutiliwe mbali kwa maana hatujui mahali wanatoa dawa na huku serekali inashindwa kutoa pesa za dawa. Kwani hao walitoa pesa wapi? Tungetaka hizo zahanati zote, zifutiliwe na serekali isaidie

Agriculture: Kuna vitu ambavyo wizara ya kilimo inatakiwa itusaidie. Kitu kama ku-control vitu vya ukulima. Unakuta ya kwamba, wale tunanunua mbengu, kunia moja ya mpegu ikiwa ni shilingi elfu moja mia tano, na huku mahindi inanunuliwa shilingi mia tatu, hiyo ni kuonyuesha ya kwamba kuna ufisadi na unyanyasi na ndio hatutaki, mabatiliko iweko.

Civil servants: Kuna watu ambao wameajiriwa na serikali, wakiwa walimu au polisi au ma-chief wote wawe na nidhamu nzuri kwa maana Kenya imearibiwa na kutokuwa na nadhamu kama kukunywa wakati wako kazini. Wanakunywa wakiwa kazini na alafu unakuta mtu, kama ni mwalimu analala darasani, kama ni polisi hata hafanyi kazi na hajui kile kinachofanyika, kama ni Chief ama DO, hajui office yake ni ya saa ngapi, hiyo kuwe na sheria, kunawengi wanataka kazi mtu kama huyo aondolewe.

Immigration: Mtu akitaka kutembea popote Kenya, awe huru na asiwe mtu wa kutishwa ati ya kwamba kuna sehemu ambayo haweze kanyakanga. Ukitaka kunua shamba au mbuzi, tuwetunasiadiana Kenya na tusahau mambo ya ukabila. Mambo ya ukabila tusahau.

Education: Elimu nayo ipatilishwe, hatutaki hii masomo, hatutaki hii masomo mabayo inaletwe vitabu leo na mwaka huu inabatilishwa. Mwaka ujao inasomeshwa na hii, na ujao unakuta imebatilishwa, wanaumiza wazazi na wananchi wa Kenya. Kwa hivyo education iwe controlled. Pia kuhsu elimu irudi ile ya zamani mtu awe anafanyiwa mtihani wa daraza la saba, kitado cha pili, kitado cha sita na university. Mtindo huo urudishwe. Na iwe methibitishwa na si Katiba ipatilishe.

Jambo lingine ni kuhuzu mambo ya societies. Kuna watu katika Kenya walikatishwa mashamba miaka nenda miaka rudi, kuwe na sheria kuanzia sasa na kuendelea ya kwamba ukikatisha watu lease, kwenye society yeyote, pesa zao ziwekwe, na kama hiyo kama aiwezegani, walirudishiwe mashamba yao kwa maana kuna watu wakata mashamba na sasa ni miaka ziadi ya thelathini na hawajapata.

**Com. Domiziano Rayatanya:** Okey, saa yako imekwisha sasa. Kuna swali.

**Com. Salome Muigai:** Asante Bwana Njoroge Umesima kuwa mtu akiwa daktari, asikupaliwe kufungua sehenati yake mwenywe, basi ukiwa daktari hawatafungua dispensaries, ni akina nani wenye watafungua?

**David Njoroge Mwangi**: Zamani, serikali ilikuwa inatumia ma-hospitali yetu kutibu watu kikamilifu na hakukuwa na

mahospitali hizi Private. Tulijua International Private hospitals, kama Aga Akhan. Kwa hivyo hizi hospitali zote ndogo ndogo ndizo simeleta wizi wa mali ya zile vitu ambazo singeweza kusaidia mwananchi. Na serikali inatenga pesa wakati wa budget ya kusaidia mwananchi kufanya nini? Unakuta dawa sinaletwa hapa kwa sahaniti yetu, inamaliza two days hakuna dawa, na unaandikiwa karatasi uende ununue dawa. Na yule anakutuma, penye anakutuma, anakutuma the very place pahali anajulikana na ni mahali anapeleka hizo dawa. Kwa hivyo ningependekeza zifutiliwe na kama ni international hospitals, siweko. Kama Aga Khan. Lakini si mtu wa kufungua ati ni daktari, dereva, ama nani, hiyo si vizuri.

**Com. Domiziano Ratanya**: Asante bwana David Njoroge, tumesikia hayo maoni yoko. John Kicheru, ni wakati wako bwana John Mucheru. Uaanze na kutwambia majina yako.

**John Mucheru**: Jina langu ni John Mecheru Kibuga. Ninataka kuelize ya kwamba wakati serikali wanaandika au wanaajiri civil servants wawe wakifuata merits, Yaani masomo. Kama ni watu wa Bunge, wawe na merits hata kama ni President, vice President hao wote.

Ya pili, tunaomba serikali walinde maisha yetu na mali yetu. Kwa sababu kuna watu wanaingilia wengine na kuwapika hawajali kama kuna serikali.

Ya tatu, tunaomba serikali waangalie wale watoto au wamama walianjwa na walio wanjwa na wapiakania uhuru. Freedom fighter walichangia sehemu kubwa ya nchi lakini watoto wao wanarandaranda tu, hawna makao, mashamba na elimu.

Ya nne, tungeomba serikali waangalie wale watu wanaoishi pahali semi and arid areas, wawasaidie na kuwaletea maji, itakayowasaidia kwa upande wa ukulima. Tuseme kama kwa irrigation na upande wa domestic use.

Yangu ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey asante Mucheru. Nitaenda kawa Josephine Ngonyo.

**Josephine Ngonyo:** Asante. Jina langu ni Josephine Ngonyo. Nitasoma Memorandum yangu mahaki nitafikisha hiyo nyingine nitaaja.

**Com. Domiziano Ratanya:** Unajua una dakika tano, na nikikwambia umemaliza saa yako, unaodika.

**Josephine Ngonyo:** Point ya kwanza tungetaka Rais asiwe na kazi nyingine ila tu kazi ya kuongoza nchi pekee. Mbunge akisha chakuliwa kuwa Rais sehemu yake ya umbuge iruhusiwe kuchakua mbunge mwingine na hali kadhalika Rais huyu ajishughulishe na chama chake, awe neutral. Wamama wapewe asili mia thelathini ya uongozi wa ubuge na 75% asili mia ya

udiwani.

Mahakama iwe na uhuru kazini bila kuongozwa na Rais na pia judge mkuu ahajiriwe na serikali na asiwe chini ya Raisi.

Bunge iwe huru bila idhini ya Rais. Pia Bunge iwe na wakati mahalumu unaojulikana, siyo Rais kujua lini kufua au kulifunga.

Wafanyi kazi wote wa serikali, wasiwe na biashara nyingine nje ya kazi aliyo ajiriwa.

Masomo tungetaka yawe ya ya bure kwa watoto wate.

Matibabu yawe ya bure kwa watu kwa watu wote, pia hospitali ya private, na biashara yeyote ya dawa zifungwe. Hizi hutuma, zifanywe na serikali bure kwa raia wote.

Msichana au mvulana akioa nje ya Kenya, waruhuziwe wote wawili kujiandisha wanaraia wa nchi zote pili.

Kila Mwezi wazee wanaume au wamama wakipitisha umri wa miaka themanini, na wawe hawana biashara yeyote wanayofanya, na hawakuwa wafanyanyi kazi wa serikali hapo awali, wawe wakipewa pesa kidogo ya matumizi kila mwezi kama shilling elfu tatu.

Viwete wote wapewe elimu kulingana na ulemavu wao na baadaye wapatiwe kazi na serikali. Kiwete ambaye hawezi kujimdu, awe akipewa chakula na nguo na serikali.

Kazi zipatiwanwe kulingana na elimu ya mtu. Wasimazi wa idara zote wawe na elimu ya kutosha kusimamia idara hizo. Elimu ambayo inayo lingana na idara yenyewe.

Mwanamume akimnajizi mtoto, tungetaka afungwe maisha.

Mungu baba wa mbinguni aabudiwe peeke yake.

Biashara ya bidha kutoka nje ya Kenya, ambazo tunaweza kupata hapa Kenya, isiruhusiwe kamwe. Kama Sukari, na tuna miwa. Kahawa machani na kadhalika. Wakulima wa cash crops zetu za Kenya kama kahawa na machani, tungetaka wahimarishwe ili tupate mavuno haya kwa wingi.

Mtu asiwe na kazi zaidi ya moja na watoto wote wasiajiriwe kazi hata ikiwa ni maid. Bali wote wasome

Kenya bureau of Standard imarishwe na soko huru ihishe katika sector zote.

Arusi yeyote ikifunganishwe, tungetaka pawe na idhini ya wazazi wa pande zote mbili. Baada ya dalaka, watoto waote wawe wakishughulikiwa na baba kuhuzu mavasi, chakula na kadhalika.

Ikiwa mbuge au diwani haridhishi watu wake, wapewe idhini ya kumng'oa na kuweka mwingine hata miaka tano ikiwa bado kuisha.

Tungetaka tupatilishiwe hii 8-4-4 system katika shule zetu, tungeta irudi 7-4-2-2 system.

Wamama tungetaka wawe na haki ya kuridhi mabwana zao, mali zao na siyo kusimamia ili watoto wakume. Tungeta pia kuwe na Commission ya kupangia Wabunge mambo yao kama mishahara katika Kenya yetu.

Polisi tungetaka wawe wakifanya kazi na vitambulisho na uniform kila wakati. Wanaraia wawe wakitoa koti kilingana na kazi zao na biashara zao.

Title Deeds huwa ya mtu binafsi, haza hapa Rift valley ni ya mika 99, lakini mahali pengine kama Kiambu ni ya milele. Tungeta hizi title deed ziwe za mile kwa watu wote katika Kenya.

Ni hayo tu hata sikuwa na mengi.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey asante sana Josephine, Simon Githenji, ndiye anayefuata.

**Simon Githenji:** Asante. Kwa jina ninaitwa Simon Githeji. Mimi mweywe ningetaka kukuzia kezi zingine ambazo huwasinapelekwa kortini. Kama robbery stroke one, and muder case stroke one.

Kwani kortini ama remand kunao watu wengine wengi sana wanaoishi miaka mingi hata bila kufanya kezi yeyote. Kunazo zile vitu zinazoitwa kibali, ama committal bundles, ile committal bndles, mtu akifanya murder case, inakaa miaka mingi sana kabla ya kutoka kwa State Counsel. Kwa hivyo ningeonelea, kwa sababu watu wengi wanateseka wakiwa remand bila kufanya kezi ama kusikiswa kwa kezi yao, ningalipendelea hizi committal battles ziwekwa kwa muda. Kwa hivyo, kama mtu ameshitakiwa leo,apelekwe remande leo na isipite mwezi mmoja kama committal bundle haijafika kortini.

Jambo la pili, Ningependelea katika nchi ya Kenya, kwa sababu iko wakati mwingine waziri aliyekuwa anaitwa Anthur Magugu, alitangaza ya kwamba, kwa ufutaji wa zigara, ile packet ya sigara iaandikwe, uvutaji wa sigara unaweza kuthuru afya ya mtu. Kwa hivyo ningalionelea baadala ya hayo, ufutaji wa sigara katika nchi ya Kenya upigwe marufuku kabisa. Na kama

mtu anapatika akivuta sigara, anashitakiwa.  Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Kuna swali hapa Bwana Githeji.

**Com. Riunga Raiji:** Bwana Githeji umependekeza, hii committal battles, lakini kama unajuwa wakati mwingine, wakati police wana-investgate makezi kama hii ya murder, inachukua muda zaidi ya mwezi mmoja.  Je ungependekeze tuajilie hao ……..au tuwapatie muda zaidi wajaribu kupata evidence yenyewe kwa……………….

**Simon Githeji:** Mimi ningependekeza, ukienda kortini ama kwa rimade, utakuta mtu mmoja ako na zaidi ya miaka saba ama mitano kwenda juu, kabla hajawahii kuonana na judge mwenywe.  Kwa hivyo, huo muda wote, inaonekana hata kama kwa polisi, statement inaweza kumaliza tu miezi miwili.  Ukienda kwa hawa wengine wanaoitwa CID's hiyo inaweza pia kuchuka muda wa miezi miwili.  Tena kwa state council inaweza kuchkua muda wa miezi miwili.  Kwa hivyo ningependekeza kama ni miezi sita isipite hapo.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey, asante kwa maoni yako Simon Githeji. Patrick Gichuki.

**Patrick Gichuki:** Jina langu ni Patrick Gichuki. Mimi ninaonelea serikali iwe iki-provide kwa education, free food, heath care na Security.

Katika masomo ninaonelea serikali ingepeana elimu ya bure hati standard eight. Kwa upande wa Enviroment, mimi ninaona, msitu imearibiwa na serikali imechangia kwa uharibifu huo. Ningeonelea, kama serikali ingepanda mti kando kando ya barabara na wale ambao wamepanda mti kwenya mashamba yao, wawe huru kuikata bila kuingiliwa na serikali.  Kwa sababu wakti mwingi unaona mtu akikata mti kwa mahitaji yake, askari wanakuja, wanamshika na anawekwa ndani.  Na hiyo hata inazuia wakulima wengi kupanda mtu katika mashamba yao.

Tena mimi ninaona kwa wale watu ambao ni wazee, wakiaja kazi ama wakizeeka, serikali iwasaidie ikiwa hawana mahali pengine pakutoa usaidizi.  Tena wafanyi kazi waruhuziwe wawakilishwe na vyama vya wafanyi kazi, bila kukataswa na wajiri wao.

Tena kwa uchaguzi ujao, ninaolea, tukitumia Katiba ya sasa na ifanywe mapatiliko sehemu inayohuziana na uchaguzi, ingekuwa bora kuliko kuongeza muda wa Bunge.

Katika serikali ningetaka kuwa kuwe na division of powers, yaani kama Legislature, Executiove na Judiciary kila moja iwe independent, na section ya 25% kwa provinces tano iondolewe.

Kuna ma-reserves kwenye watu wanatoka na mashamba bado haijakuwa demarcated. Ningependekeza iwe demarcated ndio kila mtu apate plote yake. Na candidates na Parliament na Local Authorities wawe ni watu ambao wameituimu hati kitado cha form four. Na ministers ama assistant ministers wawe wamchaguliwa kulingana na academic na professional qualifications.

Nina hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya:** Kuna swali moja, hapa umesema ile 25%, ambayo inawekwa kwa kila province wakati wa kuchagua President, iondolwe kabisa?

**Patrick Gichuki**: Iondolewe kabisa.

**Com. Domiziano Ratanya**: Sasa ungelitaka kuwe na nini pale pahali badala ya hiyo.

**Patrick Gichuki**: Awe akichaguliwa na simple majority, lakini aseme akichakuliwa, atakuwa huru na hatakuwa akiongoza chama chochote. Kwa hivyo hata akichaguliwa na watu wote bila kutumia hiyo 25% itakuwa sawa.

**Com. Domiziano Ratanya:** Simple majority.

**Patrick Gichuki:** simple majority ndiyo

**Com. Domiziano Ratanya:** Hayo ni maoni yako asante bwana Patrick.kuna Judy Gitai

**Judith Gitai:** Kwa jina ni Judith Chepleting Gitai. Yangu ni hivi;

Bunge: Tungependa President akiwa mwanamume, vice wake ama Prime Minister awe mama.

Chakula: Katika Kenya, tungependelea kuwa Chairman akiwa mwanaume, Vice wake awe mama kwa sababu, unajua chakula siku hizi imekuwa na ufisadi sana. Sasa hapa Kenya tunajua tunaelekea kwenye hali ya njaa. Lakini tukiwa na mwanamke kama kiongozi kwenye sehemu hiyo, ninajua atajua kutunza hiyo sector.

Tatu, tunahiji family courts; Family should be established in every district to conduct women cases. e.g rape and domestic violence.

Citizensship: Tungependa watoto wetu, akiwa msichana ama kijana, akiwa ng'ambo awe na passport, kwa sababu tunajuwa kwamba wasichan wetu wakiolewa ng'ambo, spouses wao wakija Kenya, hawesi kuruhuzu watoto wao wawe na passports.

Kwa hivyo tunahitaji spouses wawe na passports. Tunataka usawa kwa watoto wetu wakati wa kuridhi mali.

Tano, tunapendekeza walemavu wafikiiwe kwanza kama wakati wa kuajiri wafanyi kazi kwa sababu tunajuwa wale ambao ni walemavu kweli wamewanchwa nyuma. Serikali iwafikirie kama watu wa kwanza.

Sita, tunataka protection kwa wamama na watoto wakati wa vita.

Office ya Chief; Tunapendekeza office ya Chief wakati wako na makezi, wazee wawe hata wamama. Kwa sababu tunajua wamama tumepigwa zaidi. Kwa hivyo tunapendekeza hata wamama wawe.

Hali ya mashamba: Tunaomba tuondolewe koti ambayo tunalipia mashamba yetu ambayo tuko nayo. Kwa sababu sasa vile tunalipia koti, tunalipia nani na mashamba ni yetu?

Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Asante Judy Gitai. James Biyeko. Anyefuata ni James Biyeko, Kama yuko karibu, ni wewe James, Okey Endelea ni wakati wako.

**James Biyeko:** Kwanza akabisa nitachukua kuomba kwamba nina alama au vipengele vingi, kwa hivyo nisipomaliza kwa wakati ufuatayo, mniruhusu tu nimalize.

**Com. Domiziano Ratanya:** Vile tumefanya ni kwamba kila mtu anapewa dakika sawa na mwingine. Kwa hivyo ni dakika tano, chagua yale ya muhimu na utumie wakati wako.

**James Biyeko**: Asante sana, I want to present my prsentation in English. My names are James Biyeko.

And our current Constitution is written is English, what I am saying is that it should have a Preamble to show that it belongs to the people of Kenya and it should state all the Kenyans tribes including the smallest until the biggest.

Secondly I will talk about citizenshsip, the chapter of citizens should be the second chapter. That means it shoud actually talk of who is a Kenyan. And therefore it should follow as chapter number two. **Interjection by Com. Ratanya.**

**Com. Domiziano Ratanya:** Sorry ngojea kidogo, kuna tangazo fulani hapa, yeyote ambaye ana funguo za hii kabati ya church, hiyo ufunguo inahitajika ili watoe kitu fulani. Funguo ya curboard, kama kuna yeyote hapa ako nayo, apeanae. Okey Bwana James Biyeko, nitakuongeza hiyo dakika yako.

**James Biyeko**; Now I am saying that citizenship should be chapter two. The chapter on citizenship that tell us a Kenyan is. Should be chapter two in the new Constitution.

It should be followed by the current chapter five, which should be chapter three. The Bill of Rights which should tell us how these people who are Kenyans should be treated.

Now the Constitution we are writing once ready should be written in all possible languages in Kenya. Because it is not understood because it is written in English only. For example in Kikuyu, Kalenjini, Tholuo, Kisii Masaai and the rest.

The Constitution once ready should be sold cheaply to all Kenyans and should be available in all shops like bookshops and government offices.

Five, The Constitution that people of Kenya shall write should be the highest law in the land and should not be used to indminate Kenyans citizens of the land.

Baadaya ya Katiba kuwa imechapishwa, it should not be amended by the Parliament, it should be taken back to the people themselves who made it, because it belongs to them, it does not belong to the Parliament.

Number seven, a Constitutional Committee or Commission should be formed to take care of it, that it is not violated by those elected. Because those elected are responsible to the Kenyan Citizens.

Powers currently held by the President from the current Constitution should be vested in the Cabinet. And the cabinet should be head by a Prime Minister. Therefore the President should only be a ceremonial President to preside over what we call National days.

Employment in the country should be based on academic qualifications, performance, training and experience and with proper payments and salaries. And like the current now that we have minister who doesn't qualify in their department that they head.

Ministry polices should be made with consultation to the implementers e.g, like for example in education, the policy of education should be made once the teachers have been consulate.

That the government should be acoalition government from all elected MPs.

That the new Constitution from the citizens should be amalgamated and taught in all institutions of learning in the country.

Because many people even those who are in the university don't know the Kenyan Constitution. It is this time through the civic education that we are trying to learn. Yet we still don't understand it.

That the government should provide a balance sheet showing income an expenditure before the budget day.

The other one is that the Constitution should provide a continuous civic process for proper understanding of the Constitution by all Kenyan citizens.

Political parties should be minimized to all those that reflect nationality and if possible only three and not more.

All Government workers should properly be paid to cap bribery and corruption. Now and like current all parties to be funded by the government.

There should be a Commission formed to look into the salaries of MPs, their terms and conditions of services. Instead to the Parliamentarians to a ward them to heavy salaries.

The Government should provide free primary education and provide education. I am saying primary and not secondary and higher education. Free Primary education and they should also provide equipment like books, textbook, writing material and the like.

Elections of Councillors, MP's and the President to be done on different days. The President should acquire over 50% of national votes not 25% per province.

The Constitution should provide that the rich should declare how they get their wealth.

All ballot boxes in future should be transparent to enable the citizens to see the contents.

The Government should acquire land back from the citizens after compensation using the current rate, not the old one.

**Com. Domiziano Ratanya**: Jaribu kumaliza imebakia dakika moja.

**James Biyeko:** Nimebakisha point nne tu. The President terms of office should be two terms of tree years and not five.

Kenya should be a democratic state. Which means the citizens should have given a say anything that is done by the

Government.

All Government worker and employees should bear identification cards, or uniforms, e.g. police officer, agricultural extension officer's Chiefs and the rest.

The last point is Chiefs and Assistant Chiefs should be vetted trough voting. That means they should be apply to be voted in and not by being employed through the DO or the DC.

Thank you.

**Com. Domiziano Ratanya:** Bwana James Biyeko, kuna swali. Ngoja.

**James Biyeko:** Niko tayari kujibu.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana kwa maoni yako, swali langu ni juu ya uchaguzi, unasema uchaguzi wa Rais,wadiwani, na mbunge uwe wakati tofauti. Ungependa wakati gani? Tufanye leo moja, kesho na kesho kutwa ama pawe na week katikati ama pawe na wakati gani?

**James Biyeko:** Ningependelea kama ni udiwani, ufanywe siku yake peeke yake. Kam ni Umbunge ufanywe siku yake peeke yake.

**Com. Salome Muigai:** Hiyo tumeelewe, lakini utenganisho wa kiasi gani cha wakati? Utenganishwe kwa jumaa moja, ama kwa mwesi, tumefanya leo wa udiwani, tunangoja muda gani ndio tufanya ule wa ubunge?

**James Biyeko:** Baadaya ya udiwani kutangaswa na ule wa umbunge uweze kutangaswa. Na pia wa urais ufanywe baadaya kufanya wa ubunge.

**Com. Domiziano Ratanya**: Asante Bwana Biyeko. Utaenda pale ujiandikishe kwa register yetu. Asante kwa maoni yako. Charles Wahome.

**Charles Wahome:** Ninamacheche tu kuhuzu marekebisho yetu ya Katiba. Ya kwanza ningetaka kuhuliza katika marekebisho ya Katiba kuna arid areas na semi arid areas. Wakati ule serikali inapata pesa kutoka kwa koti au msaada wawote kutoka kwa nchi za nje, ninatakakuliza watu ambao wanaishi katika ari areas na semi arid areas, wachukue kwanza.

La pili linahuzu Parliarment, Parliament wakati hule wanendelea, katika Bunge tungetaka kuwaona kenye TV, tuone vile

wanazungumza na tuwasikie kwa radio. Ili sisi wananchi tujuwe wale wanaolala na wale ambao wanaendea, ili tuweze kuwachagua vizuri katika siku sijazo.

Na katika system yetu ya quota, yaani kuchukua wanafunzi wetu katika kitado cha kwanza au katika chuo kuu, ningetaka kuhuliza hii quota system iondolewe kabisa. Kwa sababu hii ndio inaleta hata ukabila. Mtu kama ni mwanafunzi, akienda chuo kuu au form one, aende kulingana na merit. Purely on merits.

Kuhuzu shule wanafunzi wetu, corporal punishment au kuchapa wanafunzi wetu viboko, ningetaka kusema, hii punishment isondolewe. Watoto wachapwe viboko ili wawe na nidhamu nzuri. Lakini iwe kwa kiasi, si kuhumiza mtoto.

Tena kuhuzu budget, makadilio, kuwe na makadilio bila kurudia kurudia, kuziwe na mini budget. Kama ni budget imesomwa, imesomwa mpaka tuelewe na tusiwe na mini budgets zinginge.

Na ya mwisho, hii inahuzu mavazi ya wanawake, nauliza kama Katiba yetu isiruhuzu mavazi ya wanawake kama mini skirts, kwa sababu hii ndiyo inasababisha mambo ya vitendo vibaya kama ya rape. Kwa hivyo mambo ya mini skirt ipigwe marufuku.

Asante sana.

**Com. Domiziano Ratanaya:** Kuna swali, Wahome kuna swali hapa.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana bwana Wahome, umesema kwamba mavazi ya akina mama ndiyo yenye inalete habari ya rape. Tunaona watoto wetu wakinajisiwa hata wenye tumewafunika na towel na kila kitu. Tuwafanye aje ili naounajisi wa watoto uhishe? Na pia jukumu lake mwamume kwa mambo yote hayo ni lipi?

**Charles Wahome:** Hii mambo ya rape hataingawa kuna wanaume wengine ambao wana-rape watoto wetu hata kama wamefa mavasi marefu. Ile style ambayo inafanya ni kwa sabau mwanamume anapendeswa na huyu mwanamke au mtoto au msichana ambaye amevaa mguo fupi. Kwa hivyo kama kuna mwanaume ambaye anarape mtoto au mwanamke ambaye amevaa nguo nzuri, huyu afungwe maisha.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey sasa tutaenda kwa Charles Olari.

**Charles Olari:** Kwa majina in full in Charles Olari Chebeti. Ya kwanza ningetaka Katiba mpya, irekebishe mahakama. Wawe na uhuru wa kuamua kezi ya mtu bila kuambiwe hamua hivi.

Ya pili, ningetaka Ma-chief wahajiriwe njisi wanahajiri lakini waende transfer kama ma-officer wengine wa serikali.

Y atatu. Mbunge wahamue mambo yao bila kuzukumwa na Head of State kusema hamtahamua mpaka tuzungumze ama ni aje. Awache wahamue wenyewe.

Local Authorities: Ningeta Local Authorities wapatiwe nguvu ya kutusha, kwa sababu local authorities ndio inakusa mwananchi direct wa nyumbani.

Ningetaka Commissioners hapo muangalie kwa makini maanake kuna mshangao. Councillor, Mjumbe, Rais wajakuliwe siku moja na wamalize term siku siku moja. Lakini ukienda kuangali councillor anapatiwa mshahara wa shilingi elfu saba kama mtu ambaye amehajiriwa kwa center hii, kuchunga maduka yaani watchman. Ni sawa na councillor. Na kazui ya councilor ni sawa na ya Rais na Mjumbe.

Uridhi wa mali: Ningetaka Katiba mpya iweke ama kurekebisha sheria na watoto waote wawe sawa. Wasichana na vijana wapate mali kutoka kwa wazazi wao. Isiwe wasichana wanakaa kama hawakuliwa ama wataenda, ama wakienda waende kabisa. Maanake wasichana wakienda kazini unaona zaid siku hizi wanasidia wazazi sana, na huku tunawanyima mashamba. So mimi ninasema uridhi wa mali, uwe sawa.

Masomo ya primary na nursery iwe free kwa kila namna. Facilities na mjengo.

Ningetaka kila province ijitawale. Kila Province ijitawele kama Municipality na County Council. Kwa hivyo ningetaka kuwe na majimbo. Kila jimbo, simaanishi ikitongea hivyo watu wengine wahamishwe wale ambao walikuja kwa wengine, No. Ninamanisha ya kwamba wajiongoze, kwa sababu kuna watu wengine wanatoka kwa mahali wametoka na hawezi kuamua kitu mahali alipo mpaka ahamuliwe. Thank yiou very much.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey Asante Bwana Olari, kuna swali.

**Com. Salome Muigai:** Bwana Olari asnate kwa maoni yako mimi nina swali moja kuhuzu Chief. Kwa wakati huu Chief wanahajiwa kutoka pahali fulani, kwa ajili anajua mambo yaliyuko kwenye hiyo sehemu ambapo amechakuliwa. Ukisema kwa wapelekwe transfer kama kila mtu wengine, basi unatwambia tuwaajiri tu vile huwa tunawaajiri kutoka location, na tuwapeleke location singine ama mikoa mingine ama usema tubadilishe kabisa.

**Charles Olari:** Mimi nilisema mbeleni, walikuwa wanajiheshima kwa hiyo heshima ya kuchaguliwa kuwa pale pale na kukaa mpaka aende retire. Lakini shida ni hii, waki-mess, tunang'ang'ana kuvuta ama kungojea retire. Na kuvuta mtu ni chuki kati ya mwingine na mwingine. So kwa hivyo mimi kwa maoni yangu, ni ya kwamba aende transfer, kama ni mwingine tutafunza kazi ka DO. DO huwaatoka mbali na ameelewa area.

**Com. Domiziano Ratanya**: Inaonekana una memorandum, lakini kama kuzungumza machache, don't actually read but hightlight the main points.

**James Theuri:** That is what I will do.

**Com. Domiziano Ratanya**: Five Minutes.

**James Theuri**: Further more ni fupi sana. Majina yangu kamili ni James Theuri Maina. I have the following recomentations to make to these commission.

1. If Parliament finds need to amend any clause in the Constitution, the matter should be subjected to a referendum. The said referendum should be conducted by a Commission named by President and vetted by Parliament.
1. Only a party that manages to attain a set minimum number of Parliamentarians, say ten, should be financed from public funds.
1. We should retain the Unitary system of government and some of the affairs of State should be put under local authorities which are closer to the people. Examples of such affairs are, management of primary schools, maintanance of rural roads and water supplys.
1. The language test requirements should changed so that the new requirement should be a form four or secondary school for both Civic and Parliamentary candidates. To ensure broad understanding r broad education.
1. The allowances for councilLors should be reviewed and increased to attract more compensation from Secondary and University graduates. Who would in turn provide paper-qualified manpower. These would be in keeping with the demand as per devolution of some powers from the central government to the local authorities.
1. There should be a set minimum of land acrerage owned by an individual that should be exempted from taxation say fifty hectares. Any extra one should be taxed by local Authorities so that the question of a ceiling of ownership of land should not be there. Instead any land beyond fifty acres should be taxed. The revenues so earned will would improve the services required from the from the Local Authorities. Somebody holding more than fifty hecrates if he gets feed up with the taxation should sell to those who are landless. And those we are landless will get land.
1. Any applicant for the position of a Chief or Assistant Chief should as well have attained a Secondary certificate of education. The Applicants shoulod as well be subjected to election by the residents.
1. Finally the Chief elders should get allowances from public funds. Asante.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey asante sana James , weka sahihi pale. Swali moja liko.

**Com. Salome Muigai**: Thank you very much for your very very focused submission. I have two questions. One is on the Chief and Assistant Chief being o'level, there are still parts of these country where there is a whole location without even

secondary school. So what do we do with the people of that area. Two the Chief elders, are these male or female?

**James Theuri:** Thank you, the first question I would like into like that Kenyans these days are learned and almost all over the Country from Mombasa to wherever I have found that people even graduates, I read even of a graduate taking the position of an assistant chief in Nyeri. An Assistant who is a Uninversity graduate, that means even in those areas possibilities are there are people who are qualified to secondary education.

Now the second question, I would suggest and this is my feeling that whatever job opportunity, it does not matter where, the gender question should not arise. It should be acquired by anybody a man or woman. Thank you.

**Com. Domiziano Ratanya:** Samuel Kariuki, ni wakati wa Francis Kariuki. Machine imeanza kufanya kazi sasa. Asante.

**Francis Kariuki:** Majina yangu ni Francis Kariuki Mwangi.

1. Ningependa haki za binadamu zilindwe.
1. Uchaguzi ufanywe baada ya miaka mine.
1. Ningependa kura siesabiwe katika vituo vya upikaji kura.
1. Ningependa kuwe na uhuru wa kuishi na kuwa na mali popote katika jamhuri.
1. Elimu iwe ya bure na ya sawa kwa watoto wote wa shule za msingi ichini Kenya.
1. Matibabu yawe yakidolewa bila malipo katika hospitali za umaa.
1. Mikutano na mahandamano yeyote ihalalishwe.
1. Mishahara katika utumish wa umaa ilipwe kulingana na vyeti vya elimu kuepusha migomo ya hapa na pale.
1. Ningependa jeshi la Kenya Army liusishwe kikamilifu katika kazi za manufaa kwa Wakenya kama kujenga barabara, madaraja na mashule.
1. Ningependa kikosi cha polisi wa utawala kivunjwe na kiunganishwe na Kenya police.
1. Ningependa Kenya iwe ya vyama vingi milele na milele.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey Bwana Francis Kariuki, milele na milele asante sana. Peter Mwangi.

**Peter Mwangi:** Majina yangu ni Peter Mwangi Gure. Kwanza kabisa ningependekeza ya kwamba tuwe na serikali ya umoja wa kitaifa.

1. Raisi wa jamuhuri, ningependekeza ya kwamba, awe na kiwango cha elimu cha o'level, form four na kuendelea. Asiwe na chini ya umri wa miaka arubaine na asizitishe miaka sabini. Awe hajausika na kisa chochote cha ufisadi na awe akichakuliwa moja kwa moja na wananchi.
1. Ningependekeza ya kwamba makamu wa Rais awe akichaguliwa moja kwa moja na wananchi na awe akilindwa na

Katiba na asiwe akifutwa kazi na Rais.

1. Ningependelea ya kwamba, raia wa kawaida ambao hawana uwezo wa kimahakama, wawe wakipatiwa free legal representation na malipo yote yawe yakilipwa na serikali.
1. Mawasiri wote wasiwe wanachama wa Bunge. Wawe wakiajiriwa kazi na Bunge.
1. Ningependelea ya kwamba tusiwe tukifuata mtindo wa simple majority bali kila moja awe Mbunge au Councillor ama Rais awe amefikia kiwango cha hamsini na moja kwa mia.
1. Wabunge pia ningependelea ya kwamba wawe wakichukua mawaidha kutoka kwa wananchi wakati ambapo wanapitisha mambo muhimu katika Bunge.
1. Kuhusiana na kiwango cha 25% kwa provinces, ningeonelea kitupiliwe mbali na tufuate mtido wa hamsini na moja kwa mia.
1. Kuhusina na elimu, nengeonelea ya kwamba, watoto wote wa taifa hili wapewe elimu ya bure kufikia kiwango cha form four.
1. Kuhusiana na hali ya mashamba, ningeonelea kila mwananchi aruusiwe kuwa na maximum ya 50 acres.
1. Pia ningeonelea ya kwamba kwa wale ambao wamemaliza shule, na hawakupahatika kuajiriwa, pawe na mbinu ya kuwapatia loan ili waweze kujiendelesha kimaisha.
1. Na mwisho kabisa ningependelea ya kwamba, katika jamhuri ya Kenya, wanaume wasiruhusiwe kuoa wanaume na wanaweke wasiruhusiwe kuoa wanawake.

Asante.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey asante sana Bwana Peter Mwangi kwa maoni yako. Tutaenda councillor Chenge Mwangi.

**Councillor Chege Mwangi:** Asante sana kwanza ninataka kuwe na National Institution, ambazo sitakuwa na mtazamo na hali ya Ukenya. Na hii inawezekana kama tutakuwa na fairness tukichukua watu katika idara kadha, mahospitali ama kuajiri watu. Na pass mark iwe ni qualifications ambazo sitaandama na ethics. Ni lazima tuwe na Job ethics kwa watu wote ambao watawekwe Kenya. Katika utengenezaji wa national institute, ni lazima pia tuwe na vitu kama public national growth ambao pengine ya akina mama na wanaume ndio tuweze kusema kuwa tuna mtazamo mmjoa. Tunaonekana kama Wakenya na mtazamo wa inje.

Ya pili ni kwamba mambo ya uchaguzi, ni kwamba watu ambao watachakuliwa wakiwa ni Rais, Diwani na Wabunge wapate atleast 50% and above. Na kama hawataweza kupata 50%, ni wale wawili ambao wataku karibu, warudie ili kama ni location inakuwa na representaive nzuri ya watu wote. Tusipate watu ambao ni viongozi but wamechaguliwa na watu wachache. Na pia kwa madiwani ni lazima kuwe na clause katika Katiba yetu na MP’s pia na mbunge ambao tunaweza kuwatoa kwa viti vyao kabla ya muda wao kuisha. Kam hatuwezi, tunaona kwamba kazi ya hairidhishi, ina umuhimu sana tuweze kuwatoa kabla ya kipindi chao hakijaisha kwa kuweka clause katika katiba yetu.

Jambo lingine ambalo ni kwamba katika sharing of the power nguvu ambazo siko katika bunge siletwe katika hali ya udiwani. Katika hali ya local Government ambapo watasimamia mambo kama elimu, barabara, hata rasimali ambazo siko hapo. Na hii inawezekana pia hawa watu ambao tutawajia hapa watapewa umhimu mkubwa wa kuangalia education qualifications. Atleast education ya form four itafaa.

Jambo lingine ambalo ni la mhimu kwa Wabunge ambao watachaguliwa na madiwani ni kwamba, kipindi chao wakichakuliwa kama diwani, kura siesabiwe mahali sinafanyiwa na kama mwezi moja tunachagua local government, then after one month tunaenda Parliamentary na mwisho tuwe na Presidential election ambayo inatasaidia sana.

Jambo lingine kuhuzu …..resources. Ni ya muhimu sana katika kila sehemu. Wawe na uhuru wa kuamua mali yao. Kama niforest inatakiwa kupewa raia, watu ambao wamesunguka hiyo kijiji, kuwe na ….. ambayo itachunguza na wahamue kwamba ni sawa. Kama ni barabara inatengeneswa, watu wa ile sehemu ambapo barabara hiyo inapita, wawe na uhuru wa kusema barabara hii ndiyo tunaka itengenezwe wala si hii. Isiwe inaamuliwa pengine na madiwani kule ama anaamuliwa katika bunge na mambo mengine kama hayo. Kama ni maji, pia tuamue katika sehemu ambapo watu wanatumia hayo maji.

Jambo lingine ambalo ninataka kuongea hapa ni kuhuzu bishara. Ni muhimu sana Kenya tunapoingia katika trading block kama ECOWAS na zingine na tungalie zile ambazo hasitaumiza. Maoni yangu ni kwamba Kenya haitakiwi kufanya biashara katika hizi blocks, kama hizi za Africa. Kwa sababu katika hii, nchi zingine simeendelea sana kama South Africa na inafanya mzao yetu yasinunuliwe hapa na pia Egypt imeendelea sana kuliko sisi. Hii ni mambo ambayo tungomba itoke, na kama haitaweza, tupewe substitute na pia farmers wapewe substitute. Kama pengu za bure ama 20% bei. Madinga pengine diesel na kadhalika ndio tuwese kushindana sawa na nchi ambazo simeendelea kama South Africa , Egypt na nchi zingine.

Kuhuzu lands, title deed inatakiwa either iwe ni ya familia na ninapo sema familia ninasema itolewe kwa Mzee, bibi na watoto, kutoa huu ukora wa bwana kuuza na watoto wanawanjwa inje. Na kijana yote na msichana yeyote ambaye anafikisha miaka 18, ana haki ya kupewa sehemu katika urithi wake. Kama ni Title Deed badala ya kungojea mpaka mwisho. Ni hayo tu ambayo ningetaka kutoa. Asante.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okey, asante sna Councillor ngoja pengine kuna maswali

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana diwani, langu ni swali juu ya hiyo point uliyotoa ya mwisho, jana tuliambia na mama fulani pahali tulikuwa kwenye Constituency kuwa, watoto wanapofikisha miaka fulani na kufikiria shamba ni zao, wanaona kama wazazi sasa wamekuwa pingamizi kwa mali yao, na saa ingine wanaweza hasa, huyu mama wanaweza hata kufikiria chama za kuua wazazi ama vile wengi waondoa wazazi ili wakose kusinama kati yao na imani. Kwa hivyo tulionelea kama kuwa wazazi wachukua hii mali wanayo, kama kinga yao wenyewe. Je wewe umekuwa diwani, unakaa na watu, unaona

nini juu ya hayo mambo?

**Chenge Mwangi:** Jambo muhimu ni kwamba watu wengi tunangojea kwamba tutapata hii mali. Na sana sana Kenya ambapo watu hawana Kazi, watu hawajasoma na hawana chochote kingine. Ukimaliza shule ni hiyo education ulipewa formal education na huna kitu kingine. Hii ndio sana sana unasema, inafanya hata kijana kufikiria kumua baba yake ili mali agawe. Lakini kama ingewekwa katika Katiba yetu, at 18 kama mna heka kumi utapewa moja ni yako, ingine ni ya mama, ya papa, hii mambo ingizuia mambo haya, kwa sababu tunajua ikifika hapo, nitapewa yangu. I develop kulingana na uwezo wangu, kuliko kungoja papa akufie akiwa na miaka seventy na mimi pengine nitakuwa na sixty. At these time hanikipewa haitanisaidia. Itakuwa ni bure na nitakuwa na watoto wangu pia nao wanataka ile ile sehemu ambayo nimepewa na mashamba yamekuwa kidogo. Asante.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey asante sana Bwana Councillor, uende hapo ukajiandikishe, sasa wakati wa sasa tunamuita Honourable Errick Morogo, apeane maoni yako.

**Hon. Errick Murogo**: Kwa jina naitwa Errick Morogo Mbuge wa Rongai. Natoa maoni yangu ikiwa ni yangu binafsi na wale wengi wa Rongai ambao hawatapata nafasi ya kuonana nanyi.

Kwanza ningependa kusema nyinyi kama Commission mtupe muongozo kwa mambo yenu. Tunataka umoja kati yenu. Hatutakitusikie mwenye kiti wenu anatoa mahagizo na nyinyi mko kwa field. Mimi ninaona kama he is not leading. Na sina haibu kusema kwamba lazima alead asiwe mwenye ku-mislead. Othersiwe ninatakia Wakenya Katiba mpya nzuri ambayo itachukua muda mrefu. Msiwajilie wanasiasa wawashurudishe, mpaka mharakishe au mkachukua muda mrefu. Fanyeni kazi vile tuliwachagua na Wanakenya walipa jukumu mpaka mtimize kwa wakati wenu, na mtupe Katiba iliyo nzuri.

Basi nitatoa maoni kuhuzu rasilmali za nchi hii. Mimi ningeonelea kwamba hali ya maji, serikali ya Kenya ilasimishwe na Katiba itoe maji kwa kila Mkenya kwa muda fulani. Kwa sababu tukitaka kupigana na umasikini kwa haki, lazima tuwe na maji kwa shamba la kila mwananchi. Maji ya kuweza kufanya irrigation for atleast two hectares. Na serikali isiwajilie market forces kwa mambo ya produce ya mashamba. Serikali ilazimishwe na Katiba inunue kutoka kwa wakulima na tena kwa bei nzuri. Hii inamanisha kwamba mkulima akilima heka yake mbili anajua akivuna atapata mahali pa kuhuza na atapata kiasi fulani kwa mazao yake. Hivyo hivyo serikali ujiuzishwe zaidi kwa mambo ya security na mambo ya mabarabara. Na mambo mengine inaweza kuajia wengine.

Basi kuhuzu mashamba ninajiunga na wenzangu wananchi kwamba mashamba makubwa Kenya yawe ya umaa. Lakini raia watu wapate not more than two hundred per person. Na mimi ninasema per family hata si per person.

Na pia uhuru wa kuabudu, ningependa uhuru wa kuabudu uwe unafuatana na mila zetu za ki-africa. Ninajiunga mnenaji wa

mbeleni aliposema kusiwe na mambo ya kingeni nchini mwetu. Mpaka unakuta wanaume wawili wanafunganishwa ndoa kanisani. Mambo haya yasikuje kwetu ati kwasababu inafanywa mambo mengine. Kwa hivyo freedom of whorship iwe limited na mila zetu. Hayo mambo mabaya yasifanywe kwa jina la kujificha kwa freedom of worship.

Basi kuhuzu vile serikali inaendeshwa Kenya, mimi ninapendekeza, serikali ya Kenya iwe ya democrazia na ambayo wananchi wanaona na wana-feel kwamba kuna democrazia. Kuna vyama vingi, mimi sisemi viwe vitatu ama kumi, ninasema kila mtu awe free lakini namination yao iwe ni standard. Kam ni ya chaham hiki iwe ni standard na chama kile kingine. So that the level of playing ground iwe level kwa wote. Hivi kwamba wananchi wakisema tunachakua fulani iwe ni yule wananchi wanataka kumchakua ndio iwe huyo ndiye anachakuliwa.

Pendekezo lingine ni ili kwamba tuwe na office ya makamu wa rais, tuwe na office ya Prime Minister na wadogo wao na zote ziwe Constitutional. Na hawa President asiwe na uwezo wa kuwafuta kazi. Wananchi wajague ana President asiwe na uwezo wa kufuta Prime Minister au Makamu wa Rais, ili Makamu wa rais akiwa makamu, in the event of the President kuondoka kwa njia yeyote, hakuna kurudi nyuma kwa wananchi kupiga kura. Kwa muda unao zalia wa term ya President. Hivi ni kama ile ya American System.

Pia uchaguzi wananchi wawe huru kuchagua wambuge wao. Na hawa Wabunge watimize miaka yao, yale wananchi wamewapa. Ninapinga hii celling ya mwingine kusema Wabunge wawe recalled. Mbunge hatafanya chochote kama ameshinda mwenzake kwa kura mia mbili, ni rahisi kwa yule ameacha nyumbani ku-vote na ku-manupulate mpaka hiyo mia mbili iende upande wake. Kwa hivyo wananchi itakuwa ni kura mwaka huu, kura mwaka huo. Tuwape tu wananchi wachague yule ambaye wanataka. Na huyu aende kwa miaka mitano, na asisidi miaka kumi. Wabunge wasisidi miaka kumi.

Ingine ni kuhuzu masomo, pia ninajuhunga na wengine kusema masomo yetu yawe kwa Primary na university yawe free and compulsory. Neno kubwa ni iwe compulsory ili ifikie wananchi wote katika nchi.

Pia sehemu ya Rongai unajua ni sehemu ambayo ikuwa ya wazungu na wanananchi hawa wengi wainunua mashamba yao. Wako hapa kwa sababu walijinunulia mashamba. Na kuna makezi yanendelea wengi walijinunulia mashamba kupitia ushika, companies na wakati wanataka kumiliki hao mashamba yanachukua up to ten ot twenty years. Directors wana-charge katikati, inakuwa vigumu kwa raia kupata haki zao. Ningesema katiba hi mpya tunatarajia ihunde korti special ambayo inaitwa land court. Kama vile commercial courts, criminal courts na mambo hayo. Na siwe na officers competent kusikia na kuchukua hatua na uamzi katika wakati ufao.

Ninapendekeza pia kwamba tufudulie mbali Provinces, Districts na tuwe na Constituencies. Siwe centers ya kupokea na kutawanya rasilimali za nchi. Kwa mfano Nakuru tuko na wabunge sita. Na wakati tunapata kukawanya mali za jamhuri ya Kenya, naona Nakuru hatupati haki yetu kwa sababu tukio wengi kuliko wengine. Kwa hivyo tunasema, mambo yaende kwa

Constituencies. DC awe kwa Constituency. Wawe na mbuge na wapange mambo yao. County councll iwe na Constituency, na sio kwa Districts.

Basi na lamwisho kwa yale ninasema orally tumesungumza sana sana juu ya corruption au ufisadi katika nchi hii yetu. Mimi ninaonelea tukitaka kumaliza ufisadi kwa kweli, tuwe wajasiri. Na tusema mambo ya transparent. Tusema kwa location hii ya ……kuwe na office mahali kila mtu jina lake linaoneka na mali yake. Na akiuza ng'ombe yake, ionekane amepata leo kiasi fulani. Akiwekwa keshi million mbili, kila mtu atajua hii milion mbili imetoka wapi. Kwa sasa tunasema tajiri akija hapa, anapokewa kwa heshima sana, na tujuhulishe hii utajiri yake alipata wapi. Sasa mimi nina pendekeza hata hii siri ya bank ambayo zinaweka siri, mimi ningetaka kila bank iwe transparent. Kwamba Commission fulani ako na pesa fulani na alipata kwa haki kwa njia hii na hii. Na raia waweze kukagua. Basi kwa hayo mengi, ninawashukuru kwa nafasi ambayo umetupatia na memepatia watu wa Ronga kwa freedom iliyo nzuri sana. Sioni mtu ameharakishwa akitoa maoni yake.

Basi ninatao written document.

**Com.Domiziano Ratanya**: Asante sana mheshimiwa kwa hayo amaezo yako ya memorandum yako hiyo na wakati unaenda utupatie. Tuiweke huko kwa Commission. Na sasa kuna maswali ngoja kidogo.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana muheshimiwa mimi nina maswali mawili kwako, umesema kuwa elimu iwe ya bure na kushurutishwa, kutokea kiwango kipi?

**Hon.Errick Moroko**: Asante sana, kutokea kiwango cha Primary na iwe compulosory, secondary iwe free. I know ni ghali lakini serikali iweze hata ku-tax sisi higher kidogo lakini tupate masomo free. Mpaka primary iwe ni compulsory. Na university serikali igharamie. Ighamie kabisa ili watoto ambao wana akili wasikuse kusoma kwa sababu wazazi wao ni masikini.

**Com. Salome Muigai:** Okey Swali langu pili ni juu ya security, umeleza transparency bila kuangali hali ya security wakati huu. Kama leo tumesikia malalamishi hapa na pale habari ya watu kukutwa na wezi kwao na vitu kama hivyo. Sasa tukiweka hapa kuwa mzee fulani honourable ameuza ng'ombe mia mbili na amebeba leo million tatu nyumbani, je security nayo tunaizungumzia aje ama pengine iko kwa memorandum yako?

**Hon. Errick Morrock:** Ningesema kwa security, jukumu kubwa na la kwanza la serikali iwe ni security kwa wote. Basi wakati mazee au mama ameuza mali yake kusiwe kunaonyeshwa wakati huo but after one week iweze kujapishwa. Kuonyesha imeingia hivi na hii imetoka. Pia akinunua ionekane ametumia hiyo pesa kufanya hivyo. Asante.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey asante sana Mheshimiwa tupatie hiyo memorandum na using register yetu. Sasa wananchi ninaona kwamba tumekuwa wengi na hiyo ni mzuri na ningetaka kurudia kidogo yale niliyosema asubuhi wakati tulipokuwa

wachache. Na hayo ni mambo mawili tu ya kwanza, ni wakati unakuja hapa unapewa dakika tano peeke yake kueleza memorandum yako ama maoni yako yale unayo na kama una memorandum na hautaki kuongea, unaweza tu kupeana na uende.

Kitu kingine nilisema kwamba tutafuata hii list lakini Commission ina uhuru wa hata kurugia ukiwa na sababu ya kutosha. Na kwa sababu mpaka sasa tumesikia akina baba karibu forty two, wakina mama ni kama wawili, kwa hivyo nitatumia hii nguvu yangu kama Chairman kuwaida wakina mama ambao wamejiandikisha hapa na wewe tayari nao kupeana maoni yao. Sasa nitaendelea kulingana na list yangu kuna Grace Njoki, aje. Grace Njoki sema jina lako.

**Grace Njoki:** Ritua riakwa ne Grace Njoki.

**Translator:** Jina langu ni Grace Njoki.

**Grace Njoki:** Ondu oria ingeenda turoreruo muno

**Translator:** Ile mbayo ningependa litaseme sana,

**Grace Njoki:** ne ohoro wa mueritu na mwanake

**Translator**: ni juu ya vijana na wasichana.

**Grace Njoki**: Matige kugayanio

**Translator:** waaje kuakawanywa,

**Grace Njoki:** Tondu ciana icio ni imwe.

**Translator:** kwa sababu hawa watoto wamezaliwa pamoja,

**Grace Njoki:** Kwoguo ningwenda ondu oco'yo oruruo muno akaro ne ogai wa migunda

**Translator:** na kwa hivyo ningepnda jambo hili urithi kuhuzu wa shamba.

**Grace Njoki:** Mwana wa muritu atige koheuo point ithano na ocio onge akaheuo acre ithano

**Translator:** huyu mtoto asipewe kidogo na kijana apewe kubwa.

**Grace Njoki:** Ne maigananio.

**Translator:** Wasawasishwe.

**Grace Njoki:** Haria hange engienda turoreruo.

**Translator:** Kuna mahali ningelipenda tutasame,

**Grace Njoki:** Ne ohoro wa muthuri na mtumia. Mtumia agatigo kuonuo tatari wa mocie

**Translator:** ni juu kuhusu bwana na bibi, mwanamke asionekane kama kwamba si wa nyunbani.

**Grace Njoki:** Ati indo ne cia mthuri ewike.

**Traslator**: Kwamba mali ni ya bwana pekee yake.

**Grace Njoki:** Hondu hauo hagerere indo ikoro icitu ithueri.

**Translator:** Inahitajika mali iwe ni yao wawili mke na mume.

**Grace Njoki:** Mahinda maria mthuri ange'hera ndigakoro ne andu kuga indo igothi oo no oo.

**Translator:** Na kama bwana akifariki watu wengine wasikuje kuchukua mali ya bwana yangu.

**Grace Njoki:** Tondu onani ndakwa indo igotigo iciake.

**Translator**: Kwa sababu hata nami nikifa mali itabaki ikiwa yake.

**Grace Njoki**: Ohoro ocio onge ne wa MP, Councilor na acio ange.

**Translator:** Na la tatu ni kuhuzu wabunge, councilor na wengine

**Grace Njoki**: Ange'thuro miaka itano itare methiro

**Translator:** Na kama tutakundua kabla ya miaka mitano kupita,

**Grace Njoki:** Na agi gotorutera wira mwega.

**Translator:** Na asifanye kazi nzuri,

**Grace Njoki:** ne agerero tureko tutome marua natomurege.

**Translator:** twaitajika tutume barua na tumuondoe.

**Grace Njoki:** Tondu miaka itano igegathira ne tugothinika muno.

Tr**anslator:** Na kwa sababu kabla ya miaka mitano ihishe, atakuwa ametufinya.

**Grace Njoki:** Namba inya.

**Translator**: Na nambaru ya nne.

**Grace Njoki:** Thipitari ne twagete ndawa.

**Translator:** Hospitali tumekosa madawa,

**Grace Njoki:** Na neturenda thipitari turorero muno.

**Translator**: Na tunahitaji tuangaliliwe jambo hili la mahospitali sana.

**Grace Njoki:** Ni tutwikere andu agothira ne kwaga mbeca cia gothi thipitari.

**Translator:** Kwa sababu tumeangamia kwa sababu tumeangamia maana hatuna mali ya kutupeleka kwenye hospitali za pesa.

**Grace Njoki:** Na ho namba ino angi

**Translator:** Na number nyingine,

**Grace Njoki:** Ne ohoro wa Kanjo.

**Translator:** ni habari ya council

**Grace Njoki:** Turoreruo ohoro wa kanjo neguo matige gototera indo.

**Translator:** Maana hawa askari wa council wanapoingia ni chini wanamwaka mali ya wananchi,

**Grace Njoki:** Na gokuo indo cia andu na matiracokia.

**Translator:** Wanabeba mali yao yote

**Grace Njoki:** Na tondu matirahoto gotogitera kori aria maratukora na mecika.

**Translator:** kwa hivyo kwa sababu hawajafaulu kuangalia ambao wanatuka kwa bunduki

**Grace Njoki:** Marathokeria oria orethira ciana ciake gia koria.

**Translator:** Wanaenda kuaribia mwenye anajifanyia kazi biashara yake.

**Grace Njoki:** Oguo ondi ocio turoreruo.

**Translator**: Na kwa hivyo jambo hili litazamwe sana.

**Grace Njoki:** Ne oguo**.**

**Translator:** Ni hayo**.**

**Com. Domiziano Ratanya:** Kuna swali Grace Njoki, ngoja kidogo.

**Com. Riunga Raiji**: Mama hii mambo ya Council unasema mnaharibiwa mapka hii mali yenu na upande kazi

**Translator:** Muthokagerio indo cianyo ne thigari atia?

**Grace Njoki:** Mahinda maria kanjo eroko gothiororoka goko**.**

**Translator:** Wakati hawa watu wa Councill wanakucha kusunguka hapa,

**Grace Njoki**: Makeria Town

**Traslator:** hasa mijini,

**Grace Njoki:** Ne reria tuthete town**.**

**Translator**: Wakati ambapo tumenda mjini,

**Grace Njoki:** Tukoraga macai maria tunyuaga ne matiro**.**

**Translator:** Tunakuta Chai ambayo imepigwa pale kwa stage imemwaga,

**Grace Njoki:** Ne tungenda andu acio maroro muno

T**ranslator:** tungependa watu hawa watazamwe sana.

**Grace Njoki:** Neo marathi magatunyita ogeni.

**Translator**: maana hawa ndio watu wanatukaribisha kule mjini.

**Grace Njoki:** Nekio ndauga maroro muno**.**

**Translator:** Kwa hivyo serikali itazame watu hawa wa council sana.

**Com. Domiziano Ratanya:** Sasa tunamuita Jedida Wanjiku. Ni wakati wako Jedida Wajiko. Na useme jina lako.

**Jedida Wanjiku:** Kwa majina ninaitwa Jedida Wajiku. Ningetaka kuzungumza kuhuzu wasichana na wavulana wanao enda ng'ambo. Inaonekana msichana akienda ng'ambo kwa masomo na aolewe huko na apate watoto, wakati wa kurudi hapa

Kenya inaoneka watoto wake na mwana yake mzungu anazuiliwa kuingia Kenya. Lakini mvulana akienda apate bibi huko na watoto kuingia Kenya ni rahisi. Ningetaka kuhuliza Serikali yetu hakuna msichana na mvulana, wote tulibeba miezi tisa. Kwa hivyo hakuna mtoto wa kijana na wa msichana. Ningetaka hiyo mambo ichunguswe sana.

Lakini kuhuzu wafanyayi kazi wa serikali, wakati wamemaliza miaka hamsini na tano wanapatiwa retire, na wakati huo inaoneka wanatumia barua ya retire lakini pesa haipatikani. Wanachukua muda kwenda Nairobi kuangalia pesa zao. Ningetaka wakati retire inanatayarishwa pia pesa ziwe tayari. Wafuatanishe pesa na retire yao. Sina mambo mengi.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey asante sana Jedida, sasa ni Naomi Wambui, Naomi wambui yuko? Lucy Wanjiuku na Martha Mwala naye angoje. Lucy Wanjiku, ni wewe Lucy Wanjiku. Niwe Lucy Wanjiku? Asikii. Na aseme jina lake.

**Translator**: Aria ohoro waku reuo.

**Naomi Wambui:** Anaitwa Naomi Wambui.

**Translator**: ogo ohoro waku.

**Naomi Wambui:** Neye ndire na maundu mangi

**Translator:** Anasema yeye hana maneno mengi ya kusema.

**Naomi Wambui:** Ne gutu gwakwa gutaragua wega.

**Translator:** Anasema ni masikiyo yake iliharibika si kupenda kwake.

**Naomi Wambui:** njikaraga kahora.

**Translator:** Na anaka pole pole.

**Naomi Wambui**: ne ogu tu.

**Translator:** Ni haya tu.

**Com. Domiziano Ratanya:** Martha Mwala sasa.

**Martha Mwala:** Njetago Martha Mwala.

**Translator:** Martha Mwala

**Martha Mwala**: nderenda kuga mbego iria tuhandaga.

**Translator**: Ninataka kusema mahindi ambayo tunapanda sisi,

**Martha Mwala:** Na pego iria toheyago.

**Translator:** na pengu ambazo tunapewa,

**Martha Mwala**: Cietu ondu umwe.

**Translator:** sizawasishwe.

**Martha Mwala:** Tukeendia

**Translator:** Tukiuza

**Martha Mwala:** Tuendie ouguo

**Translator:** tuuze hivyo hivyo.

**Martha Mwala:** Tukegora tu gore ooguo.

**Translator:** Na tukinunua pengu

**Martha Mwala**: Na tugore ouguo.

**Translator:** Tununue hivyo hivyo.

**Martha Mwala:** Wa keri

**Translator**: la pili

**Martha Mwala:** Gatiba ndikaye kungerero.

**Translator:** Katiba isiongoswe muda,

**Martha Mwala**: Eee

**Translator:** Ndiyo

**Martha Mwala:** Wa gatatu

**Translator:** Na la tatu

**Martha Mwala:** Maundu maria tukorago namu goku borori.

**Translator:** Mambo ambayo tuko nayo hapa nchini

**Martha Mwala:** Ne turi na Chief.

**Translator:** kuna Chiefs,

**Martha Mwala:** Na Head man

**Translator**: kuna headmen,

**Martha Mwala:** Na kwena mundu tucagorete wa gothi Mbung.

**Translator:** kuna mtu tumechagua wa kwenda Bunge,

**Martha Mwala:** Na andi acio othe marenduo maturarage ithui.

**Translator:** Na hawa watu wanahitajika watutaseme sisi.

**Martha Mwala:** Wa kanna

**Translator:** La nne

**Martha Mwala:** Ne twaheruo uhuru.

**Translator:** Tulipewa uhuru

**Martha Mwala**: Na turarurana ithue ene.

**Translator**: na tunatazamana sisi wenyewe kwa wenyewe.

**Martha Mwala:** Goko gotiti mthuko.

**Translator**: Hapa hakuna mzugu,

**Martha Mwala**: Wathi office no mundu muro.

**Translator:** Na tukiingia offisi tunakuta tu ni mwafirika.

**Martha Mwala:** Uhuru ne witu.

**Translator**: Na uhuru ni wetu.

**Martha Mwala:** Na twarima irio citu tutingetokio ne cio.

**Translator**: Na kama tukilima chakula chetu hakitupi utajiri,

**Martha Mwala**: Koria tuikaraga tondu ne twaumere gikuyuni tugethi Rivft Valley tutire na murori.

**Translator**: na kama tulitoka Kikuyu tukakuja Rift Valley na hakuna mtu wa kututazama,

**Martha Mwala:** Tukwenda andu aguturora itora ritu.

**Translator:** Na kwa hivyo tunaka wale ambao tunachagua waje watutaseme,

**Martha Mwala**: Chief na Headman maturore.

**Translator:** na headmen

**Martha Mwala:** Kinya mthigari.

**Translator:** na askari,

**Martha Mwala:** Tutige gokara ugua athine athire.

**Translator:** lakini tusikae hivyo masikini pekee yetu.

**Martha Mwala:** Ne ndaigania

**Translator:** mimi nimetosheka.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey sasa wananchi, tukiendelea kuongea namna hivyo, hayo maneno mnaongea yataenda kwa machine. Na itakuwa kwamba hatuchungui maoni ya wananchi lakini ni Kelele tu tunaweka hapa. Kwa hivyo mnyamaze, yule anakuja hapa atoe maoni yake. Na wewe wakati wako ukifika uje utoe maoni yako. Muache hiyo mikutano mingi ambayo tunasikia. Na tuliagana asubuhi tutaheshimiana na tutafanya hayo mambo kwa njia nzuri. Kwa hivyo, hiyo kelele hatutaki kuisikia tafadhali. Na nikimalizia hapo, pengine tutaeshimiana kwa hayo, ningetaka kumuita Lucy Wanjiku. Okay kama Lucy Wanjuku hayuko, tuendelee kwa wengine ambao tuliajia. John K. Koskey. Ni wakati wako sasa.

**John K. Koskey:** Kwa majina nai John Kikurui Koskey. Maoni yangu ni kwamba ningetaka deputy Preasident achaguliwe na wananchi. Asichaguliwe na President kama ilivyo wakati huu.

2. utengeneswe kamati ambayo inahusika na mishahara ya wabunge, kuliko hao wenyewe wajijadilie kuhuzu mishahara yao.

3. Inahuzu mambo ya elimu, kuwe na elimu ya bure katika Primary school. Kusiwe na vitu kama kuitisha pesa ya

watchaman, vitu kama pesa ya watchman, office mantainance na na kadhalika.

3. Ma-councillors wawe watu wa form four, wasiwe ni watu ambao hawajasoma ama wa standard seven. Councillors wote wawe ni wa form four. Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Asante sana. John J. Komu, John Komu. Naona John Komu hayuko, pengine alileta memorandum naiona imeandikwa hapa. Tena tanaenda kwa Kiprono Komu, Kiprono ni wakati wako sasa. Ni wewe Kiprono, endelea.

**John Kiprono:**

**Translator:** Asante sana Commissioners pamoja na Mbuge wao.

**John Kiprono:**

**Translator**: Anasema anaona ni vizuri Katiba iangalie upande wa watu,

**John Kiprono:**

**Translator:** na mifugo, lets say pastoralist.

**John Kiprono:**

**Translator:** anaona ufukaji ni kitu ya mhimu kwa upande wake.

**John Kiprono:**

**Translator:** anaona mfugo ina faida nyinngi kwa sababu kwanza inatupea nyama, maziwa, mbolea na mambo mengi ambayo tunaweza kuhitraji katika ukulima.

**John Kiprono:**

**Translator:** Siku hizi wakulima tuna kilio kwamba bei ya mazao yetu iko chini zaidi.

**John Kiprono:**

**Translator:** Kuna hasara wakati anajaribu kufanisha uhuzaji wa mfugo na madawa yale anunue ili kutunza hiyo mifugo inatofautiana mbali.

**John Kiprono:**

**Translator:** anasema kama Nissan, jumvi na mambo mengine kama matibabu ya kutibu mfuko ni hali ya juu kuliko vile yeye angeuza mfugo yake. Bei ni tofauti.

**John Kiprono:**

**Translator:** Vile vile hata mazao kama mahindi ni vile vile.

**John Kiprono:**

**Translator:** Anasema ni hayo tu ambayo amekuwa nayo.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay, asante sana Kiprono, uende hapo kwa register yetu. Na yule ambaye anayfuata ni Francis Kios. Francis Kios tuambie majina yako vizuri.

**Francis Kios:** Majina yangu ni Francis Sirma Arap Kios na mimi sitarudia yale yamesemwa na wenzangu kwa vile pia nimeandika memorandum ndefu. Nitasema tu machache ambayo sikusikia yakitajwa na wenzangu.

Na ya kwanza ni Road safety in our Country, yaani barabara zetu nchini Kenya. Mabarabara zetu nchini Kenya yamegeuzwa kuwa vijijio vya wanadamu na ningependekeza kwamba katiba mpya ichao iangalie kwamba shida hii inakabiliwa vilivyo. Na njia moja ya kukabidhi ni kwamba, kama ni gari ya mzigo, ikibeba mzigo zaidi ya kiwango chake, ama ni gari ya abiria ibebe abiria zaidi ya kiwango yake, na ipatikane kwamba, kabla ya ajali haijatokea, na ionekane kwamba kabla ya ajali, lilikuwa limepitia road block ya polisi, basi insurance ambao wanainsure hayo magari wafanya uchunguzi makali. Na wakipa kwamba polisi walikuwa wameangalia lakini hawakufanya lolote, serikali iwajibike. Na kama kumetokea hivyo kwa kila mtu anayekufa awe kutoka mtoto ata mzee, serikali igharamie kwa kulipa jamii yake pesa isiyo chini ya shilingi million moja kwa mtu mmoja. Vile vile ikiwa ajali imesababishwa na barabara mbaya, ama gari lilikuwa likenda kwa speed nzuri, ikifanywa uchuguzi ipatikane kwamba, gari hilo limefanya ajali kwa mashimo au barabara mbaya pia serikalio iwajibike.

**Com. Domiziano Ratanya**: una dakika moja sasa.

**Francis Kios:** Ninaendelea kumaliza. Na ilituweze kumaliza corruption katika nchi yetu hata kama hii ya hongo barabarani, polisi wasaidiwe katika kazi zao na wapewe hali nzuri ya kuishi, manyumba safi na hali ya kazi nzuri.

Na ya mwisho ningesema wakati wowote Katiba ya nchi wakati itakuwa ikiandikwa, siusiswe kabisa na mambo ya uchaguzi. Uchaguzi iende kado na marekebisho ya Katiba yaende kando. Wakati wowote nchi hii itakuwa ikirekebisha Katiba yake. Nafikiri ni hayo tu.

**Com. Domizianio Ratanya**: Asante Francis Kios. Sasa tutaenda kwa Joseph Chege. Francis uende hapo. Kuna Joseph Chege.

**Joseph Chege**: I am Joseph Chenge and this are my points. President should be under law always. He should not be above the law.

Members of the Parliament should not be chosen to be ministers. They should maintain their posts.

Salary given out, should be directly proportional to the job done by a person. Citizens should be the ones to change the Constitution but not he MP or Cabinet to the President.

There should be equality in terms of development, e.g. road construction, hospitals and schools. Some areas should not be favoured than other areas.

Every citizen should have freedom to express his or her view in case of any bad happenings. e.g. killing somebody anyhowly.

Taxes and revenues should be maintained at the capability level all citizens. Primary education should be free.

Missionaries in our country should be respected. Employment vacancies should be increased by promoting factories as well industrialization.

Examination of K.C.P.E and K.S.E the leakage should be prohibited because the leakage always comes when the examination time reaches.

All citizens should have freedom of movement to every part of Kenya,. President should not threaten any citizen in our country. Devil worshiping should be condemned out of Kenya.

Elections should be done fairly and without cheating.

Thank you.

**Com. Domiziano Rataya:** Joseph Chenge, nenda pale ujiandikishe. Sasa tuna John Njoroge. John Njoroge ni wakati wako.

**John Njoroge**: Thank you Commissioners, I have three views to make. In order to minimze the joblessness, I suggest that those Kenyan tycoons who have millions of money outside the country to bring them back and utilize the money here in form Industries and so on. By then they create job opportunities and if not the money be forfeited and taken by the Government.

Common job that nay common man can handle, should be put in such a way that the employed inter into a conduct with the Government at a certain term, I mean if the lost term should be around ten years.

And the last is all the natural recourses, by this I mean should be utilized. There are saying there are some oil wells in the country, which are dormant. They should be utilized. By so doing they will be facilitating the economy. Also I support the one-man one job.

Thank you.

**Domiziano Ratanya**: Sasa tutakuwa na Joseph Keiyo lakini mbele ya hapo nitampatia Councillor wetu wa hapa wanatangazo la muhimi. Kabla pengine hajaenda. Councillor ebu tangaza hilo haraka sana.

**Councillor Peter Mwangi:** Ninatangaza kwamba ile harambe ingefanywa kesho, haitakuweko kesho mpaka wakati mwingine na hiyo tutaongea kwa sababu ni ya kwetu kinyumbani, tutaongea baadaye hatuwesisema saa hii. Asanteni. Muendelee kuchanga mpaka siku ile ingine ambayo itatangazwa. Ile ya Honourable Kibaki na other honourable MP's ambao wangekuja hapa kesho haitakuweko. Tunaomba msamaha for the inconvenience caused. Asanteni.

**Com. Domiziano Ratanya:** Baada ya hili tangazo kuna Joseph Koiyo. Joseph ni wakati wako sasa.

**Joaseph Koiyo:** Kwa majina ni Joseph Koyo. Yangu ni maoni juu ya kwa masomo ya shule. Maoni yangu ningesema masomo ya Secondary yawe ya free. Kama vile ya Primary.

1. Maisha ya binadamu, tuseme watoto kama mayatima wasinyanganywe mashamba yao na watu wengine.
2. Katika Security, kuna wizara ambayo ni idara ya polisi, wanachunga watu na unakuja kuta wao wanaiongia manyumba ya watu na kubomoa instead ya kutafuta mwizi ni nani.
2. Sisi ni wakulima, unakuta mavuno yetu tunauza kwa pesa kidogo lakini mahali tunanunua mbengu, ni ya bei ghali sana, na kwa hivyo tunafanya kazi ya hasara. Kwa hivyo maoni kwa ukulima tuongesewe kama gunia moja ya mahindi iwe elfu moja and above.

Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Asante Joseph, tunaenda kwa Allan Gitiha Kinyanjui.

**Allan Gitiha Kinyanjui:** Ningetaka kutoa maoni yangu katika Commission hii kuhuzu Katiba. Ya kwanza ningesama Ma-chief wawe wakipewa training za kutosha na pia elimu ya kutosha na transfer.

Results za mashule, hasa secondary schools, ziwe sikitangaswa katika magazeti vizuri kama zamani. Ili kuePusha wanfunzi ambao wanapelekwa katika University kwa njia sisizo faa bila kupita.

1. Masingira ilindwe vyema. Kwasababu tunshanga kuona kila mtu analia juu ya masingira. Chief, DO, na raia wanalia juu ya masingira sasa tunashindwa ni nani ambaye anasitahili kuchunga masingira, ama ana jukumu la kuweza kuchukua wakati wowote mazingira ikiharibiwa. Kwa mfano kama vile maji, kuna unyakuzi kama wa maji na mito, watu wanatumia kivyao. Dam na mengineyo.

2. Wakati wa uandikishaji wa asikari wowote, army na wengine, ningeuliza exercise hii ifanyiwe karibu kama katika location. Kwa sababu wakati inatangaswa kule district, pengine watu wengine hawapati nafasi na pesa za kufika huko

na wanafunzi wetu wamejaa manyumbani wanahitaji kuhajiriwa.

3 Ningeuliza katika Katiba hii mpya kutolewe marriage certificate tofauti au mara pili. Kwa sababu, kanisa inasimamia harusi kwamba wale amabao wameunganishwa wasitengane. Lakini wakati mwingine unakuta serikali inakubali hawa watengane. Kwa hivyo ile certificate moja inafanya hawa wawili kukongana.

2. Barabara yetu ingaliwe na iwekwe lami. Kwa sababu sisi tuko mbali sana na soko. Na wakati tunahitaji kwenda sokoni, tunakuta soko tayari limeuzwa kwa sababu barabara yetu ni mbaya gari sinafika simejelewa so ningeomba barabara yetu ingaliwe.

**Com. Domiziano Ratanya:** Wakati wako sasa umekwishe Bwana Allan.

**Allan Kinyanjui:** Iko swali moja tu.

**Com. Domiziano Ratanya:** Maliza hiyo haraka.

**Allan Kinyanjui:** Ya mwisho ningeuliza wakati wa kuchakua President, kila kabila katika Kenya liewe nafasi ya kuwa President. Kwa sababu ikiwa wana haki ya kuwa Wakenya basi pia hao wawe na haki ya kuongoza nchi kama President. Kwa hivyo iwe kama Location. Asante.

**Com. Domiziano Ratanya**: Kuna swali Allan. Keti kidogo kuna swaali.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana bwana Allan Kinyajui kwa maoni yako. Mimi swali ni kuhuzu hizi certificate, marriage certificate, sikukuelewa mzuri. Unataka mtu akifanya harusi, akiajana na bibi ama na bwana wa kwanza akioa mwingine apatiwe marriage certificater ya pili ama una maana gani?

**Allan Kinyanjui**: Ninataka ile cerificate ambayo inatolewa na serikali, wakati watu wamefanya harusi kwa DC, iwe sawa na ile inatolewa na kanisa. Na wakati mwingine serikali inaruhusu kuajana kwa wawili wa ndoa. Na kanisa inakata katika sheria zake. So ile certificate inakuwa haina use. Kwa sababu kama serikali inakupali tuachane, na kanisa kule imekubali tukae pamoja, ningesema wale ambao wanafanya arusi kanisani, wapewe certificate ambayo inalingana na sheria za kanisa.

**Com. Domiziano Ratanya:** Esther zote, Easther? Kuna mama anayeitwa Esther zote hapa? Inaoneka huyo hayuko. Nancy Waithera, Nancy Waithera? Tuna Jim Kamore? Bwana Jim yuko? Jim Kamore. Ni wakati wako Jim.

Asante sana ma-Commissioners na wahusika wote. Majina yangu ni kama mlivyosikia ni Jim Kamore.

La kwanza pengine ningependa kuzungumzia mambo ya Commissioners. Tumeona katika serikali hii ama wakati huu kuna Commission Nyingi ambazo simeundwa za kuangalia mambo kadha wa kadha. Niikuzia kidogo, tunaona wakati wa zamani tulikiwa JM Commission ya kuangalia kifo chake Tom Mboya, marehemu Muge na hata wakati wa tribal clashes, lakini matokeo yake sisi kama raia ambao pengine tulitoa maoni yetu, hatukuyapata. Kwa hivyo tafadhali matokeo ya Commission hii ningeomba tuyaone.

La pili ni soko huru, soko huru zaidi imeguzia sana sisi wakulima wa kawaida ama wananchi wa kawaida na hii ni kuhuzu uhuzaji wa mali yetu kama mahindi, maharagwe na kadhalika. Unapata ya kwamba ndio kunatokea mahindi kutoka Tanzinia Zambia Uganda na Kadhalika, unapata bei yetu ya mahindi imeshuka chini sana. Na sasa kwa sababu ni willing buyer na willing seller, yule mkulima anaumia zaidi.

Nije mambo ya maji, maji katika Constitution ile tuko nayo sasa wamema kwamba kufikia mwaka wa hii na mbili, kila mtu atakuwa akinywa maji masafi. Na hata waleo watu wengine hata yale maji msafi hawajapata. Ningeomba sana tuangaliliwe mambo ya maji.

Basi tukisema 2005, pengine kila mtu awe anakunywa maji safi maanake ungebeba maji na chupa. Ungekuja kuyakunywa hapa mfirijini tu.

Lingine ni campaign expenditure, tunapa ya kwamba tunaambiwe kiko kiwango hiki. Elfu kadha, lakini ukifuata sana, unaona inazidi hata wanatumia ma-billion ya pesa. Na lile linalofanya hatakuwe na ulanguzi, yule tukimchagua councilor, MP lazima atafute njia ya ku-recover zile pesa zake, na hata mishahara wapatishe juu ili apate zile pesa alitumia sitarudia wapi. Maanake hawezi akafanya kazi ya bure.

Lingine ni mambo ya distribution of resources. Resource distribution unapata ya kwamba sehemu zingine wana resources kama barabara, unapata hata wengine hata hawana haja na kutumia zile barabara. Ukienda pale asubuhi mpaka jioni, hakuna gari inapita, lakini ng'ombe sinapita tu. Na hapa ukiona unaona ya kwamba hapa magari ni mingi sana barabara ndio mbaya.
Tuangaliwe.

Ukiangalia mambo ya Aids kama ni chakula, chama chotechote kile kitangoza, iwe ni serikali ya mungano ama ni chama fulani, wasitumie chakula cha misahada kuwa ndicho wanafanyia nacho. Hiyo waondoe kabisa. Na Constitution itwambie wazi wazi.

Lingine tunakucha mambo ya AFC loans. AFC laons siku hizi siyo ya mwananchi wa kawaida. Imekuwa ya wale wako nazo.

Na mimi ni wakawaida huu ni wakati wa kiangazi. Hapa tunaita lower subukia, mwisho wa maendeleo, ndio kwa sababu mambo hayajafika. Loans hapa huwezi ukapata mtu anapata loan ya AFC. Bado inasonga upande wa wale wa mashamba mkubwa. Na mimi mtu wa hsekari moja, sipati ile laon. Tafadhali the payment nayo tuangaliwe. Hapa ni pahali pa kiangazi, tuangaliwe sana.

La mwisho, ni wale waizi. Mtu amechaguliwe pengine ni Councillor ama MP, na halafu apatikane na jambo fulani la wizi, tafadhali asichaguliwe kwa bunge. Na ni mwizi na alikuwa anaongoza parastal body, na ameiba hapo na ameimaliza, si mambo ya kumpa promotion baadaya ya kumtoa pale. Ni yaho tu asante sana.

**Com. Domiziano Ratanya:** Asante Jim tutaenda kwa Ibrahim Kamau.

**Ibrahimu Kamu**: Asante sana. Jina langu ni kama vile ni Ebraham Kamau Kamau. Yale maoni mimi ningetoa kwa Tume hii, ni life ya Parliament. Mimi singependelea iongeswe. Tungeenda kwa uchaguzi na ile Constitution iliyoko. Na kama kuko na marekebisho iwe ni nyinyi Ma-Commissioner, mharakishe ile ya kutusaidia tufanye elections.

Jambo lingine ni mambo ya shule, siku hizi kunaonekana hakuna watu kujitolea kabisa. Na hata watoto hawajitolei. Mimi ningeonelea mtitindo ule wa zamani, urudi, na ndivyo wakati hata kama examination zile za form four, mbeleni silikuwa sikitoka kwa magazeti, na hata wakati huo magazeti yalikuwa yakipa pesa kabisa. Ni kwa sababu kila mtu alikuwa anataka kuona shule yao au watu wao wamefanya nini. Lakini siku hizi kwa sababu watoto wanajua results sikitoka ni yeye tu ataenda. Hakuna kufanya bidii.

Ile ingine enforcement of laws. Kunaonekana tuko na laws ambazo simepitishwa lakini hazina nguvu. Ikiwa ni upande wa barabara, mabarabara siku hizi yameingiliwa mpaka mtu unaona unafunga barabara, na kila barabara iko na area yake. Ziwe enforced na ikiwa ni mto, kwa sababu kila wakati tunalia njaa, kwa sababu mazingara yamearibiwa kwa kiwango hiki. Kutoka kwa forests, chemi chemi za mito, mahali ambapo evaporation inafanyika ndio tupate mvua, imeharibiwa.

Jambo lingine ni freedom of worship. Ningependelea watu wawe wakiabudu kulingana na siku zao. Na ikiwesekana, hata serikali wakati wa kuwa na mkutano wawe wakifanya mikutano yao na isiwe siku ya kuabundu kwa sababu wakati mwingine wale wanao abudu. Tusema wale wanao abudu siku ya Jumamosi wanaokena kama wanakata kwenda hizo mikutano. Laikini ni kwa sababu…………………………….

Nao government officers wawe wakipewa mushahara ambayo ni mshara mzuri ili tuepukane na mambo hii ya rushwa. Kwa sababu rushwa ndiyo imefanya watu warudi nyuma kabisa. Lakini nikiangalia mimi ninaona ni kwa sababu ya mishahara.

Kuko na jambo lingine, circumssion ya wasichana, tunasikia wengine kama wanataka kurudisha watu miaka nenda miaka rudi, iwe si kutu ya ku-force. Kama kuko mtu anataka kuatahirisha, ni atahirishe kiviyake. Lakini isiwe ni kutu ya kuforce. Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okay Bwana Kamau hakuna swali, kwa hivyo utaenda hapo ujiandikishe. Jackson Mburu. Kuja sasa ni wakati wako.

**Jackson Mburu:** Asante sana, majina yangu ni kama vile ambavyo mumesikia, ni Jackson Mburu kutoka sehemu ya Vyiomerere. Ni na mapendekezo kadha ambayo nigependa kuwakilisha. Na ningewakilisha kwa kingereza.

Kwanza ni citizenship: An automatic citizen should be a person whose both parents are indigenous Kenyans.

Halafu ninaingia kwa defence and national security: Establishment of Martial Courts with stiff punitive measures should be used as a mechanism to discipline the Armed Forces.

**Com. Domiziano Ratanya:** Jackton ukiendelea kusoma hivyo, dakika yako tano itakwisa. Sema ile ya muhimu. Umepakisha dakika mbili.

**Jackton Mburu**: The Constitution should regulate the formation and conduct of political parties in the following way. Define the initial financial base to form parties. Set a limit of parties to be three, which should have a national wide representatives.

The Constitution should limit the powers of the President such as, inserting sections, which say he is over the law and that he can never face prosecution. The Constitution should provide a removable or vote of no confidence after the person being proved misbehaving in the office or misuse of powers.

The Provincial Administration should pay their role without enegaging themselves with political affairs. There is need for every citizen to understand to what is contained in the Constitution. So it is therefore good to make arrangements to know which media can be used to educate people. Still the Constitution play a create role in education, it should guarantee bursary funds to the poor children and those who are not able to get school fees so as to conquer illiteracy in the county.

So free education should be imposed. Still the Constitution should pay a great role in setting a side funds to the youth especially in making sure that in every Constituecy we get a running project so as to create employment to the young people.

**Com Domiziano Ratanya:** Bwana Mburu ujaribu kuharakisha kwa sababu watu ni wengi.

**Jackson Mburu:** The government should value the need the motivate young farmers mostly in providing a better marketing policy and applying a fair price. That one which will not despise or kill the morally of the farmers. Rather the farmers should enjoy.

**Com. Domiziano Ratanya:** Thank you Jacton. Tutaenda kwa Paul Malenye Maina., hakuna Paul, hayuko Karibu. Anaingia?

**Audience:** Anaingie

**Com. Domiziano Ratanya:** Wengi hawataki kukaa hapa mpaka usiku. Kwa hivyo Paul Marenye Maina, sasa ni wakati wako na usisome memorandu, mhakuna wakati. Umepewa dakika tano just hightlight the main points. Five minutes only.

**Paul Maina:** Thank you bwana Comissioners. Nimekuwa mmoja wa wale ambao wamekuwa wakiongoza elimu ya Katiba katika eneo hili. Na nitawakilisha memorandum yangu baadaye.

**Com. Domiziano Ratanya:** Say your name,

**Paul Maina**: Paul Malenye Maina. Kuhuzu Katiba ningesema tungehitajika tuwe na utangulizi na huu uatangulizi una ndani yake kuwe na hstoria ya watu wa Kenya vile tumekuja mpaka penye tumefikia na pia tuwe na vision ambayo ni ya kutengeneza Katiba. Taifa ambalo ni more united.

Na pia katika directive of principles pia tunge-include sisi ni watu ambao tunamcha Mungu na pia tungeomba katika Katiba yetu, maneno yaliyo katika our National Anthem, haki iwe ngao na mlinzi pia yawe yanatuongoza katika Katiba mpya.

Pia ningependa kuzumzia uraia. Ningeomba mtu yeyote ambaye anazaliwa na wazazi ambao ni Wakenya apate uraia. Na pia kuwe na vile vitu ambayo vinatambulisha mtu ka raia. Kitabulisho na birth cerficate. Na zipeanwe karibu na watu.

Ningependa pia kuzungumzia kidogo kuhuzu utawala au uongozi. Tungependa uongozi au serikali ambayo ina undwa na vyama vyote ama coalition government.

Pia ningependa kuzungumzia kuhuzu haki za binadamu. Ambapo ningesema kaa vile zilivyo katika Katiba yetu ilivyo sasa, pengine tungeoza tu, sehemu za watoto na wamama. Iwekwe katika Katiba hiyo na walemavu pia walindwe kabisa.

N apia ningezumzia Commissions ambazo tungehitaji katika Katiba ijao,hasa tukitengeneza hii Katiba tungehitaji Commissions ambazo sitaongoza maisha yetu na serikali yetu. Nikianzia na Commission ambayo tuko nayo sasa ya Katiba, tungeomba

iendelee kubaki ili ituongoze katika kuelewa na kuishi kwenye Katiba hiyo.

Pia ningeuliza tuwe na Commission ya kuangali hali ya mashamba na utumizi wa mashamba. Tuwe na Commsission pia ya kuangalia haki za binadamu. Tuwe na Commission ya kuangalia haki za binadamu. Tanajua tumeishi, tumekosa kuishi hata kinyume na katiba ambayo tuko nayo sasa. Na sasa hivi kuweza kurejea, tunajua watu wetu wasinakia haki zao simekuwa violated. Kwa hivyo tungeomba hiyo Commission itusaidie kurejea kuishi kikatiba kulingana vile tutakavyo kubaliyana.

Ya mwisho mwana Commissioners ningependa pia kuzungumzia kuhuzu mazingira. Mazingara tungenomba zote wananchi wa Kenya tuhuzike katika kulinda mazingira. Mashamba yote katika Commission hiyo ya mashamba pia iangalie yale mashamba ambayo hayatumiki, tuweze kupanda mti na tuweze kuilinda sisi wenyewe. Asanteni.

**Copm.Domiziano Ratanya:** Okey asante sana Bwana Paul, kbala sijaita mtu mwingine, ningetaka kuwajulisha kwamba Commissioner mwenzangu hapa Com. Riunga Raiji atatuwacha kidogo kwa sababu anaenda kuangalia mambo mengine ya muhimu. Na kwa hivyo mkiona hayuko hapa, ni kazi ya muhimu anaenda kuangalia na si kutoroka. Kwa hivyo tuendele sasa Commissioner Raiji ataenda wakati wowote kutoka sasa. Twende kwa Peter Mkinya. Peter Mkinya? Ninaona Peter hayuko. Michael Njuguna.

**Michael Njuguna:** Kwa majina ni Michael Njuguna Mugwe. Na nina mambo kadha ambayo ninataka kusema juu ya Elimu kwa sababu elimu imekuwa kitu ambacho kinakarimu pesa nyingi ama mambo mengi.

Kwa kawaida sisi ambao ni wazazi tunaadhika kwa sababu muongozo kwa sababu muongozo wa elimu unafanyiwa mabadiliko leo na Kesho na tunaadhirika kunua vitabu kwa sababu hicho kitabu cha mwongozo ambacho kinaitwa syllabus serikali haizingatihi ama idara ambayo inahusika haizingatii kulingana na matakwa yake.

Ya pili ni hali ya ulinzi, kwa sababu ulinzi umekuwa hapa na sikusema ni hapa ni kwa sababu wanao usika hawasingatii ama hawangali matakwa ya kazi yao. Kwa sababu utaona, mtu akiwa hapa na mwingine pale na kuna jambo linateteneka hapa mbaya na wanao usika ama walinzi wakitwa wanakawia. Kwa hivyo tunataka kuzungumzia hali ya ulinzi ili tuwe huru kwa kila jambo.

Tena la tatu ni hali ya utabibu. Tukiangalia katika ma-hospitali zetu tunaona mambo yamekuwa mabaya sana kwa sababu hii inayoitwa cost sharing. Inaleta mambo mengi jungu nzima kwa sababu mtu akiwa mkonjwa hapati dawa kulingana na ugonjwa wake. Anaitishwa hiki na hiki na hizo zote ni pesa. Kwa hivyo ama ninapendekeza serikali ichugue jukumu la kuangalia kila wizara inafanya kitu gani.

Tena tuangalie upande wa utawala. Ningependelea ama ningependekeza utawala tuondolewe ama tuondoe utawala kutoka

kwa DC, DO tuwaje tu Ma-Chief na manaibu wao na wanao usika wazee wa kijiji na mkuu wa mkoa. Kwa sababu bwana chief an wengineo ndio wanatujua sana. Tunachukua muda mkubwa kuona bwana DC ama DO sisi wenyewe. Na nikisema hivyo wakaaji wa hapa wanauhakika kwa maana tunawajua tu Ma-Chiefs ambo tukonao hapa.

**Com. Domiziano Ratanaya:** Sasa jaribu kumaliza Michael. Wengi wanangoja.

**Michael Njuguna:** Tena ningependekeza kusiwe na harambe ya lazima kwa sababu tunahadhiriwa. Ikiwa mtu hana pesa anahadhiriwa na kuambiwa leta hiki kwa sababu ni harambee. Kwa hivyo ningependekeza tusiwe na harambe ya lazima. Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okay asante Michael Njuguna Mukuwe. Nitaenda kwa Pual Kamau. Tutaenda kwa Paul Kamau kama hayuko Benard Kihara.

**Beanard Kihara:** Haya asante sana. Kwa vile nimepata nafasi hii kuzungumzia kidogo. Mimi sina mengi ni kidigo lakini yenywe siju kama itaonekana ni muhimu. Yale maneno yote ambayo imezungumzwa tangu nifikehapa, yote yako kwa sheria na iko kwa Katiba. Lakini haifatwi. Kwa hivyo ile Katiba tunataka kutengeneza au ile inaelekea kutengenezwa wakati huu, tafadhalini ifuatwe. Kwa sababu hata kama ile iko ingefuatwa hatungekuwa na shida ile ambayo iko. Kwa sababu shida tunayo ni nyingi kwa sababu sheria haifuatwi. Kwa haivyo hata ungetengenezwa mpya na haifatwi, itakuwa ni kazi. Kwa hivyo ninaomba ile ambayo itatengenezwa ifuatwe vizuri na itakuwa mzuri na itakuwa ya muelekeo mzuri. Kwa Kenya yetu. Na mimi nafikisha hapo.

**Com. Domiziano Ratanya**: Asante sana. Pastor Peter Musila. Ni wewe sasa. Sema majina yako Peter.

**Pator. Peter Ngurio Musila:** Maoni ni kuhuzu kikundi ambacho ninaogoza katika upande wa kikanisa.

Ya kwanza, tumeonelea kuwa mtu akiwa na uwezo wa kifedha, wa kuweza kuleta maendeleo na kujenga barabara ama dam, asije akakatashwa.

Ya pili, ndani ya katiba tuwe na kifungu ambacho litalinda uzao wa nchi hii. Mtu ambaye hajafikisha umri wa miaka thelathini na mitano hasiruuziwe kukunya pombe.

Tatu, kila division iwe na mbuge.

Nne, kila raia ambaye amfikisha miaka hamsini na tano na zaidi, imewapasa wasaidiwe. Kwa sababu siyo wote abao wamefanikiwa kimaisha.

Tano, Kenya ni nyumba, na Rais ni baba na mikoa ni wamama. Tumeonelea ya kuwa kila mama aweze kulinda watoto wake kwa kila njia ili waweze kuendelea klimaisha. Asante.

**Com Domiziano Ratanya:** Asante sana Pastor, kuna pastor mwingine anaitwa Geofrey Mwangi.. Huyo simuoni. Kuna Jackson Mosoini. Daniel Chemrom, Daniel Chemron, anakuja okay Samuel Rob atamfuata. Samuel Robo yuko karibu, okay Samuel kaa hapo.

**Daniel Chemron**: Jina langu ni Daniel Chemron Cheboi. Maoni yangu ni haya. Utozaji wa ushuru and licences, inasitahili kuangalia ama ingalie hali ya mahali, kwa sababu mahali pengine ni makavu na kwingine kuna mabado mazuri lakini na sehemu kuna mabado wale walio na shida na mabado mabaya, wanakuwa na shida ya kulipa uhuru.

Ya pili ni vifaa muhimu kwa mwanadamu wa kawaida, inasitahili kusimamiwa na serikali. Kwa mfano mazao ya shamba kama mahindi na pia na maziwa.

Ya tatu ni elimu, shule za secondary sinasitahili kusimamiwa na almashauri ya wazazi yaani PTA, baadala ya BOG, kwa sababu PTA wako na watoto saidi na ndio watu wa sehemu mbali.

Ya nne ni kwamba, there should ber, bahadhi ya hii Katiba, inasitahili kuwe na wakati ama kuwe na elimu kila wakati ya kuelimisha watu mahali pale. Tuseme in locational level.

Ya tano ni kwamba, serikali ya mitaa ama local government, isimamie mashule yote katika miradi mbali mbali. Kwamba mfano ujenzi ya madaraza na maendeleo katika shule.

Ya sita ni kwamba, kuhuzu maendeleo ya mtaa ama location, inasitahili wenyeji wapewe uwezo ama mamlaka ya kupanga maendeleo ambayo inasitahili kwao. Baadala ya jukumu lolote liwajiwe councillor. Hayo ni maoni yangu.

**Com. Domizaino Ratanya:** Okay asante sana Daniel. Nimwita Samueli Rob, Samuel Rob, alikuwa karibu? Okay huyu hayuko? John Chemron, kuna Daniel Chemron na John. Joel Chepkwony anamfuata.

**John Chemron:** Kwa jina majina kamili ni Johh Chemron, haya maoni ya ambayo ninaonelea ni hasa kwa upande wa ulinzi. Upande wa ulinzi siku hizi iko nchini sana. Sisemi kwa sababu ya kitaifa lakini hasa kwa local area. Tunaona iko chini sana na corruption imeingilia huko ndani sana.

Kwa upande wa biashara tunaona soko huru, nafikiria wengine walikuwa wamezungumza kuhuzu hiyo sana, hiyo ndiyo wameweka raia wema katika umasikini sana. Na kwa uaria bibi asiruhusiwe ama kuja ku-register mtu au bwana kutoka nje.

Lakini bwana anaweza kuregister kuwa raia bibi.

Alafu katika afya, upande wa cost sharering ambaye tuko nayo katika Ministry, hiyo Bado imetuletea umasikini kwa sababu watu wanaumia sana kwa kupata matibabu. Kwa sababu kuna wengine ambao hawana chochote na anaweza hata kubaki bila kutibiwa.

**Com. Domiziano Ratanya**: Okey asante sana. Kuna swali moja, ngoja.

**Com. Salome Mugai:** John Chemron umetueleza kuwa Mkenya mwaume anweza kuja kuandikisha bibi yake akawa mwanakenya. Lakini siyo mama amuleta bwanayake amuandikishe kama raia wa Kenya. Ungetupa sababu zako tafadhali. Kwa nini hiyo ubaguzi ?

**John Chemron:** Kwa sababu bwana yuko na uraia ambao uko mzito kidogo, kwa hivyo tukiamua, hawa watasidi, watu watachukua nafasi hiyo kutoka nje wakuwe tu wakiingia ndani kwasababu wanajua watakuwa registered kuwa raia kirahisi sana. Kwa hivyo mimi ninaonelea hapo si mzuri sana.

**Com. Salome Muigai:** Mimi na wewe tukiwa hivi, wewe ni kakangu na mimi ni dadako, kwa nini uraia wako unakuwa mzito kuliko wangu.

**John Chemron:** Kwa sababu hapa ni nyumbani**.**

**Com. Salome Muigai**: Na mimi?

**John Chemron**: Mimi ninasema hivyo kwa sababu tuki-encourage hiyo, tutapata nafasi ya akina mama walete watu kutoka nje sana. Kwa sababu atasema tuko sawa na utakuwa raia mwema huku nyumbani.

**Com. Salome Muigai:** Lakini akina baba wanata watu, hiyo ndiyo sielewe tofauti gani iko hapo. Wewe unaleta watu ikiwa watu wenye unaleta niwakike, na mimi nileta watu wenye ninaleta niwa kiume, tofauti hiyo inakuwa wapi, ndio yenye sielewi tafadhali. Kikatiba, unajua Katiba ni wakati wa kusawawisha. Playing ground. Nieleze nielewe, I don't want to debate with you, lakini nataka kukuelewa tafadhali.

**John Chemron**: Hiyo tu nimesema tu kwa sababu ya ku-encourage, watakuwa encouraged kabisa. akina mama kuleta watu kutoka nje sana.

**Com. Domiziano Ratanya:** Hapo Bwana John pengine tunataka kusema kama bwana ni wa hapa, Mkenya, na bibi ni

mzungu, unasema namahivyo? Sasa bwana abaye ni Mkenya saidie bibi yake ambaye ni mzungu kuwa raia? Unamanisha hivyo?

**John Chemron:** Yes

**Com. Domiziano Ratanya**: Ni namna hivyo ulikuwa unasema, si kupendekeza lakini ni kwa kufafanua ni namna hivyo?

**Com. Salome Muigai:** Kwa nini sisi wenyewe nami nije na bwana yangu Mzungu pia awe mwana Kenya? Hiyo ndio ile haki sielewe tofauti yake.

**Com. Domiziano Ratanya:** Kwa hivyo kama msichana ni wa hapa, kama msichana ni Mkenya, naweza naye kwenda kuandikisha bwana yake ambaye ni mwingereza hapa kuwa citizen? Anaweza?

**Com. Salome Muigai**: John anakata.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay ni maoni yako hiyo, tulikuwa tunataka kuelewa lakini asante sana. Muigai Kuria,

Muigai Kuria, unajua tunataka maoni ya kusaidia kutengeneza Katiba ywetu mpya. Kurekebisha, kwa hivyo tuambie maoni yako kwa njia nzuri ambayo tutaelewa. Mapendekezo.

**Muigai Kuria;** Jina langu ni Muigai Kuria. Na maoni yangu, hospitali zetu hapa mashambani hasitengenezwi vile vilivyo. Yaani kuhutumiwa. Kwa sababu huwa hazina dawa kila wakati.

**Com. Domiziano Ratanya**: Kwa hivyo unapendekeza nini?

**Muigai Kuria:** Ninapendekeza siwe na dawa kila wakati.

**Com. Domiziano Ratanya:** Ndio sema namna hivyo.

**Muigai Kuria:** Siwe na dawa kila wakati, kwa sababu ukienda kwa hospitali unambiwa utoe pesa ili ununue kati. Inaandikwa jina lako na ugonjwa uliyo na nayo na mara ya mwisho unaambiwa hakuna dawa uende ukanunua katika Chemist. Na hii hospitali ni ya serikali.

**Com. Domiziano Ratanya:** Hiyo tumeelewa.

**Muigai Kuria:** Na tena tungetaka serikali iwe ikiutumia watu wa mashambani kulingana na mimea yao. Mahindi, maziwa na ng'ombe. Ukiwa na ng'ombe nyingi na unataka kuhuza, hakuna mahali ya kupeleka kwa sababu hiyo KMC ilimalizika na KCC ya maziwa pia. Serikali haishughuliki nayo. Kwa hivyo ishughulike nayo.

Ya tatu, tupatiwe uongozi mwema kati ya wanadamu. Kusiwe na ubaguzi kwa makabila yote ya Kenya.

Na ya nne tuwe na Raisi mwenyewe akiwa anasimamia ufisadi, usiendelee mahali anaongoza. Kwa sababu ufisadi umendelea sana katika Kenya. Na tena tuwe kuanzia Rais, Wabunge wote, wawe na serikali ya kudumu isiyo na uchojezi baina ya watu wote walio Kenya. Kwa sababu uchochezi ndio unaharibu Kenya yote nzima.

**Com. Domiziano Ratanya**: Fanya haraka wakati wako umeisha.

**Muigai Kuria:** Serikali ya sasa isema Bunge iongeswe muda. Mimi ninapendekeza isiongeswe hata kidogo. Nimemaliza.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay asante sana kwa maoni yako Muigai. Sasa tutaenda kwa Julius Arap Rono. Julius hayuko. Syvanus Khayenga.

**Syvanus Khayega Kusijiru:** Maoni yangu ni kama ifatavyo. Katiba mpya nina pendekeza tupate introduction kwa hiyo Katiba kwa sabab ya leo haina very good introduction.

Kuhusu Rais, tunataka Rais ambaye awe kati ya umri wa miaka thelathini tano hadi sabini na tano. Iasiwe tu tumeajia age inakuwa mpaka miamoja na kitu. Tena awe mtu morally upright na wakati wakujakuliwa awe na kura zaidi ya hamsini na moja. Tuondoe hii ya simple majority ambayo ni twety five in five Provinces. Hiyo haifai. Mtu akiwa na 51% atakuwa amepata kura za kutosha kutoka taifa nzima.

Na tena wakati wa uchaguzi wa Rais na Parliament na civic, siwe tarehe tofauti. Tusiwe tu na tarehe moja zote tunafanya tarehe moja hapana, kwa sababu hiyo inaleta irregularities. Pia ninapendekeza kura siezabiwe kituoni ama kupelekw mahali pengine, to avoid riging. Elections sifanywe na ECK na ECK iwe independent kwa sababu sasa ninaona ECK si independent lazima wagoje amri kutoka mahali fulani. Na tuwe na pia runoff wakati wa uchaguzi. Tusiwe ati mtu akipata 35% kwa sababu ameshida, hiyo simple majority, tuna-declare President ama winner. Tuwe na run-off after two weeks tupate uchaguzi mwingine.

Viongozi wetu wawe watu wakuheshimiwa kabisa. Yaani high integrity. Wakati huu tuna viongozi ambao wamehusika na ufisadi na mambo mengi machafu lakini bado wanatuongoza. Lakini katika katiba mpya, ninataka mtu awe morally upright. Na kila kitu kiwe kizuri kwake. Tuwe pia na na uwezo wa kuita wale wabunge wale wanapotelea kule Nairobi. Tuwe na ile

power to recall.

Na tena ni kushangaza ya kwamba muhajiriwa anaenda kuamrisha ni pwsa ngapi atapata. Kwa hivyo tusiwe wabunge wanajiamlia mishahara yao. Tuwe na Commission ingine kado ambayo ita-regulate ama itangalia mambo ya mishahara ya Wabunge.

Tunaona wakati huu bunge haina uwezo sana lazima bunge ya leo inasikiza kutoka kwa Executive. Executive iko na nguvu zaidi kuliko bunge. Kwa hivyo tunataka Buge ambao itakuja iwe na nguvu zaidi.

Vyama vya kisiasa nasema ni vingi sana, arobaini na kitu ni saidi. Napendekeza vya viwe vine tu. Na viwe na uwezo na viziwe vya kikabila ama visiwe vya dini fulani. Visilemee upande wowote. Na viongozi wao pia wachaguliwe watu wa elimu wale wameelimika, vizuri na pia morals zao ziwe za standard.

Tunataka equall funding for all parties na tena pia Radio na Television ya Kenya KBC iwapatie muda wa kutosha. Kwa sababu wa leo tunaona tu chama kimoja ndicho kinawakilishwa kwa KBC.

Okay asante sana nilikuwa na mengi .

**Com. Domiziano Ratanya**: Sasa wananchi ningetaka kuwankumbusha ya kwamba kwa sababu sasa tumefika saa nane ama pengine imebakia dakika hivi, saa yangu inasema ni saa nane. Na tunaona tuna watu wengi sana ambao wanangoja karibu sabini. Na tunataka kila mtu kila mtu aseme kitu. Kwa hivyo nitawaonya masaa.

Badala ya wengine kwenda bila kusema kuwe na dakika chache ya kusema ili kila mtu aseme kitu. Hiyo si ni sawa sawa.? Na mengi kutok sasa yamesemwa, hatutaki sana watu warudie yale yamesemwa ya elimu ya nini, uje kutoka sasa uje na yale ya muhimu ambayao hayakutajwa. Na nimebungua dakika sasa zimekuwa tatu. Ili kukifika jioni tuwe kila mtu amesema kitu. Na tena tusiende nyumbani usiku. Ninajua wengi wanaenda mbali sana.

Tumekubaliana hapo wananchi? Kwa hivyo ukiambiwa wakati wako umekwisha, heshimu hiyo kwa sababu tunaeshimu hapa kila mtu. Na tungetaka hiyo amri mpya na David Muriuki Mwangi. Dakika hiyo tatu. Sema hayo ya muhimu. David Muriuki Mwangi. Ni wakati wako, yuko hapa? Okay kama hayuko, Ezekia Ndikiriki hata huyo naona hayuko. Peter Gitau, hatumuoni, Kiptoo Job, Isaac M. Kagua, huyo ninaona no obsever. Daniel Wajira, Joseph Kamau, Philip Kamren. Kamren Alex, ni wewe? Okay Kamren Alex, ni wakati wako sasa na useme kwa ufupi, yale ya muhimu, dakika tatu.

**Kamren Alex:** Maoni yangu ni kama yafuatavyo, kwa vile Kenya Kiswahili ndicho lugha ya taifa, maoni yangu ninaonelea Wabuge pia katika Bunge mijadala iwe ikijadilwa kwa Kiswahili.

Kenya iwe na waziri mkuu na manaibu wawili na Rais asiye kuwa na kazi au mamulaka mengi. Kuwe na uhuru wa kuabudu lakini makanisa yawe yakichunguzwa kabla ya kusajiriwa ili kuzuia mengine yanayo hatarisha maisha ya wana nchi.

Uchaguzi uwe ukifanyika kila baada ya miaka mitano kama ilivyokuwa. Wakuu wa mikoa mabalozi na makatibu wakuu wa wizara mbali mbali wawe wakichaguliwa na raia………….

**Com. Salome Muigai**: Peter Mbuthia? Peter Mbuthia? na mimi ni mwalimu na unasema present Madam ndio najua uko.

**Peter Mbuthia:** Yangu ni haya tu matatu. Jina langu ni Peter Mbuthia Githu

**Com. Salome Muigai:** Tafadhali tungekuwa na mkutano mmoja ndio tusikilizane. Asante.

**Peter Mbuthia:** Yangu mengi yamezungumzwa hapa lakini ninataka kuhuliza sisi hapa Kenya, mtu akiwa na miaka kumi na nane inatakikana awe na kitambulisho. Sasa hapa kuna hii habari ya kuoana, kwa nini tusiwe na Katiba ya kuona. Kwa sababu msichana ama kijana akimaliza shule anaenda kuolewa.

**Com. Salome Muigai:** Unataka kupendekeza waoane wakiwa na miaka mingapi?

**Peter Mbuthia:** Kuanzia miaka ishirini hapo.

**Com. Salome Muigai:** Ishirini wote wafulana na wasichana.

**Peter Mbuthia:** Msichana awe na mika ishirini na tano hapo. Habari ya ukimwi, umeleta matatizo makubwa sana, maanake watu wengi wanakufa. Sasa kwa nini dadangu ameolewa na wakati Babake anapata ukimwi, Bwanake anamrudisha kwa wazazi wake? Na wale watoto alikuwa amepata naye hiyo ni gharama tena kwangu.

La mwisho ni juu ya upatanishaji wa Ministry na reshuffle ambayo inatakiwa kuwe na kiwango fulani cha muda ambapo Minister fulani anakaa hapo kama mwaka moja ama pili hivi halafu unabaDilisha.

Ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana Bwana Mbuthia, Paul Chechuru. Na ninataka kujua wakina mama wenye wanataka kuzungumza. Baada ya Paul Gichuru nitawapa nafasi ya kuzungumza. Paul Gichuru. Shadrack Mwangi, Shadrack? Patrick Mwaura? John Cheserem, wa Box 169 Subukia. John Nyoro, Geofrey Kimani.

**Geofrey Kimani:** Jina ni Geofrey Kimani. Maoni yangu ni kuhuzu Inchi yetu. Tungetaka elections should be done as in the Constitution after five years, nor prolonging time.

Constitution should be taught to all Kenyans fully. Police torture should be stopped.

Education be provided freely. Primary and Secondary, after the education, employment or any national building should be care of.

Medical attention should be provided freely by the Government, cost sharing should be stopped.

Political parties should be provided with finance equally to look upon problems of the Constituion. All political parties should treated with equal representation. Eg Security. Political parties should limited as to three political parties and when they are financed should keep account books.

President shouldn't be above the law and can be Prosecuted if he commits an offence.

Abortion should be an offence and one should be jailed for two years unless for health of the mother.

Employment should be given to every body. If a person does not have employment should have any activity and the government should look upon that.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana nina swali moja kwako. Umesema abortion ama utoaji mimba usiwe wa halali na mwenye kutoa afungwe miaka miwili, ni yule tu mama mwenye kubeba mimba ama yule baba mwenye kusema sijui na sitaki kujua pia yeye afungwe, ama ni mama pekee yake.

**Geoffrey Kimani:** The mother is the bearer of the whole thing. So she should be convicted.

**Com. Salome Muigai:** But it take two to make a baby, so by the time one person says I don't want to know, they are already aborting the half of the foetus? Unajua uzuri wa Katiba ni wakati wa Kihodo. Sasa unaonaje hiyo mambo.

**Geoffrey Kimani:** May be a man they had talked about the love making, may be the woman was but getting money from the man,

**Com. Salome Muigai:** Does it matter he made a baby. Na yeye ni baba wa yule mtoto.

**Geoffrey Kimani**: And that chid has the right to live.

**Com. Salome Muigai:** And tha father has a responsibility.

**Geoffrey Kimani:** Then the father should be taken to the court and should take care of the baby.

**Com. Salome Muigai**: Now you are making a Katiba yenye inalinda masilahi ya baba na ya mama na ya mtoto wa Kenya. That was Joseph Kimani. Can I have Florence Njeri sasa.

**Florence Njeri:** Kwa majina ni Florence Wainaina. Maoni yangu ningetaka kunaina aina mbili ya Title Deed hapa Kenya. Sisi zote tupewe aina moja.

**Com. Salome Muigai**: Gani?

**Florence Njeri:** Ya maisha. Mama apewe mamlaka ya kutawala mali ya mumewe akifa. Isiwe ni watoto wanatawala. Tupate elimu ya bure kutoka shule za malezi. Tupate elimu ya bure kutoka elimu ya malezi hadi shule za secondary.

Serikali itayarishe pesa za malipo za uzeeni kabla ya mtu kwenda retire. Tusiletewe chakula kutoka inje iwepo tu kuna njaa.

Mbuge akichaguliwa akose kuhudumia wananchi tupewe nafasi ya kuchagua mwingine, hata councillor.

Vijana ambao wantunga wasichana mimba na kuwawachilia, serikali iwafuate na kulea hao watoto.

Wazee waache kunywa pombe na vijana. Ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai:** Grace Wanjiru.

**Grace Wajiru:** Njetaguo Grace Wanjri Kimani**.**
**Translator:** Anaitwa Grace Wajiru Kimani.
**Grace Wanjiru:** Kwendaga kwario ohoro wa gothokio kwa mtitu**.**
**Translator:** Nataka kuongea kuhuzu masingira na hali ya kuharibiwa kwa msitu.
**Grace Wanjiru:** Tondu ciana, mawera ne magete.
**Translator:** Kwa sababu watoto wetu wamekosa nafasi ya kazi mahali hapa kame.
**Grace Wajiru:** Koru Thirikari ya cokia wira forest toria korare mbere**.**

**Translator:** na kama serikali ingerudisha kazi katika forest kama vile ilivyokuwa zamani

**Grace Wanjiru:** Na cia caiana citu ciandekuo kuo forest kohandaga mti, na gotukata mtitu.

**Translator**: Basi na watoto wetu wahajiriwe kutunza yaani kulinda forest na kazi zingine za forest.

**Grace Wanjiru:** Borori no wagere tondu ohoro wa gothukakia no uthire.

**Translator:** Na hata nikaona mti inaweza kuwa nzuri na hata hali ya uharibifu wa mti sasa itaweza kuwa imekwisha.

**Grace Wanjiru:** Wa keri**.**

**Translator**: Jambo la pili

**Grace Wajiru:** Ohoro wa kohoia Ngai wekerero makeria tondu neguo ongehota goturia boruri.

**Translator**: Na sasa habari ya kuabudu Mungu sasa itiliwe maanani sana maana hiyo inaweza kuifadhi hali ya nchi yetu.

**Grace Wajiru:** Oguo maheuo weyadhi we kohuo ne getha bororі ogea na hinya**.**

**Translator**: Kwa hivyo wapewe uhuru wa kuabudu ili nchi yetu iwe na nguvu.

**Grace Wanjiru:** Wa gatatu

**Translator**: Jambo la tatu

**Grace Wanjiru:** Tuwethutha muno tondu ona barabara tutire**.**

**Translator:** Ni hali ya hapa kwetu lowe Subukia, kwa ajili hatuna barabara,

**Grace Wanjiru**: Mbura ya ura tukorago na thina muno tondu ona ngari itikinyaga.

**Translator**: Yaani mvua inaponyesha magari hasiwezi kufika hapa kwetu.

**Grace Wanjiru:** Oguo tukahoua Thirikari ituthondekere bara bara neguo tukahoto gutethika.

**Translator:** Yaani kwa hivyo serikali iweze kuangalia pale ili kiangazi inapoingia serikali iweze kutusaidia katika hali ya njaa.

**Grace Wanjiru:** Oria Onge ne wa cukuru**.**

**Translator:** Jambo lingine ni la shule

**Grace Wanjiru:** Thirikari ithi na mbere agetutethagia ohoro wa cukuru**.**

**Translator:** Yaani serikali iendelee kutusaidia kuhuzu hali ya shule,

**Grace Wanjiru:** Tondu goku ne gwathina muno tutegemagera okurima tu.

**Translator:** Maana hapa kwetu na sehemu zingine tunategemea hali ya kilimo tu.

**Grace Wanjiru:** Na hende iria riuo riara tutiyonaga kendu tukuo tutwere cukuru ne getha ciana ithome.

**Translator:** Na wakati jua inapowaka, hatuna kitu kingine cha kupeleka shuleni ili watoto waweze kusoma.

**Grace Wanjiru:** Oguo Thirikari angetutethia no tuone tutethikete**.**

**Translator:** Kwa hivyo serkali ikitusaidia kwa upande huo tutaweza kuwa tumefaidika kweli.

**Grace Wanjiru:** Mwana hendi iria angerituhero ne maundu athiyaga kuri ithi na nyina**.**

**Translator**: Maana mtoto mambo yanapo kuwa mgumu anaenda kwa baba na mama,

**Grace Wanjiru:** Na uguo Thirikari neuo mathi maitu.

**Translator:** na kwa hivyo sasa serikali ndio baba na mama wetu.

**Grace Wanjiru**: Ohoro oria onge ne wa mai.

**Translator:** Habari zingine ni kuhuzu maji.

**Grace Wajiru:** Tugerega mai kondu na guku kianda.

**Translator:** Yaani kwetu ni huko upande wa juu na maji tunaenda kuchota huko chini.

**Grace Wanjiru:** Oguo Thirikari engetohe mai no tukene muno.

**Translator:** Kwa hivyo serikali inapotusaidia hapo lower Subukia kuhuzu maji tunaweza kushukuru sana.

**Grace Wanjiru:** Ndigothiyaga na mbere kugaga oro'oguo.

**Translator:** Kwa hivyo maoni yangu ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai**: Asanate sana, Monicah Wairimu.

**Monica Wairimu:** Nderenda kwaria ohoro wa muthuri ahiketie mtumia.

**Translator:** Ananena juu ya mume akioa mwanamke.

**Monica Wairimu:** Maganere na ciana iria menacio gotigatweke muthuri ocia ona thina ne'arigeyaga indo ciake.

**Translator:** Atosheke na watoto ambao amezaa ndani ya nyumba lakini isiwe kwamba ana watoto wengine ambao watakuja kurithi mali yake.

**Monica Wairimu:** Ndiri no ondu onge**.**

**Translator:** Ni hiyo pekee yake.

**Com. Salome Muigai**: Nina swali kwako mama, hawa watoto wenye wanataka hiyo urithi ni wa huyu mzee?

**Monica Wairimu:** Aca ndinge'yenda ne umaraya ocio.

**Com. Salome Muigai:** Lakini mama mzee mwenye kulea mtoto, yeye ndiye anajua pahali gani amezaa mtoto na pahali penye amezaa. Unasema hawa watoto ndio wanthi?

**Monica Wairimu:** Aca ndingeyenda ne umaraya ndamuheketie

**Com. Salome Mugai:** Kwa hivyo hawajulikani ni nani? Mzee mwenye kuwazaa anawajua na ndiye mwenye mali?

**Monica Wairimu**: Ndamuheketie

**Translator:** Hajamuoa.

**Monica Wairimu**: Mtumia atahekete akareho muci ocio onge ne umaraya**.**

**Translator:** Na hajamuleta nyumbani, lakini huyu ameletwa.

**Com. Salome Muigai** : Haya mama, kama wewe ungekuwa mmoja wa hawa watoto wenye wamezaliwa kule, ungetaka baba yako akupe usrithi wako mahali hapo?

**Com. Salome Muigai:** Lakini watoto wenye kuzaliwa hapo?

**Monica Wairimu:** Matigeciareruo oumarayani**.**

**Translator**: Wamezaliwa katika umalaya

**Com. Salome Muigai**: Kwa hivyo huyo mtoto hana haki,

**Monica Wairimu:** Ndari na ma**.**

**Translator:** Hawana haki

**Com. Salome Muigai**: Una watoto wasichana.

**Monica Wairimu:** Yee

**Com. SalomeMuigai**: Jina Langu ni Lucy Mwangi.

**Lucy Mwangi:** Maoni ya kwanza ni kuhuzu budget. Lugha ya taifa kwa Wanakenya ni Kiswahili. Ni vizuri kila kitu ambacho kinatangazwa kwa wananchi inafa kutangazwa kutumia lugha ya kiwahili, ili kuona kila Mkenya ameelewa kinaendelea.

Kuhuzu wanfunzi ambo wamemaliza shule. Katika eneo letu, tunaweza kuwaona vijana wengi ambao wamesoma lakini elimu imepuhuzwa. Tunapendekeza ni vyema kama mwanafunzi akiwa shule achague kitu ambacho kinaweza kumsimamia kama vile kuchagua course fulani ambayo baada ya masomo atapata kazi.

Wizara zote kote nchini zifanye kazi bila kuingiliwa kisiasa na mtu yeyote.

**Com. Salome Muigai:** Mimi nina swali moja kwako asante sana kwa maoni yako, Lucy Mwangi. Wewe ndiye msichana mwenye tumeona huku wa miaka kidogo. Je kuhuzu hii Katiba, ungewasimamia aje wasichana wa rika yako, kuna mambo gani yenye ikingefanyika ili hii Katiba iwe ni Katiba yenye imesimamia mama wakimo wa kimo kama chako.

**Lucy Mwangi**: Ningependa pengine kama Katiba ingependa isimamie wasichana especially kama mimi kwa kuwaajiri kazi. Wengi ambao wameliza shule na wamekaa tu na kuolewa direct. Kama wangepata kazi, ni vizuri.

**Com. Salome Muigai**: Anything else.

**Lucy Mwangi**: No.

**Com. Salome Muigai:** Asante Zacharia Njoroge. Zacaharia Njoroge? Harron Wairobi.

**Harron Wairobi:** Kwa majina ni Harroni Wairobi. Yangu ni kuhuzu masingira yetu. Kwa sababu ninaona tunaumiya sana kwa sababu ya wale wakuu wa kuu wa kwanza kutoka wakati wa hayati. Walichukua mashamba makubwa ya wazungu kwa sababu raia haina ma-society. Halafu mazingira yetu yamearibika kwa sababu wamekawa forest kwa raia wenyewe hawana mashamba.

**Com. Salome Muigai :** Ungetaka kupendekeza kitu gani?

**Harron Wairobi:** Napendekeza mashamba ya serikali isiingiliwe. Kwa sababu sisi tutakosa maji. Na mti itaisha kwenye msitu. Kwa sababu yule mwenye alipata hili shamba hana ujuzi wa kupanda mti mingine.

Kwa hayo mimi sina mengi.

**Com. Salome Muigai:** Z.M. Kimingi.

**Zachari M. Kimingi:** Kwa majina ni Zachari M. Kimingi. Kwanza ningetaka Vice President awe anachaguliwa na Parliament.

Ya pili ningetaka watu wote wa Kenya wawe na medical services ikiwa ni free. Wapewe free medical services.

Pia ningetaka upande wa elimu, ningetaka Primary education iwe ni free na compulsory.

Tatu, ningetaka muhula wa President uwe ni miaka minne badaala ya mitano. Na iwe ni mara pili, two terms.

Hiyo ingine ningetaka top Government posts siwe sinakuwa approved by the Parliament. President awe na nafasi ya kutoa wale angetaka na lakini Parliament to approve.

Na hiyo ingine ningetaka votes, wakati wa elections, zile votes, kulw tunapkia kura, tunaesabia pale pale. Pia ningetaka vyama viwe tatu. Hata siyo nine. Ziwe tatu, maximum ya three.

Pia ningetaka Constituency iwe inakuwa determined by population ya that particular constituency. Si area ya hectarege na

square kilometers, lakini iwe ni population yenyewe to determine the Constituency.

Na ningetaka mambo ya marriage na kesi ya mashamba yote iachiwe village elders. Yaani elders to decide.

Na MP's na Councillors wale ambao wanashindwa na kazi yao, pawe na nafazi ya kuwaondoa kutoka kazini kwa sababu wameshindwa na kazi yao.

Tuna wale ambao mashamba imekuwa too much. Serikali inunue mashamba hao halafu iwape wale ambao ni landless. Wapakie na kitu kama fifity hectares.

Freedom of worship, iwe ni limit, hakuna devil worshiping in Kenya. Tukatae hiyo kabisa. Nafikiri waja niachie hayo tu.

**Com. Salome Muigai:** Nina maswali mawili kwako. Ya kwanza ni hii ya land cases irudishwe kwa wazee. Akina mama wanatutetea sana wakati tunapoenda kusikiza maoni ya kila pahali akina mama wanasema, hii mashamba ikirudishwa kwa Wazee kwa ajili Wazee ni akina baba pekee yao. Wana wanawaonea. Hawasikii kama wanafanyiwa ukweli. Wewe amoni yako ingekuwa nini juu ya hiyo. Nina swali lingine, nina maswali mawili.

Swali hilo la pili ni kuwa umesema kuwa tuangalie jumla ya watu ndio tutengeneza kikao cha Bunge. Na kuna watu wengine wenye wanakaa pengine wengine juu ya mlima na wengine chini, teremi ya pahali inakuwa ni mbali na ni teremi ngumu kabisa, hao pia unataka tufanye nao nini na hao pia ni Wakenya?

**Zachari M. Kimingi:** Kwanza hii ya land case. Tunajumhisha akina mama in that committee. Hiyo ita-bring fairness.

Haya hii ingine ya pili, one of the factors iwe ni population, ikiwa ni geography, tutaangalia kweli, lakini sanasana tuangali population. Sijui kama nimejibu.

**Com. Salome Muigai**: Umejibu vile unaweza. Asante sana. Mureith Kariuki, Mureith Kariuki? Jackson Kithuku. Jackson una dakika zako tatu.

**Jackson M. Kithuku:** Nina mapendekezo yafuatayo.

1. Money should not bear portraits of different serving Heads of States. We should actually have the a portrait of the founder President alone like is the case with American Dollar.
1. Let have definite ministries which should be outline in our Constitution. These should not be charged for ever. I propose a maximum of fifiteen ministries.
1. For effective governance the country should have a Prime Minister and a President whose role will be mainly

ceremonial

1. Reduce the powers of the President, appointment of Minister should be vetted by Parliament after the President had nominated them.
1. The government should establish a welfare fund for all Kenyans to alleviate the problem of poverty.
1. The country particularly with the Aids pandemic which is claiming lives of many employed people they are living behind orphans and other dependants and we feel that if there was some kind of a welfare to take care of every body. At least even if they earn a salary of five hundred to one thousand, at least there will something. To take care of those people who are left behind.
1. The President should be made to attend Parliamentary sessions at least once a week, to answer crucial question about these running of the country
1. And lately, we should maintain the unitary system of government as it caters well for our local multy ethnic groups. Spread all over the country.

**Com. Salome Muigai:** Nina maswali mawali kwako. Umesema kuwa tumpate Waziri mkuu, kwa hivyo Waziri mkuu ndiye atakuwa mkubwa wa Serikali, na pia Uunasema President akileta Mawaziri, yaende Bunge, basi Waziri Mkuu itakuwa jukumu lake kuanzisha kuwateua hawa mawasiri lakini siyo Rais tena? Tena hata hilo jambo unasema Raisi aende kwenye Bunge siku moja aende kujieleza vile anavyofanya. Sasa mkuu wa serikali ni nani. Rais ama nani?

**Jackson M. kithuku:** Hiyo itatengemea na kama lile wazo litatiliwa maanani. Kam tutaendela na vile ilikuwa, ndio nilikuwa ninasema Rais aingie kwa Bunge.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana kwa maoni yako. Cherioyot Pokomo. Tarubo Kiptoo,Tarubo Kiptoo? Harrison Kamau.

**Harrison Kamau:** Presidential appointee………..interjection by Com. Salome Muigai.

**Com. Salome Muigai:** Anza kwa jina lako

**Harrison Kamau:** Presidential appointee be approved by the Parlaiment. The President should not be above the law.

- Speciall children be well cared for in a special unit in every zone.
- Elections of the vice Presidet should be done by the Mp's.
- Political Parties should be fund themselves.
- We should have a maximum of three parties.
- Street children should be catered for by the Government.
- Mayors be elected directly by the people.
- Civic education should be in school syllabus.

- All ministers should be graduates and be acquinted with their Ministries.
- Salaries be based on the value of work done not certificates.
- Cases in the court should have a limit. A case should not take a long time.
- The quality of a person should be considered during employment.
- A person appointed by the President should be fired with a good reason.
- The Constitution should be supreme
- Court fee should be very minimal
- Retrenches should be well compensated.
- Land take by the Government should be compensated.
- Indigenous language be taught in school

Thank you.

**Com. Salome Muigai:** Thank you very much, Mr Harrison Kamau. Dickson Chrichri, Dickson Chirchir. Kuria Ndirangu,Kuria Ndirangu? Charles Mihang' Nderitu. Johanna Mwiruri. Daniel Gichui, Francis Manyanji, Joaseph Wainaia, Richard Koech.

**Richard Koech:** Kwa jina ninaitwa Richard Koech Bundotich. Maoni yangu kuhuzu Katiba ya nchi hii, ni hivi, mapato ya kila sehemu, kama ni kutoka kwenye kilimo ama ama service zingine kama malipo ya ushuru, ziwe sikirudishwa kwa sehemu hiyo kwa maendeleo ya barabara, mahospitali na vitu zingine za public

Kuhuzu security, Kenay hii kwa maoni yangu, nikependelea, kila watu watatu, kuwe na askari wa usalama.

Ya tatu ni kuhuzu watoto, watoto Kenya hii kwa maoni yangu wangepewa masomo ya bure. Na Serikali itilie maanani zaidi mpaka daraza la nane. Pia wapewe matibabu bure.

Ya nne, ni kuhuzu changaa, droughts ama makojwa kama ni wanyama , serikali iwe ikilipa wananchi. Kama itakavyo tokea. I go ahead.

**Com. Salome Muigai**: Uaona huyu ananizumbua, I haven't beern paying attention. Thak you for stopping.

**Richard Koech:** Okay, nitarudia, kuhuzu chan'ga, tuseme "droughts" ama magonjwa kwa wanyama, kwa maoni yangu ningetaka serikali iwe ikilipia. Ikiwalipa wananchi. Kama kutatokea ukosefu wa chakula, serikali iwe ikilipia wananchi, kuliko kupewa chakula ya relief. Kama kuna makonjwa kama ya wanyama ambayo itatokea wananchi wawe wakilipwa. Kwa mfano tuseme diseases zitokea kama area hii, ng'ombe sikufe, ama magonjwa mengine, serikali iwe ikilipa.

Ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai**: Thank you very Mr Koech kwa maoni yako. Jacktom Moru. Job Kigeni,

**John Kigeni**: Kwa majina ni Job Kigeni Chebuleyo. Maoni yangu kuhuzu Katiba ni kama ifatavyo. Kwanza ni mambo ya land issues. Mashamba. Utakuta katika Kenya hii kuna watu ama matajiri ambo labda wako na mashamba…………..Interjection by Com . Salome.

**Com. Salome Muigai;** Tafadhali huko nyumba makiendelea kupiga kelele, ndio yenye inashikwa na hizi kanda zetu za kunazia habari. Na tungetaka kusikia maoni yenu tu. Siyo kilele zile zenye hasitatueleza watu wa hapa walisema nini. Kwa hivyo tafadhali tutuliye kidogo.

**John Kigeni:** Kuhuzu mambo ya mashamba utakuta kuna matajiri ambao labda wako na mashamba katika sehemu mbali mbali katika nchi hii yetu. Na utakuta badhi ya hayo mashamba huwa hayatumiki na kuna wale ambao hawana kabisa chochote wanaenda wakiombahomba vibarua. Napendekeza kila Mkenya apewe shamba akiwa amehitimu umri wa miakaa thelathini, hectare ya five hectares, that is average.

Maoni mengine ni kuhuzu dowry au mahari. Utakuta kwamba katika Kenya hii, sehemu moja uwa inahuzisha kulipa mambo ya mahari. Kwa mfano utakuta kijana anapooa, wazazi wake wanalipishwa mahari. Na utakuta katika jugumu la kulea watoto, kila sehemu inasaidia kwa njia yeyote ile. Kwa hivyo ikiwa ni baba wa kijana, pendekezo langu ni kila upande walipe mahari, sio upande wa kijana peeke yake.

**Com. Salome Muigai**: Kila pahali kila mmoja kilipa mahali kwa nani Bwana Kigeni?

**John Kigeni:** Sasa tusema kama kwa upande wa bibi awe wanatoa kitu kidogo halafu wanapatia wale wazazi wengine.

**Com. Salome Muigai:** Na wale wengine wanalipa nani?

**John Kigeni:** Wale wengine. Haya kwa upande wa Rais, kuna sheria zingine ambazo uwa anatakiwa, ningependekeza akatiliwe power zake. Kwa mafano nomination of MP’s and councillors. Utakuta baada ya mtu kufanya ama uchaguzi ama kuomba campaign, unakuta ameshindwa lakini Rais mwenyewe anawarudisha pale katika Bunge. Hayo ndiyo maoni yangu.

Asanteni.

**Com. Salome Muigai:** Tom Leberichi. Daniel Barno.

**Daniel Barno**: Kwa majina yangu kamili ni Daniel Barno. Maoni yangu ni kuwa pendekezo langu kuhuzu swala la elimu ni kuwa elimu serikali igharamie kwa sababu elimu ni kwa ajili ya watu wote kwa sababu kunazo familia zingine ambazo haziwezi kujimudu ama haziwezi kusaidia kila mtoto apate elimu kwa nchi. Kwa hivyo serikali ichukue hilo jukumu kuanzia class nane mpaka form four level na hata katika university kwa sababu ni vyama sana kama nchi ingekuwa na watu wenye wameelimika.

Lingine tena ni kwamba ni kuhuzu swala la Urais, ni kuwa uwezo uwe wa ustani kwa Rais. Kwa sababu njizi tunavyoona ni ya kwamba, ikisemekana ishukishwe mpaka liwe halina uwezo kamili, basi ataiongozaje nchi. Kama halina uwezo. Kwa hivyo jukumu hilo vilevile liwe tu lingaliwe lisiwe lile la chini sana ambalo halina maana.

Kw a hivyo kuhuzu Parliamentary, ni kwamba ni vyema tu kama tumefanya uchaguzi mmoja kwa ajili mtu kama ameshida kwa kiwango ambacho ni cha kadiri kama vile ni ya hamsini na moja kwa mia, aendelee kwa sababu, tukisema hajashida ama hajafanya nini tuwe tukirudia. Ebu tuelewe ya kwamba hata ile sehemu ya kurudia kurudia ni hasara kwa nchi ama kwa sisi. Marasilmali zetu sinaendelea kupongua kwa sababu ya mambo ya kufikiria pengine huyu haingekuwa vile .

Na lingine ni kuwa kama ni upande wa ujumbe ama wa Bunge, vile vile akifika hayo kiwango ametosha kuendelea. Kwa hivyo yangu nafikiri ni hayo.

**Com. Salome Muigai:** Asanate sana bwana Daniel Barno kwa maoni yako. Sasa nataka kumuita Bwana Ptrick Kichui.

**Patrick Gichui:** Kwa majina yangu ni kama vile wametaja hapo. Patrick Muiri Gichui. Na pendekezo langu ama maoni yangu ni kama ifuatavyo.

The Constitution should respect and regard the Kenyan people as supreme,it should recognize all Kenyans, respect and protect them and their property. It shoud also recognize the ethinic, …….and cultures. The Constituion should ensure equal and fair distibution of resources and job opportunities. Every Kenyan as a right to secure a job.

The Government should state, must protect is citizens. There should be no policies like retrenchment, meaning security on workers should be provided not unless or in case of wrong doing like stealing.

The aged should be taken care of by the Government I.e, from sixty years by paying some pensions and provided with health care, e.t.c. Other less advantaged people like orphans and the disabled, the Government should also take care of them.

The Constitution should protect the entire and encourage every family to live united as a the nation as discouraging street people and children.

The Constituion should protect the rights of children belonging to the couples who live together, separated or divorced. And even those ones born of the marriage.

**Com. Salome Muigai:** You have one more minute. I gave you three minutes. So reading takes a longer time. If you just the highlight because what is there, it takes a shorter time.

**Patrick Gichui:** The Constitution should recognize inter-tribal marriage. A law should be the guiding rule rather than different cultures of their origin.

Elections, election fro civic and parliamentary and Presidential should be done once every five years. All the polling stations should be in public place. After casting of voters, the counting should be done at the Polling Station and the Officer in charge approve the result having witnessed by the agent.

**Com. Salome Muigai**: The last point.

**Patrick Gichui:** Infact they are many, but what I don't know is what to do but I will just propose if you don't want to finish so that people can hear.

**Com. Salome Muigai:** I do, that is why I am giving you a chance to do the last point.

**Patrick Gichui:** The winner should be determined by simple majority in these including the Civic Parliamentary and the Presidential Elections. Civic and Parliamentary elections to be done together and Presidential different after the civic or Parliamentary.

**Com. Salome Muigai:** Thank you very much sir.

**Patrick Gichui:** Nilikuwa ninafikiria kwa vile watu sio wengi sana wenye wanangojea

**Com. Salome Mugai**: Wakimalizika nitakupa nafazi nyingine.

**Patrick Gichui:** Basi nitangojea.

**Com. Salome Muigai:** Haya.

**Patrick Gichui**: James Njuguna, endelea James Njuguna, ananza na majina yako kamili tafadhali.

**James Njuguna:** Majina yangu ni James Njuguna Gichuhi na ningetaka kutoa maoni yangu nikisema uchaguzi wa President unaeza anzia ikiwa mtu ni wa miaka arubaini hadi sabini.

Ningetaka kusema, hali ya msitu, forests, kuwe na forest reserve katika Kenya, Kwa sababu hali ya masingira imeleta taabu nyingi sana ya mvua katika nchi yeu.

Ningetakusema la tatu hali ya mashamba, katika wakati huu, kila mtu awe na huru kunua shamba popote katika nchi yetu.

La nne ningehitaji hali ya soko huru, wananchi wanapata hasara kubwa wakati wamelima, kilimo chao, na hiyo mahindi inanunuliwa kwa bei ya hasara ama sukari umenunua kwa bei mbaya kwa sababu ya nafaka zimetolewa nje. Kuwe na percentage katika vitu vya kutoka inje.

Ningetaka pia hali ya Parliament ijisimamie, judiciary ijisimamie na pia Constitution ijisimamie. Ili isichanganyike wakati wa uchaguzi ama baada ya uchaguzi. Ningetaka pia voting wakati wa kupiga kura watu walizie kura mahali wanapikia. Wawe wamechaguliwa hap na isomewe hapo. Kwa hivyo matoleo iwe kwa voting place.

Ningetaka pia kazi, ikiwa kuna kazi inapeanwa, mtu apewe kazi kulingana na masomo yake.

Ni hayo tu. Asante.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana, David Kuria Kirogo. Joseph Chemtei, Jane Wangeshi , Grace Wajiku Kimani. Alipata nafasi ya Kusungumza, okay, Rebbeca Nduta, alizungumza, Luzy mwangi alizungumza, Regina Nyambura, James Ngungu Kashiri. Daniel Macharia, Ibrahim Muhindu Kikonyo. Karibu.

**Ibrahim Muhindi Kikonyo:** Asante sana kwa vile nimepatiwa nafasi hii na sasa jina langu ni Ibrahim Mhindu Kikonyo. Na yale ningependa kuzungumza hali ya mashamba ya Rift valley. Katika mashamba ya Rift Valley tumepatiwa Title deed lakini hizi Title Deed wakati tunaingalia, tunaona imeandikwa mwaka wa tisaini na tisa. Na hapo tukajiuliza ni mahagano gani hii Title inakuwa ya miaka tisaini na tisa. Na sisi ni Wanakenya. Tungependelea sana kwa maoni yangu, hizi Title Deed ya Rift Valley iwe kama Title Deed za Central Province ama ya ………… kama vile tukiwa WanaKenya. Tuakae kama wengine. Nikiangalia ninaona ile mambo iko ni ile ya kikoloni ya zamani.

Hii mambo ya mashamba wakati tulikuwa tunahitisha uhuru wa Kenya, tulikuwa tunatakia kila mwanchi wa Kenya awe na uhuru wa kudumu. Na sasa mashamba yale yalikuwa na wakoloni, ma-settlers, sasa yako na ma-settlers wengine ambao walingia Kenya. Kuna wengine wako elfu tatu ya hectare. Kuko na wengine wako na elfu tano. Ningependelea kwa maoni yangu, hii mahekari mingi namna hii, watu wengi hapa Kenya hawana mashamba, na wengine hata hawana mahali pa kaburi ya kusikwa wakifa, pengine watasikwa barabarani. Sasa tafadhali Katiba ichukue jukumu ya kuchukua hii mashamba igawie wananchi.

Maoni yangu ni kwamba hatutaki wenye mashamba makubwa kunyanganywa, lakini shamba lake iwe kama hekari hamsini na ingine igawiwe wananchi. Ndio kila mawnanchi awe na makao. Kwa sababu tukiangalia sana, hata watu wetu katika Kenya wana taabu zaidi ya makao. Ukienda kwa mashule unaona watoto wale wanazaliwa wanaendelea kuoa, na sasa hawa hawana makao. Watu hawa ndio ninaona wanarudi kuangaika hata pengine wakawa wezi. Kwa sababu hawna chochote wala makao wala nini.

**Com. Salome Muigai:** Mzee una takika yako ingine moja. Kwa hivyo endelea kumalizia. Asante sana.

**Ibrahim Muhindi Kikonyo:** Sasa kwa hivyo tukiangalia zaidi mambo ya kikoloni inatufinya sana. Kitu kingine ni kuhuzu mkesi inayouziana na mashamba, watu wengine wale maharamia wanaenda kuwa mawakili katika korti na wanapewa pesa. Wanaenda kufanya kesi na wanashinda wananchi ambao hawana nguvu na kutaka kuwanyang'anya mashamba yao. Na hiyo si haki. Ni afadhali kesi kama hizi zirudishwe kwa Chef na wazee wa kijiji kwa sababu hao ndio wanajua mambo ya mashamba kuliko wakili. Wakili hakuna kitu anajua kwa maana huyu ni mtu aliyeandikwa na anatamani pesa. Sasa hiyo ninaona afadhali katiba ichukue jukumu la area hiyo alafu itusaidie sisi tukiwa wananchi. Kwa sababu hapo ni shida kubwa. Wazee weninge hizi kesi sinaenda kumaliza hata miaka kumi kwa korti na hao huenda kortini kila siku na hana nguvu na pesa ya kwenda huko. Hana gari.

**Com. Salome Muigai:** Hiyo point tumeeliwa Mzee. Kuna nyingine,?

**Ibrahim Muhindi Kikonyo:** Ukinikubalia ninaweza kutoa nyingine.

**Com. Salome Muigai**: Basi ninakubalia nusu dakika.

**Ibrahim Muhindi Kikonyo:** Kile kingine ni hii mambo ya utoto kama mtu akiwa kama mzee sasa nyumbani na mama, tumzeeka, na tumezaa watoto wetu. Na hawa watoto unaona mtu anaoa msicha wa mtu. Akienda nyumbani kwao, hanazaa watoto wawili ama watatu alafu baaadaye, akiona huyu msichana ananuka, anamfukuza na kumrudisha kwa baba yake. Sasa hawa watoto ndio unaona wanakuwa choKora.

**Com. Salome Muigai**: Ungetakaje Mzee, Ungetaka katiba ifanye nini?

**Ibrahim Muhindi Kikonyo**: Ninataka Katiba iangalie sana, yule mtu anayeweka msichana mimba na anazaa afUATWE sana. Asomeshe hawa watoto kuliko kuletea Wazee waliomaliza kazi na kumleta kazi nyingine,na hao wameyazeeka. Nafikiri hayo mwalimu imetosha. Asante.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana mzee umejieleza vizuri kabisa. Jiandikishe pale tafadhali.
Araja Okimwa. Margret Wambui Peter. Monicah Wairimu Mbao. Geoffrey Kiraku, ni wewe Mzee, okay. Njoo utupe maoni yako.

**Geoffrey Kiraku**: Asante sana, mimi manaitwa Geofrey Kiragu, na kwa maoni yangu Serikali ilifanya vizuri kusema tutoe maoni. Katika Katiba maoni yangu ninasema mtu atoe maoni yake vile Serikali inataka itutawale.

Mimi ninataka Katiba iandikwe kwa lugha ambayo inaweza kueleweka . Ikuwe kama bible. Ndio kila mtu aweze kusoma mambo yote. Mtu akipelekwa kortini najuwa ya kwamba inakosa sheria fulani lakini ya siku hizi ni ile ya mkoloni.

Ya pili ninataka mjumbe yeyote pahali amechaguliwa awe na office kwao, pahali anawakilisha. Hatutaki kumtafuta huko Nairobi na tunataka awe na office pahali anapo wakilisha.

Ya tatu, hatutaki serikali ya majimbo, tunataka serikali moja. Kwa hivyo kwa moani yangu tena, kwa mtu pahali alipo, anakuwe abaki hapo baadala ya kusema ati hapa si kwenu, watu wabakie pahali walipo.

**Com. Salome Muigai:** Umemaliza mzee,

**Geoffrey Kiragu:** Bado inabaki moja tu.

**Com. Salome Muigai:** Basi hiyo moja itoe.

**Geoffrey Kiragu:** Mimi ninataka President awe akichaguliwa na raia. Ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai**: Basi asante sana Mzee. Peter Mwangi Wahome, John Maina Mwangi.

**John Maina Mwangi**: Asante sana. Mimi ninaitwa John Muriuki Maina, Mambo yangu ile mimi naona ni ya kutengeneza Katiba ni hili moja.

Siku za Mzee Jomo Kenyatta, sisi tulikuwa tunasoma masom ya bure na siku hizi watoto wanakuwa kama machokora hawasomi. Kwa sababu wazazi hawana pesa ya kulipia karo watoto wa shule.

**Com. Salome Muigai:** Sema Pendekezo lako?

**John Maina Mwangi:** Pendekezo langu ni kusema aendelea ndelee kusaidia wazazi kwa sababu watoto wale wengi ni watoto wa masikini, wale ambao hawasomi. Serikali ianglie hayo maneno.

**Com. Salome Muigai**: Endelea,

**John Maina Mwangi:** Wangalie maneno ya watoto kuhuzu masomo kwa sababu wazazi hawana pesa ya Karo.

**Com. Salome Muigai:** Hilo tumeelewa nenda kwa jambo la pili.

**John Maina Mwangi:** Jambo la pili ni mambo ya Hospitali. Ukienda kwa hospitali unaitisha pesa na zamani ziku za Mzee, kukuwa na malipo. Watu walikuwa wanatibiwa bure.

**Com. Salome Muigai;** Asante endelea.

**John Maina Mwangi:** Hii ni mambo ya wazazi na watoto wao. Wengine hawatengenezi watoto wao kulingana na mila na desturi. Tuko na mambo ingine ilikuwa inarudishwa kwa Chief na Wazee wa mitaa. Kenya police wako na kazi yao, sasa moani yangu, Chief yuko na kazi yake na wazee wa kijiji. Kwa hivyo ni wajibu wa kila mtu kujua kazi yao.

**Com. Salome Muigai:** Hilo ndilo la Mwisho.

**John Maina Mwangi**: Ndiyo ya mwisho.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana John Maina Mwangi.

**John Maina Mwangi**: Asante sana.

**Com. Salome Muigai**: Florence Njeri Wainaina., Daniel Mimariki, Samuel Mburu Kamau. Sammy Chege, wewe ni Sammy Chenge, wewe ni Samy Chege, unasema present Mandam?

**Sammy Chege**: Unasema Present Madam,

**Com. Salome Muigai**: Asante ndio ninajua unakuja nisimwite mtu mwingine. Endelea na utupe jina lako.

**Sammy Chege:** Asante jina langu ni Sammy Chege Mwangi.

Pendekezo la kwanza ningetaka kupendekeza hii hoja ya ati wamama na wanaune watoshanishwe kimaisha. Kenya ni nchi ya Kiafrica na ina kimila na desturi zake. Hatutaweza kwenda kuiiza zile tabia za wazungu………….Interjection by Com. Salome Muigai.

**Com. Salome Muigai**: Tafadhali zungumzia kwa Microphone ili uende kwa recording.

**Sammy Chege:** Ninasema ninataka kupendekeza hii hoja ya kusema ati wanaume na wanawake watoshanishwe kimaisha. Kenya ni nchi ya Kiafrica na ina mila na desturi zake. Sasa wanawe na wanaume wakitoshanishwa, itaingilia mila na desturi zetu na pia tena kidini. Kwa hivyo ningetaka mwanamke achukue wasifa wake katika jamii na mwanaume achukue wasifa wake.

Jambo la pili ningetaka, pia katika hii idara ya polisi, ikiwa wanalinda serikali, pia wao nao kuwe na idara ingine ambapo hata hao wakipata makosa huwe wanashitakiwa.

Hoja ya tatu ni kuhuzu remand. Mimi ningependekeza rimande imaliswe. Mtu akishikwa anaenda na kufanyiwa kezi na kurudi nyumbani. Na iwapo kezi haitafanyika siku hiyo, basi aiongojee akiwa nyumbani. Maanake mgine anaenda anateseka pale remand pengine anatumwa kortini ndani na mwishowe pengine ile kezi haitamuangukia. Basi anakuwa ameteseka bure.

**Com Salome Muigai**: Asante sana kwa maoni yako Sammy Chenge, lakini Sammy nilikuwa na swali moja kwako. Hizi desturi zetu za kiafrica, sinabadilika ama simekaa pale pale penye silianza. Kwa mfano wewe na mimi tunatoka kwa mila yenye ilikuwa haifahi hizi nguo zenye tumevaa, hatutumii hizi vifaa vyenye tunatumia leo na sasa tunasitumia. Hii mila inaendelea ikibadilika ama inakaa tu bale kama kitu chenye kimekufa?

**Sammy Chege:** Hapo ndipo ninasema tunahikiza mia za wazungu, kwa vile hata nguo tunavaa za wazungu. Ndipo maisha inaendelea kutukandamiza. Kwa hivyo tusiingishe hata tabia za wazungu basi utakuta hata ndoa tutakuwa tukifanya sinafunjika. Kama vile wao wengi hawatili ndoa maanani.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo unanaona mila zetu hasibadiliki?

**Sammy Chenge**: Mila zetu tuwe na msingi. Tusibadilishe kama mavazi.

**Com. Salome Muigai**: Lakini sinabadika ama sinakaa tu? Sikiwa timamu hilo ndilo swali langu?

**Sammy Change:** Simenda sikibadilika.

**Com. Salome Muigai:** Francis Kigeni, Francis Kigeni? From a youth group. Monica Wajiku, Lucy Muthoni, Michael Mwangi Kitahi, singers group.

**Michael Mwangi Kitahi**: Kwa Majina ni Michael Mwangi Kitahi. Pendekezo langu ni kuhuzu hali ya ma-groups. Kweli hapa ama katika nchi yetu ya Kenya kuna Ma-groups wengi wao ni watu ambao hawajasoma. Na wengi wameungana kujifanyia kazi zao kujipatia mali yao ama matumizi, lakini kwa sababu ya pesa, wanashindwa. Mapendekezo yangu ni kwamba, serikali ichukue jukumu la kuwasaidia.

Pendekezo langu lingine ni hali ya manyumbani. Ama hali ya watu kukaa kwao manyumbani. Kam ni Wazee waweze kuongeza na watoto wao. Na kuwa eliza vile nchi inastahili kukaa. Na kama Mzee ameshindwa na kuongea na watoto wake, anaomba mzee wa karibu kumsaidia kwa maana manyumba inakuwa mkumu kwa sababu Wazee hawataki kuongea na watoto wao.

**Com. Salome Muigai;** Je hii inaweza kuwekwa kwenya Katiba. Unapendekeza hiyo iwekwe kwenye Katiba.

**Michael Mwangi Kitahi:** Ndiyo

**Com. Salome Muigai:** Iwekwe je? Pendekezo lako ni lipi

**Michael Mwangi Kitahi:** Iwekwe kulingana na watu, hali ya kukaa. Pendekezo langu lingine ni hali ya watu kuwa na amani. Amani inatoka kwa watu kulindwa na serikali. Kwa maana serikali imekuwepo ili kuwalinda watu. Hasa kama polisi, Ma-Chief na manaibu wao. Wanasitahili kuwalinda watu kulingana na ma-area zao. Kwa sababu hali ya msozano unaingia kulingana na watu kukosa kuelewana.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana Michael Mwangi Kitahi, Ptrick Gichui, Patrick Gichui, Margret Njoki Kuria, Magret Njoki Kuria? Francis Kithenji.

**Francis Kithenji:** Jina langu ninaitwa Francis Kithenji. Maoni yangu ni ni kuhuzu Ulinzi. Sisi watu wa Kenya, ni kusikia ninasikia ya kwamba kila bahali watu wanauawa na wakuuawa na tuko na serikali, hii inamanisha sasa wananchi hawatapata watu wakuwachunga. Na mimi maoni yangu kwenye Katiba tuwe tunalindwa kwa mali zetu na mambo yetu yote.

Jambo la pili, ……interjection by **Com. Salome**

**Com. Salome Muigai:** Mzee ngoja kwanza, endelea.

**Francia Kithenji:** Mimi ninasema ya kwamba, ulinzi hakuna kwa watu wa Kenya. Kwa maana kila…………. hata radio inasema watu wanauawa. Serikali yetu ichukue hili jukumu maana kwenye Katiba ya kwanza hata wakati wa hayati, ilisema ya kwamba tulindwe pamoja na mali yetu.

Jambo la pili, ninaonelea kamba Chief awe anachakuliwa na raia. Pia zamani alikuwa nachakuliwa na raia, akiwa na masoma ama hana lakini ako na ulimi wa kuongea na raia. Hii mabo hii yote iwe inaendelea barabara. Kwa hivyo maoni yangu ninaendelea kusema hali ya masomo, 8-4-4 imalizike. Maana 8-4-4 pia hatuelewi sisi wazazi vile inaendelea. Zero ukiongeza zero inakuwa zero. Kwa hivyo ningependekeza Katiba ya sasa kwa maoni yangu 8-4-4 imalizwe. Irudi ile ilikuwa ya Gari Francis. Ili tuelewe kila mmoja. Maana hata watu wa form six wanshindwa na kuesabu. Maoni yangu ni hayo.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana ebu nikumbushe jina lako, Francis Kithenji. Thank you. Daniel Kamu Nderi.

**Daniel Kamau Wa-nderi:** Maoni yangu kuzu Katiba, ninataka kama rahisi akichakuliwa , awe na kazi moja, iwe kazi ya urais, asiwe mwalimu ila ya urais tu.

Ingine ni mimi raia, niwe nikilindwa na mali yangu. Hali ya uchumi, mimi ndiye inajua vile nitafanya. Kwa sababu mimi niko na mikono, serikali na kama inalinda,nami nitafaNya kazi yangu vyama. Hayo tu ndiyo maoni yangu.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana Bwana Daniel, jiandikishe pale. Wanjohi Macharia.

**Wanjohi Macharia.** Jina langu ni kama vile mmesikia, Wanjohi Macharia. Vile mimi ninataka kusema Katiba yenye iko ndio tunaka kupiga kura nayo. Tuchague yule kiongozi tunayependa. Hatutaki kichagua viongozi ambao hatujapendekeza, tupikie kura yule tunamjua na mwenye atatusaidia. Kwa sababu wale tumechagua wakati miaka iliyopita wanaenda na kuchukua mushahara na ila hatusaidii na tunateseka bure. Tuko na taabu ya shule, makanisa na mambo ya nyumbani kama ukulima na hata hatuna soko. Tunataka maziwa yetu yawe yakipelekwa kwa KCC. Na maziwa yetu, yakifika kwa cereal board tupatiwe pesa hapo hapo kama vile kulikuwa na KFA, kwenye tulikuwa tukipeleka mazao yetu na unalipwa hapo hapo.

Kuna chama kingine tunasikia kinaitwa Mungiki. Hiki chama sisi hatukitaki. Tunataka serikali ichukue sheria na hatutaki kuvaa ng'ozi wala tunataka maendeleo kwani tuko na uhuru.

Shule zetu……………….interjection byu Com. Salome Muigai.

**Com. Salome Muigai:** Zungungumzia kwe microphone Mzee kwa ajili ya hiyo kilele. Leta microphone karibu na mdomo wako.

**Wanjohi Macharia:** Shule yetu tunaka kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la nane, hiyo iwe ni ya bure kama zamani. Hatukuwa tunanunua kalamu, vitabu vya kusoma , yote ilikuwa inaletwa na Serikali. Serikali yetu itusaidie kwa maneno haya.

**Com. Salome Muigai:** Jambo la Mwisho Mzee ?

**Wanjoki Macharia**: Hospitali serikali inalipa nusu na sisi nusu, na yule mwenye hana pesa ya ile nusu anateseka na hawezi kwenda kwa hospitali ya Private kwa sababua hana pesa. Tunata hospitali iwe bure kama zamani.

Asante sana.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana jiandikishe. Rafael Kamau.

**Rafael Kamau:** Kwa jina ni Rafael Kamau. Na kwa mapendekezo yangu, ya kwanza ni juu ya mahakama, ninaona iheshimiwe na ijiheshimu yenyewe kwa sababu unaona anashikwa na ana hukumiwa. Na akitaka kufanya rufani akiwa amefungwa na mahakama ile ile, nafanya rufani na ionaona mtu yule ambaye alifungwa yuko inje. Na alikuwa mhalifu na rahia wanajua na akishapewa rufani, anarudi na anaendelea na ualifu wake. Kwa hivyo, tunaona mahakama ni vizuri ijiheshimu kwa sababu kwanza alienda kortni na akaukumiwa na baadaye tena akaachiliwa. Kwa hivyo tunaona wale wanaotoa rufani wako inje na alikuwa amefungwa, ni kama kuambiwa aende akatafute pesa apate kupeana kule. Kwa hivyo hiyo iangaliwe sana.

Ya pili ni juu ya uchaguzi. Maoni yangu ni kura kuesabiwa kwa vituo vya mahali kura emesabiwa.

Ya tatu ni juu ya watumushi wa serikali kama PC na ma-DC nahata DO's wawe wakiandikwa …..Interjection by Com. Salome.

**Com. Salome Muigai:** Ngojea nipe nafasi kidogo, tafadhali tutulie ili kelele za mvua, kelel zenu wenyewe halafu yule mwenye anazungumza, hatasikia hata kidogo. Na kanda zutu za kunazia habari sitajukua tu hayo makelele. Tafadhali tutulie ili hizi kanda tukifikisha kule Nairobi, wale wanatume wenye hawako hapa nao wasikie maoni yenu. Endelea.

**Rafael Kamau:** Wasiwe wakiandikwa na rais. Wwe ni watu ambao wanaandikwa ana tume ya uajiri.

Ingine ni juu ya makamu wa Rais tena kuchaguliwa……..interjcetion by Com. Salome Muigai.

**Com. Salome Muigai**: Na hiyo iwe ni ya mwisho Mzee.

**Rafael Kamu**: Na asiwe anachaguliwa na Raisi. Awe akichaguliwa na bunge. Na kwa sababu umenikatiza kidogo, waja niseme hii ya mwisho. Habari ya Ma-chief, wapewe uwezo mkubwa na wawe wakichaguliwa na wananchi wale wakaribu. Lakini wasiwe wakuchaguliwa na kuandikwa na serikali huko inje. Wawe wakichaguli mahali wanafanyia kazi na wapewe mamlaka kwa sababu hao ndio wako karibu na wananchi. Ni hayo tu.

**Com. Salome Mugai:** Asante sana kwa maoni yako, Nelson Chebor, Nelson Chebor?

**Nelson Chebor:** Mimi ni Nelson Chebor. Maoni yangu ni kwamba serikali itupatie elimu bure. Kuanzia Class ya kwanza mpaka ya nane.

Ya pili, serikali ipatie nguvu Chief kwa sababu hawa ndio wanajua na hao ndio wanaweza kuwa na uwezo.

Ya tatu, serikali itupatie matibabau ya bure na maji. Kwa sababu serikali inasema inataka kuotoa umasikini lakini ni kama wanarudisha umasikini. Kama vile mwaka huu, mahindi tulipata lakini ilienda karibu bure,si umasikini umetokea kwa sababu watoto wengi sasa hawako shuleni, wamefukuzwa. Kwa sababu ya kukosa karo.

Na ingine ni hii mambo ya Katiba ya Bunge, tupige kura kama Katiba mpya imetokea.

Na ya mwisho, Serikali iangalie mambo ya ufisadi kama mambo ya ulinzi na despline. Tena nilikuwa nimesahau ingine, Mambo ya discipline kwa watoto wa shule, ati hakuna mambo ya kuchapa watoto, hiyo irudishwe kwa shule kwa sababu hiyo ni kuanzisha ukora kwa hiyo iangaliwe kabisa.

**Com.Salome Muigai:** Asante sana bwana Chebor. Elizabeth Wahiga Mathenge. Maina Kamangu. Kenneth Kamuren.

**Maina Kamangu:** Kwa jina ni Maina Kamangu. Pendekezo langu ni hili. La kwanza kuwe hakuna mtu yuko juu ya sheria.

Ya pili, hakuna mbunge afahaye kuwa waziri isipokuwa wasiri atolewe kwa wale watu hawajachaguliwa. Kwa sababu akichaguliwa yule alikuwa mbuge, hawezi kutumikia watu wale walimchagua, na atumikie Rias yule atakuwa yuko.

Ta tatu, hii sheria ambayo iliondoa watu ndani ya forest, iondolewe kabisa watu warudi kwa forest kama zamani. Kwa sababu walitoka huko kwa forest, ndio njaa iliingia kwa dunia. Na kwa sababu ya hiyo, watu walikosa kazi na njaa ikaingia. Hata

hakuna mti inapatika huko kutoka ile siku waliondoka huko. Yangu ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana Bwana Maina Kamangu, Jiandikishe pale, Kenneth Kamren.

**Kenneth Kamren:** Asante sana kwa majina ni Kenneth mine I will read something I have prepared here.

**Com. Salome Muigai:** You have three minutes sir.

**Kenneth Kamren:** The first one I would like the new Constitution……….Interjection by Com. Salome Muiga.

**Com. Salome Muigai:** Say your name

**Kenneth Kamren:** The first one, I would like to put forward in about the land. Land is the most basic economic necessity available in these country and n the past, ownership of land has been misused. In this area there are so many people who have land and they don't utilize it. I would like the recommend that if the land has been idle for the last ten years. The State should take over the land and allocate it to certain people. Because there is ….. People owning land all over the country and they don't use it and we have enough poverty.

The second point I would like to put is about the executive about the President and the Prime Minister. I would like asking to ask for the powers of the President reduced and given to other organs of the Government. New Constitution should provide that the President should not dissolve Parliament, not to appoint Commissions because there are so many resources which have been used by the Government on Commissions and these Commissions end up doing nothing. And Presidne should not appoint civil Servant.

I would propose that there should be a position of the Prime Minister whose duties should include running of the government, day to day, the political parties should elect the Prime Minister, that is the head of Government with majority in an election. The said Prime minister should appoint the Minister from the winning party. There President therefore I am recommending to be the head of state and commander in chief.

Another issue is about the Local Authorities. I would propose in the new Constitution that election of Local Authorities be determined by the new Constitution in such away tht the Mayors and the Chairmen should be elected directly by the people.

And again I would like the issue of the Title Deeds to be centralized. In such away that every district should process title deeds and issue them instead of people going to Nairobi. In Past there has been so many faulty titles because of some tenders of some officers in Nairobi, issuing fake Title Deeds.

And then the last issue which I would like to the Commission to take into the consideration is about the management of forests. Forest should managed by the Locals themselves and a committee should be formed in every district such that forests should be revered to trustees so that the revenue got from the forests should be taken by the locals who should manage their own forests. So that this forest officers should not be the ones managing them because they have accused these responsibilities. Thank you.

**Com. Salome Muigai:** thank you very much, I have seen that our technology is failing as once again, Jiandikishe pale Bwana Kenneth Kamren. Samuel Muriuki. Asamuel Muriuki.

**Samuel Muriuki:** Okay, mimi ninaitwa Samuel Muriuki na mapendekeze yangu ni kama ifatavyo. Kwanza kabisa…………Interjection by **Com. Salome Muigai.**

**Com. Salome Muigai:** Ebu zungumza kwa sauti ya juu ili wengine wasikie.

**Samuel Muriuki:** Kwanza kabisa nitaongea kuhuzu elimu. Mambo ya elimu ningependekeza kwamba, elimu ya shule ya msingi ipeanwe na serikali bure, ili kufanya watoto Wakenya angalu wapate kufahamu elimu ijapo kidogo. Iwapo kama haitakuwa ni mpaka darasa la nane, iwe mpaka daraza la tano, namna hivyo.

Jambo lingine ningesema kuhuzu kuabudu, ningalisema uhuru wa kuapudu usidi kuwepo lakini vikundi ambavyo vinafnya kuabudu, kunatakikana viondolewe. Maanake vikundi vingine vinaitwa ni vya kuabudu lakini vinaleta utaza na sinasemakana si halali lakini bado siko. Kama vile Mungiki na singinezo ambazo sinazumbua wananchi wengi wa Kenya.

Kitu cha pili ni kuhuzu executive ya serikali. Ningependelea kwamba Rais asidi kuwa mkuu wa serikali wala pasiwe na jambo la wasiri mkuu ama makamu wa raisi zaidi ya mmoja. Hili litakuwa ni kukimbilia jambo ambalo sisi siwenyeji nalo na ambalo ni la kuwiga.

Jambo lingine ningependekeza kwamba political parties ama vyama vya kisiasa visizidi vya vitatu. Maanake sasa hapo manaleta ukawanikaji haza wa kikabila.

Jambo lingine ni kuhu parastatals ama mashika yanayoanzishwa na serikali…………………….
Kuhakikisha kwamba jambo la job opportunities ama nafasi za kazi kwa vijana hasikosekani.

Jambo lingine ni kuhuzu Commisttes ambazo sinateuliwa na serikali. Ningependekeza kwamba committee hizi ziwe huru wala siziingiliwe na mkuu wa serikali husuza ni kwa sababu report zingine huwa sinaundwa lakini hasifiki ama zinafinjwa.

Jambo lingine ni kuhuzu Judiciary, Jambo hilo pia ningependekeza kwamba Judiciary let it maintain independence. Pasiwe kamba kutakuwa na kuteuliwa katika Judiciary ambapo mtu ambaye atateua Ma-Judge, bila shaka watatekeleza kulingana na matakwa yake.

Mwisho kabisa, ninasema kwamba jambo la urekebishaji wa Katiba, ningependa lisifanywe kwa upesi ama kwa kazi sana, kwa sababu ni jambo sentive. Hebu twende taratibu mpaka Katiba itayarishwe kulingana na itakavyo kuwa. Na ningependekeza kwamba, kabla ya uchaguzi, pawe na Katiba ambayo ni ya muda tuu. Maanake tukifanya uchaguzi na Katiba hii imetuzumbua kwa wakati mwingi. Asanteni sana. Kweheri.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Kijana mwenye maono, tunapendelea sana maoni yako. Samuel Erika.

**Samuel Erika:** Pendekezo langu na la nchi………..Interjection by **Com. Salome Muigai**.

**Com. Salome Muigai:** Jina tafadhali.

**Samuel Erika:** Jina langu ni Samuel Erika. Pendekezo langu ni Katiba mpya iangalie masikini wale wenye wako Kenya, hatutaki uamasikini. Zamani tulinyanyaswa na wazungu na wakati tulipata uhuru umasikini uliisha. Na tena hatutaki wazungu warudi hapa tena ama Katiba ya kurutisha wazungu. Tunataka Katiba ya kuangalia masilahi ya watu kwa njia ya amani, na isiwe ya kutenganisha watu, na kila kitu kiliyoko hapa kilindwe. Hata ikiwa………..…. ama mtoto.

Katiba iangalie masilahi ya Ma-Chief na mikutano.Wanunuliwe magari na sisi zote tuwe kitu kimoja. Kama ni kura tupinge kwa amani na tuchague watu wanyenyekevu tunao wapende kwa njia ile inafaa. Na wala si kwa njia ya ukabila kama huyu ni Mkamba, Kikuyu ama Mkingi maanake wote ni watu wa Mungu. Kwa hivyo sisi zote tuko hapa kurekepisha Katiba ya siku sijazo. Na Rais achaguliwa na wananchi na tusiunde Katiba ya kuaribu nchi ila ya kutengeneza nchi. Na umasikini uishe.

Na barabara tena inagaliwe sana kwenya Katiba. ……………interjection by **Com. Salome Muigai.**

**Com. Salome Muigai**: Point ya mwisho Bwana Erika.

**Samuel Erika:** Na ma-hospitali, watu waangaliwe sana kwa sababu malipo ya hospitali imekuwa kubwa sana. Wenigine ni masikini na hawana pesa. Mtu anaweza kukojenga haraka, na akipelekwa hospitali kunahitajika pesa na hana, atafanyaje?

**Com. Saloem Muigai**: Asante sana kwa maoni yako tunayawekea maanani. Jiandikishe pale. Elijah Taramu.

**Elijah Taramu**: Asante sana kwa majina ni Elijah Talamu. Pendekezo langu ni kuhuzu mambo ya elimu. Ningependekeza serikali kama ingeweza kupeana masomo ya bure kutoka darasa la kwanza hati daraza la nane.

Tena mambo ya forest ilindwe na ikiwa kiongozi yeyote katika nchi hii awe akilinda mali yake. Wa sababu kuna wengine ambao hawna makao, ama seshemu yeyote ya kuishi. Na ikiwezegana serikali intenge pahali karibu na forest kama crown land. Ili mtu yeyote akilemewa apate mahali pa kuishi. Kwa sababu sisi hakuna yule hataki kuwa mfugaji.

La tatu ni mambo ya madawa kienyeji. Kwa sababu tukiangalia kwa upande wa hospitali, watu wanasumbuka sana kuhuzu dawa na tunafuata ya wazungu. Pendekezo langu ni kwamba tunataka Serikali iweke maanani mambo ya dawa ya kienyeji. Kwa sababu tukiulizwa vile tulikuwa tunaishi zamani, tulikuwa tukitumia madawa ya kienyeji. Na hata wakati huu wale walikuwa wanaelewa wamekosa njia kwa sababu ya mambo ya kisasa. Wazungu waliandika mambo yao yakuwa mustari wa kwanza.

**Com. Salome Muigai**: Point ya mwisho.

**Elijah Taramu:** Point ya mwisho kwa wale wanao subuka sana kwa sababu ma-chief walikuwa wanatusaidia mbeleni na ningependekeza ma-chief waangali na wapewe nguvu zaidi kwa sababu yeye ndiye yuko karibu na wanachi na achaguliwe na raia maanake ndio wanamfahamu vyema. Serikali iangalie hilo jambo sana kwa sababu tunawahitaji kwa mambo yetu ya kinyumbani, ya Wazee ,Wamama na Watoto.

Na ya mwisho kabisa ni watoto wahadhibiwe. Apigwe akionyeshwa kiboko, kwa sababu ninakumbuka kutoka mwaka wa sitini, mtoto akikosa, alikuwa anapigwa hata na mgeni wakati anakosa. Na hiyo ndiyo ilikuwa inaleta discipline kwenye tulikuwa tunaishi. Kwa sababu kitambo kufikia kwa mzazi ilikuwa ngumu. Asante sana sina mengi.

**Com. Salome Muigai:** Swali moja kwako, unajua wakati huo hatukusikia habari ya watoto kufa shuleni ati wamepigwa na mwalimu, mpaka wakafa na wakaenda hospili. Kwa hivyo wewe unaonaje kwa kuwa huo wakati kumpa mtoto nidhamu pia imebatilika, tunasikia watoto wamekufa, wamesimia kwa shule, ungeona tunawezaji kutumia haya na kulinda huyu mtoto pia?

**Elijah Taramu:** Kitu muhimu yao ni mkuu wa shule apate kuangalia walimu wale wako rough. Kwa sababu kuna wale ambao wanatumia mambo mengine ya kienyeji katika sehemu ya masomo. Ili hata awe akiangalia time table kamili na kamati ushughulike na viboko iendelee taratibu.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana. Peter Kithiri, Peter Kithiri, Moses Mwangi, Karibu, na sasa nampa kila mtu dakika mbili mbli kwani kumenyesha na hatutaki tuwe kwenye hii barabara yenu kwa kisa na matope, itakuwa shida sana. Tungetaka

kuondoka bila kisa. Ulikuwa hutaki kueleza, nikuandika tu, haya. Mureithi Kariuki, dakika mbili Mureithi.

**Mureith Kariuki:** Jina ni Mureith Kariuki and my views are as follows: Well I will start with political parties. The political parties should be limited to two only. Parties should be financed by the Government and specifically from the Public funds.

The local Government: The Councillor and the mayors and the Chairmen of Council should be elected and they should have a minimum qualification that is per academic education that is. For anybody to be elected as a Councillor he should have a least minimum of C- in an O certificate. These should also apply for the ministers, that are the MP's not ministers. And for minister should they should be graduates specilised in the ministries.

Executives: The President should not be should not be any Constituency, that he should be above the Constituency and he should have at least a minimum acadamic qualification of a graduate. The Vice President have a minimum academic qualification of a graduate. The vice President should be elected and he should also be atleast a graduate. The President should be elected by the a 51 % of the total votes that is to be an outright winner.

The Constituencies should be demarcated as per population but not on consideration of that service. The election days should be separated. That is we should have election days for the President and the election days for the MP's and an election day for the Local Government councillors.

The election date should be specifies in the Constitution that is the President should not have the rights of calling for election whoever he feels like. Electoral Commissioners should be appointed by a parliamentary body, which consists of all the participants or all the parties.

Education should be free and compulsory, that is Primary education, the poor but bright children should be educated by the government up to the university. The community should be given power to protect the enviroment and natural resources, and specifically the forests.

The Presidential Commissions reports should be made public and not be shunned. The President should not have right to shunn the reports.

**Com. Salome Muigai:** You have fifteen seconds.

**Murethi Kariuki:** And lately Madam, Chief and Sub-chiefs should be elected and they should have a minimum education qualification of a C- in O level cerificate. Thank you.

**Com. Salome Muigai:** Thank you very much Murethi, Samuel Kamathi, ni wewe karibu. Daika Mbili.

**Samuel Kimathi:** Moani yangu ni Wabunge wasiwe wakipitisha hoja bila kupitia kwa wananchi.

**Com. Salome Muigai:** Anza na jina lako.

**Samuel Kimathi**: Samuel Kimathi

**Com. Salome Muigai**: Anza na jina lako, semea kwa microphone tunafanya recording. Tafadhali jina lako. Bado hulisemi kwa Microphone

**Samuel Kimathi:** Samuel Kimathi Kithenji.

**Com. Salome Muigai:** That is right.

**Samuel Kimathi:** Ninachangia Wabunge wasiwe wakipitisha hoja bungeni bila kupitia kwa wananchi.

Shule za Primary siwe za bure ili wananchi ambao hawana pesa waweze kujimudu.

Ya tatu, mkuu wa sheria awe akiteuliwa na Bunge.

La nne, watumishi wa serikali ambao ni wafisadi wawe walifunzwa kazi na kusitakiwa mahakamani. Ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai:** Thank you very much asante kwa kutumia wakati wako vizuri. David Murethi. Dakika mbili Murethi.

**David Murethi:** Jina langu ni Murethi Kaguru. Objectives, rights of the children. Children should have two parents, mother and father, no single parent should be Kenya unless through tests.

Free basic education in Primary schools and medical care.

Kenya should have two Parliaments, the house of representatives and the Senate. The Senate should see the Constitution is exercised well by the Government. Have power to take the President to the court.

Kenya should have a domant political President and the Prime minister elected by the Kenyans.

Not all parts of Kenya are economic productive, therefore, they cannot generate economy equally. In that case Federalism should not be exercised.

Last, the Electoral Commission should be a none political body. Elected or nominated by the strong parties or all parties.

Thank you.

**Com. Salome Muigai**: Mimi nina swali kwako umesema , rudi tafadhali, umesema hatutaki watoto wenye mzazi momja tayari tunao watoto wenye wana mzazi mmoja, tutafanya nini nao. Kwenye Katiba unataka tuseme nini?

**Daniel Murethi:** There should be law to be enforced to control all that.

**Com. Salome Muigai**: How does it get controlled, mwenye anazaa mtoto, msichan wako leo akipata mtoto, unataka tufanya nini na jambo hilo?

**Daniel Murethi**: The father of the Child should control the child until the age of twenty four.

**Com. Salome Muigai:** okay. John Mwaura, Alicen Chelaite, Alicen Chelaite. Karibu Madam, leo nakupa dakia pili.

**Com Salome Muigai:** Yes Madam Commissioner thank you very much, my names are Alicen Chelaite. I am contributing as an individual na Madama Commissioner can you release give me five minutes like others I was busy mobilizing. That is why you see many people.

**Com. Salome Muigai**: Okay, you have three and a half.

**Com. Salome Muigai**: Thank you very much. Preamble: I recommend that our Constituion have a Preamble which say we the people of Kenya to ikiwa our forty two tribes iwe named properly ili watu wasiwajwe inje kwa Constitution na pia tuwe na features ya kuonyesha ya kwamba hii Constitution ya Kenya kama animals zetu ama milima, mito na whatever.

Structures of the government, ningependekeza ya kwamba tuwe na coalition or coalition which is government of national unity with a Prime Minister. Why I say that ni kwa sababu tukiwa tu President pekee yake, tumeona vile Kenya imeenda.

MP's lazima wawe na full time, kwa sababu wanalipwa pesa nyingi na kila wakati tunasikia hawako kwa buge ama kwa Constitution. Kiningine ni MP's , kama wanalala wakienda Parliament na hawafanyi kazi kwa wananchi, waitwe nyumbani through vote of no confidence na tuchague mwingine aende.

Concillor na MP's wawe nominated by parties na wawe na special interests and 50% wawe wanaume 50% wawe wakina mama.

Parliament should be independent. President asiwe na powers zozote over parliament. Wapewe unlimited powers trough standing orders. A formative action be constitutionalized. So that it can allow women participation in Parliament and Local Authority and other decision-making positions.

Constituion should entrage the time for Parliament. Isiwe kwa mkono ya President. Extention of Parliament ifuatwe ile iko kwa present Constituion on section 59, bahali inasema mpak tu iwe na vita ndio Parliament iwe extended. Otherwise iendelee kwa hiyo miaka Constituiton inasema .

Executive: Presidential qualification should be O'level and above, that is degree. Functions of the President should be defined. Lazima isemwe na yeye tu awe na powers ya national issues ifike chini. President should not a amember of Parliament. Presidential election iwe na siku yake na Parliament na Local Authority iwe siku yake. President should not be above the law. Kila mmoja hapa Kenya awe chini ya sheria ili akifanya makosa apelekwe kortini.

Judiciary iwe independent.

**Com Salome Muigai:** Thirty seconds mum,

**Alicen Chelaite:** Niko na mingi

**Com. Salome Muigai:** Utaleta memorandum, tutaisoma.

**Alicen Chelaite**: Sina momorandum nilitaka tu………..

**Com. Salome Muigai**: Iaandike tafadhali utupatie.

**Alicen Chelaite:** Asante basi, Judicial iwe independent, President asi-appoint judges, family courts be established in divisional level na wakina mama judges na wanaume wawe huko ili wamama waweze kusima maneno yao bila uoga.

There is need for Constitutional courts in these Country. Local Authority act 255 be rebuild. Kwa sababu ile iko ilikuwa ni ya wazungu. Mayors, Chairmen be elected. Salaries ya Councillors itoke kwa mfuko ya serikali na isiwe ya Local Authority. Local Authority be decentralized na wapewe powers. Ile package ya Kenya one third iwe shared within the Local Authorities.

**Com. Salome Muigai**: Thank you very much Alicen……..

**Alicen Chelaite**: I have only one for the commttes ya road, busaries…….Intejection by Com.

**Com.Salome Muigai :** That is one for the roads. Do that one for the roads.

**Alicen Chelaite**: Thank you for being kind to me. Haya nimesema ya kwamba kuna pesa inapewa wanchi ya barabara, HIV Aids, bursary, ya latrines ile ya local authority ile pesa imekuwa misused. Kuwe na Committee itakayo kuwa Constitutionalized, ili wananchi wenyewe waone hiyo pesa imefanya kazi. Madam Chairman, asante sana. Mungu awabariki lakini nilikuwa na pengi lakini hiyo inatosha.

**Com. Salome Muigai:** Ninajua wewe una mengi lakini asante sana. Peter Wabugu.

**Alicen Chelaite**: Hakuna question hata moja?

**Com. Salome Muigai:** Nikikuhuliza swali moja utaniba majibu ya another three minutes. Alicen ninakujua. Asante sana umejieleza wasi wasi.

**Peter Wabungu**: Kwa majina ni Peter Mwangi Wabungu. Ningependekeza kuanza na area zile hasina security. Wenye wanakaa area hizo wakubaliwe kuwa na silaha. Wakati mwingi tunapoteza kwa kufuata watu ambao wana silaha tukiwa mikono mitubu. Na hata tukiwafuata na kuwashika hatunanjia ya kuwanyang'anya zile vitu vyetu walizo iba., kwa maana wao wako na silaha na sisi hatuna chochote.

La Pili ningetaka wakati wa retire ma-officer wa serikali wasiondoke kwa office bila kupatiwa pension yao. Wakikubali kuondoka inakuwa shida na mtu anaenda hata miaka kumi.

Employment: Kulingana na qualifications, tunaonelea kuna watu wako na kiwango cha chini kwa upande wa masomo na wanapatiwa mishahara ya juu na pia kuna wengi wanamasomo ya juu, kwa hivyo kazi ilingane na qualifications. Na hata mishahara ilingane pia. Na haya maneno ndio inaleta mikomo mingi kwenye mashule.

Jambo lingine ni National youth service. Ningependelea na ningependekeza sana watoto wetu wakitoka shuleni, wapatie kwa National Youth Service wote na liwe jambo la lazima. Na serikali iwatafutie kazi wakimaliza ile course watakayofanya kwa national youth service. Serikali isiwawachie ati wakimaliza hiyo course ati wajitafutie kazi, watatafuta wapi na hawana employment experience.

Jambo lingine ni uhuru wa kuishi kila pahali mtu anataka akiwa ni Mkenya. Kusiwe na mpaka wa native reserves. Mtu akitaka nunua shamba iwe ananunua Coast ama Nyanza ama wapi, iwe wazi. Bora kipande yake iseme yeye ni Mkenya apatiwe haki ya kuishi bahali anataka. Hii native reserve ndiyo inaendesha mambo ya ukabila. Na ndiyo inaleta clashes.

**Com. Salome Muigai**: Point ya mwisho Mzee

**Peter Wabungu:** Wasio jiweza walishwe na serikali, ni jambo la haibu kuona wasio jiweza wakiomba Katika matown yetu na serikali yetu iko huru. Kwa hivy iwe jukumu la Serikali kuwasimamia na wakulima wa hekari moja tafadhalini wapewe loan facilities. Na iwe…………(inaudible) na kukiwa na kiangazi wangaliwe ili wasipotesa.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Mzee. Daniel Muteo. Anza na jina lako.

**Daniel Muteo:** Daniel Kwa majina ninaitwa Daniel Muteo. Niko na memorandum lakini taweka nguvu kidogo.

Kwa uapnde wa serikali, ningepndea mikono mitatu ya serikali ifanye kazi bila kuigiliwa ama ifanya kazi bila kuingilia sehemu za yule mwingine.

Ingine ni upande wa watumishi wa serikali, Kwa mafano kama Ma-chief na hata Ma-Do, wangetoka kutoka kwa wananchi. Namahanisha kwamba wachaguliwe kama wabuNge. Tena ningeomba tuwe na vote of no confidence kwa WabuNge wetu na Ma-councillors. Kama wakifanya kazi mbaya tuapatiwe ruhusa ya kuwang’oa na kuweka wengine.

Upande wa walemavu ningeoba Katiba mpya iweze kushughulikia sana watu ambao hawezi. Yaani serikali iweze kuangalia mambo yao kama ni masomo, wasomeshwe bure na hata wapatiwe course na mwishowe wahajiriwe kama wafanyi kazi. Tena masomo ya msingi na vioo vikuu iwe ya bure.

Kuna mambo mengine ambayo inahusu mambo ya unyanyazaji wa watoto. Tunasikia watoto wajanga wanaendelea kunyanyazwa, wanatetendewa maovu mabaya mabaya kama kunajisiwa naomba Katiba ambayo tunatengeneza kwa sasa, yeyote ambaye atapatikana akiwa amefanya madhambi kama hayo, achukuliwe sheria kali. Yaani afungwe na asifungwe chini ya miaka kumi.

Tena wakina mama wapatiwe nafasi katika uongozi. Upande wa kuabudu ningependa tumuabudu Mungu tu ambaye ni muumba wa Mbingu na Dunia. Tena katika nchi yetu ya Kenya, tunaomba kuwa tusiwe na masquaters kwa sababu wananchi waote walipikani uhuru ili wawese kuishi katika nchi yao kwa starehe. Asante.

**Com. Saloem Muigai:** Umemaliza kabla sijakupa onyo. Asante. Peter Murethi. Uko?

**Peter Murethi:** Mimi ni Peter Murethi kama umeniita. Jambo la kwanza ambalo ningependekeza ni kwamba wakati tumefikia kwa uchaguzi, watu kama Wabunge hata President Wote wawe wakistep down. Hivyo ninamanisha kwamba Commission iwe ikisimamia serikali. Ndio President asiweze kuwa na power ya kuamrisha wakati wa uchakuzi.

Jambo la pili ni kwamba kuwe na sheria ambayo inasimamia hali ya mti na haswa kwa ma-forests. Kwa maana mti ile tunapanda kwa mashamba yetu, hiyo ndio imewekewa maanani sasa ati tuwe tukichukua permit za kutumia miti yetu huku mashambani. Kwa hivyo mtu akitaka kujenga huwezi kujenga wakati hufao kwa sababu ni lazima utafute permit.

Jambo la lingine ni kwamba wakati budget inasomwa na pesa sinatolewa, siwe kwanza sikienda kwa yale mambo ya muhimu anayohuzu raia. Kwa mfano, kwa upande wa education, madawa na upande wa defence. Yale mambo ya muhimu kabisa, ndio ile pesa ingine ikikosekana iwe raia hawatatezeka.

Ni hayo tu asante.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana Bwana Murethi kwa kulenga mambo yako. Samuel Too. Samuel Arap Too. Okay.

**Samuel Arap Too:** Kwa jina ninaitwa Samuel Arap Too. Mimi ningependa katika Katiba, wauzishwe wazee wa mitaa. Na serikali iwalipe kwa ile kazi ambayo wanafanya. Kwa sababu gani? Kwa sababu hawa wazee wanafanya kazi na wanasaidia watu nyumbani kutatua shida zao. Kama kuna kesi ya mashamba, hawa wazee wahusishwe. Kwa sababu wanaelewa undani kati ya wale wenye shamba na yule ambaye anaingilia.

Pili, ningependa serikali iajiri watu ki-contract ili kila mtu aweze kuwa na sehemu ambayo atahusika.

Tatu, ningependa sehemu ya mahakama, ukiangalie vile mahakama ya Kenya iko, inasehemu ambapo mwananchi wa kawaida, kama hauna pesa hauwezi kuparticipate katika korti. Kwa hivyo iwe rahisi ya kwamba mimi nikiwa na shida na niwe kukushitaki kesi kortini, iwe ni irahisishwe kuliko ikaae mweizi moja pili hati miaka mitatu au mininne. Inanikarimu mimi ambaye sina pesa kwa hiyo process.

La tatu, kamati ya tribunal, ambao huwa ndio wanahusika kwa upande wa mashamba na dalaka. Kusiwe inafanyiwa mbali na sehemu ambao kitendo hicho kinafanyika. Isiewe tu katika hali ya korti ama kwa DC iwe katika hali ya nchini. Ije hata kama office ya Chief ama katika sehemu ambazo inawezekana mtu wa kawaida kufika. Ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana Arap Too. Joseph Wang'ombe. Titus Amusama, Titu Amuzama. Anza na jina

lako.

**Titus Amusama**: Ninaitwa Titus Amusama

**Com. Salome Muigai:** Uzungumzie kwenya microphone ndio tupape ku-record.

**Tutus Amusama:** Mimi ninaitwa Titus Asirengu Amzama. Niko na Memorandum hapa lakini mpaka niisome. Kwa sababu mpaka nirudi na nakili mahali ninakuwa kwa sababu ni collective.

**Com. Salome Muigai:** Una dakika mbili kwa hivyo pahali utakuwa umefikisha, nitakusimamisha. Endelea.

**Titus Amusama**: Ukinisimamisha itakuwa haina maana kwa sababu kwa sababu kwa sababu niende na nakili. Ninaomba.

**Com. Salome Muigai**: Endelea.

**Titus Amusama:** Ya kwanza ni kuhuzu Bunge. Kipengele cha kwanza, Commission should be elected by kuna Tume ambayo huwainaundwa. Inafaa iwe elected by the Parliament sio President.

Kipengele cha pili, wabuge all ministers should taxed salary wise and also their business checked for taxes. Yaani biashara zao singaliwe kwa ushuru.

Any payment to MP's should be given to those who have fully participated in the National Assembly in Parlaiment.

Nominated MP's or Councillor to be those have not contested in any seat and Presidential powers should be limited.

Kuhuzu judiciary kuna haya mambo ya kuhuzu vifungo. Sentence of criminals of small offences should do community work. E.g stealing chicken, clothes or low value goods should be under communal work.

To defend cases in court limited time should be issued by the court so as to a void victimization or cunning lawyers or people. Kuna watu wanakaa sana kortini na kesi inakaa muda marefu.

Ineffective judges who postphone cases for any long time should be acused or be prosecuted also be discouraged.

Law enforcer who fail do so to be highly charged.

Kuhuzu afya, health, smoking in public should be forbidden and government to provide free medical services to the poor. For Private licenses……interjection by **Com. Githu Muigai.**

**Com. Salome Muigai:** You have another thirty seconds.

**Titus Amusama:** For private hospital license to be highly charged so as to enable poor people to enjoy medical services.

Military people should not be allowed to harass people in any form. E.g. beating them, abusing them or anything. Any Kenya or person in Kenya having more than one million in his or her account should be taxed yearly,

No person or groups of people to have foreign accounts from their source Kenya business or work.

**Com. Salome Muigai**: Last point.

**Titus Amusama:** Land lords or land ladies to be taxed yearly. Most of them do not have licences.

**Com. Salome Muigai**: Thank you very much. Peana memorandum yako tutaisoma neno kwa neno. Nakufika hapo nimefika mwisho wa orodha ya majina ya watu waliyo jiandikisha kuzungumza. Sijui kama kuna mwingine. Ulikuwa umejiandikisaha, wewe mzee ulikuwa umejiandikisha? Na nani mwingine nimeona mkono juu, si tayari umeshazungumza ? unasikia kuna wengine hawajapata nafasi ya kwanza kwa hivyo nitakupa dakika moja na nusu na mzee nitampa dakika mbili kwa ajili ya umri. Unaona hiyi kinjwa yake ni tofauri na yako?

**Patrick Gichuki Mwaura:** Tafadhali Madam Commissioner……..…intejection by Com. Salaome Muigai

**Com. Salome Muigai**: Wengine niwapa dakika mbili na wewe umechelewa, ninakupa dakakia moja unusu.

**Patrick Gichuki Mwaura**: Nilikuwa hapa na niakaomba ruhusa nikiwa na Councillor tuende tukahairishe mambo ya harambee.

**Com. Salome Muigai**: Kwa ungekuwa tayari umeanza maoni yako.

**Patrick Guchuki Mwaura:** Asante sana Madama Commissioner, kwa majina mimi ni Patrick Gichuki Mwaura, na mkazi wa hapa.

Jambo la kwanza amablo halijazungumziwa ndilo ninataka kuongea juu ya kwanza. Ni supremacy of the Constituion.

Constitution yetu iwe na Kipengele ambacho kinaiba nguvu. Kiasi kwamba hakuna yeyote yule yeyote anaweza kuibadilisha.

La pili. Bunge letu liwe na uhuru wa kutosha. Raisi asiwe na mamulaka ya kukutaa jambo lolote ambalo limejadiliwa Bungeni.

Nguvu ya raisi ipunguzwe, kiasi kwamba asitumie uwezo ambao anautumia wakati huu, hii office ambayo inatumia kuwadhulumu wananchi.

Elections, maoni yangu yanasema kwamba kuhuzu uchaguzi ya kwamba serikali iwahakikishe wakombea viti vya ubunge na urais, usalama, wapewe askari wasio sidi sita kulinda compaign zao, hao askari wawe na katabu kinachiidwa campaign events occurance book. Ambacho kwa hiyo kitabu wanaandika chochote kinachotokea kuhuzu uchaguzi. Ili tuwe na uchaguzi ambao hauna fujo na vita na nini.

Aridhi, aliyezaliwa Kenya awe na haki ya kurithi aridhi kabisa lakini raia ambaye anaomba kumiliki uraia hapa Kenya asiwe na haki yakuwa na aridhi yeyote katika Kenya.

Gender: Wanawake na waume watumiwe kisawa katika ukawaji wa uongozi elimu na kadhalika. Hasa katika Bunge tuwe na tuluthi moja ya akina mama katika bunge. Provincia Administration, tuwe na Provincial Administration lakini tuondolewe ma-chief na manaibu wao.

DO afanye kazi hiyo akiwa na councilor wa ineo hilo. Ma-Chief wengi na manaibu waoa ula mishahara yao. Mbunge ama Councillor asipotimiza wajibu wake na kufanya kazi kuligana na matakwa ya wale waliyo mchagua. Wanachi wana haki ya kumregesha nyumbani. Kuwe na tume ambayo itaangaliwe ambayo matakwa yao yatapelekwa huko.

**Com. Salome Muigai:** Two last points.

**Patrick Gichuki Mwaura:** Kwa hivyo tuwe na haki ya kumrekesha mbunge nyumbani. Yeyote atakaye pita uchaguzi ambaye ameshida ni lazima awe na 51% and above. No extention of Parliment at all costs. Kiongozi ameaba kulinda Katiba. Kama Katiba yetu inasema kuwe na miaka mitano ya wabunge kwa hivyo hakuna extetion. Kuvunjwa kwa bunge Rais asiwe na nguvu, tuwe na kalanda ya bunge ambayo inasema bunge inasitahili kuvunjwa lini na uchaguzi ni wa lini.

Hali ya marriage, katika pupolation ya Kenya akina mama ni wengi kuliko wanaume. Mimi kama Patrick Njunge, Nikitaka kuwe na wanawake wawili wote wawe na kibali cha kusema ya kwamba wako na certificate ya kuwe wote ni bibi zangu. Kwa hayo machache ama mengi, nawatakia heri. Asanteni.

**Com Salome Muigai:** Asante sana mzee nawe nakupa dakika mbili.

**Paul Ngungi Kangu'**: Kwa majina ni Paul Ngugi Kangu na nitaenda haraka. Nitanzaia freedom whorship. Ninapendekeza freedom of whorship in Kenya………interjection by **Com. Salome Muigai**

**Com. Salome Muigai:** Umetuambia jina lako Mzee?

**Paul Ngungi Kangu':** Nimesema Paul Ngugi Kang'u. Na ninahanzia kwa number moja ni freedom of whoship. Katiba ikubali kuabudu Mungu Ambaye ni wabinguni . Yaani kuna freedom of whorship na wengene wanaabudu makanisa ambayo ni ya kishetani.

**Com. Salome Muigai**: Endelee Mzee sasa tumeelewe, endelea tu kutupa mapendekezo yako.

**Paul Ngungi Kangu':** Number ya pili ni will of a man, iwe kama vile alivyoandika akiwa hai, hata akifariki, iwe ndiyo itatumika. Hiyo ni ya mambo ya nyumbani.

Number nne ni hali ya mashamba, pasiwe na mtu ambaye atakuwa na hekari ya over one hundred hectares, Iwe maximum. Kwa sababu kuna watu wengine wanamashamba makubwa sana na wengine hawana.

Na ingine ni mambo ya Rongai Constituency, ni very large na ningependekeza katika Katiba iwe pili. Kwa sababu ni very large. Na ingine ni ya President. Presidential prorogative imekuwa, wale watu ambao walikuwa wakiapointee na President, wapelekwe katika Parliament na wawe wakiithinishwa na Parliament. Kuhuzu prorogative iwe imegawanywa na watu wale wamechaguliwa na wanachi.

Na pahali per tree in farms ya wanachi, point pili za mwisho. ..

**Com. Salome Muigai**: Maneno mawili ya mwisho.

**Paul Kungi Kangu**: Trees in the farms of people yaani mashama ya watu ninaona katika area zote katika replic, watu wamedharau mambo ya kupanda mti kwa sababu ukipanda mti unenda kuchukua permint. Kwa hivyo ninaona hakuna haja ya kupanda mti. Kwa hivyo watu wakupaliwe in law kupanda mti lakini wawe na uhuru wa kusikata. Kwa sababu wanajua ni yake na atakata kwa kiwango kile anataka.

Basi ya Mwisho nui mambo ya councillors ana Chairmen wa wa council wawe wakiwa direct elected by the people.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana mzee . Kufikia hapa nimefika mwisho wa kikao hiki cha Tume ya Marakebisho ya Katiba ya kikao hiki kinyekilikuwa cha Rongai Constituency hapa Kivoronjo na kabala hatujamaliza huu makutano ningetaka

kuwashukuru sana wakaaji wa hapa kwa ajili ya kutukaribisha na kukaa nazi, kuwajaa kazi nyingi mkaja kutueleza mambo yenye mngetaka kuona kwenya Katiba ijayo. Ningetaka pia kumshukuru Bwana MP na Tume, ambao watupa soda tukanywa, na tungetaka kuwashuru sana na pia ningetaka kuwashukur wakaaji wa hapa wenye wametulisha.

Tunashukuru na pia wafanyi kazi wetu na watu wenye wamejaribu sana kufanyia kazi hii mitambo yenye imekuwa na shida shida mpaka mwishoni wakaweza kutoboa na ikafanya kazi, tunataka kwashukuru sana. Na mwisho ningetaka kumshukuru mwenye kiti wangu wa kikao hiki Bwana Ratanya na pia Raiji mwenye ilimbidi kwenda kabla ya wakati. Na mimi Salaome Wairimu Muigai na washukuru sana.

Na ningetaka kumuomba mmoja wenue atufungie nakwa maombi. Mzee unataka kuomba. Unatoa maoni kwa Mungu aliye hai na hiyo ni maoni makubwa mzee. Endelee Mzee.

**Peter Kamau**; Asante sana Peter Kamau katika shamba hili la Naymamithi sub-location, Oserious Location. Turudishie Mungu Shukrani.

Mungu baba tunajiweka mbele yako wakati huu wa njioni kwa mambo mengi ambayo tumetoa na pia kwa wageni ambao ulituleta ili tuweze kuunda Katiba Mpya. Yote tunayaweka mbele yako tukijua ya kwamba utawarudisha salama salamini na yote tuliyoyatoa katika kikao hiki tunaingojea siku ya pili tutaipata. Hasa ikaendesha katika Kenya yetu kwa jumla. Ikilinganishwa na iningine ambayo imetolewa kila bahali itakuwa ya kunda umpya Kenya yetu. Ndio kila moja wetu awe na furaha kwa kazi njema aliyofanya. Kwa hayo yote tumetenda katika kikao tunakuomba uwe kiongozi mwema na uwe chairman wa kikao hiki. Yote tunamaliza kwa jina lako. Na tunajua ya kwamba wangeni wetu watarudi salama salamini utawaongoza katika mwendo wa mabarabara kwa sababu wanatumia magari ambayo imetenezwa na binadamu. Na wafika nyumbani tutakurudishia Mungu shukrani tukisikia walifika salama wa salamini. Tunaomba kwa hayo machache katika jina la yesu alye Mungu na Mwokozi wetu.

Amina.

**Com. Salome Muigai:** Kwaherini na Mungu awabariki.

**The Meeting closed at 5.00 pm.**

&&&&&&&&&&